



**KUAWEZESHA VIONGOZI WA KANISA
•AFRIKA MASHARIKI•**

MARKO—SEHEMU YA 2

Mwandishi

Jonathan M. Menn

**B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974
J.D., Kornell Law School, 1977
M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007**

**Equipping Church Leaders East Africa, Inc.
714 S. Summit St., Appleton, WI 54914
+1-920-2846841 (mobile and WhatsApp)
jonathanmenn@yahoo.com
www.eclea.net**

2021

Wanazuoni wengi wanafikiri Marko ndiyo injili ya kwanza kuandikwa. Baba wa imani Papias anataja uandishi wa kitabu hiki kuwa wa Marko, na anasema taarifa zake alizipata kutoka kwa Petro mtume. Hilo halikutiliwa shaka na kanisa la kwanza, na hata taarifa mbalimbali zinaonesha hivyo. Kitabu hiki ni cha kivitendo. Ni moja ya injili zenyenye kufanana (synoptic) zingine zikiwa ni pamoja na Mathayo na Luka, kwasababu injili hizi tatu zina simulizi nyingi zinazofanana, katika mtiririko ule ule, na mara kwa mara kutumia maneno yale yale. Ingawa ndicho kitabu kidogo kuliko injili zingine, mara nyingi kinatoa simulizi za kina, zenyenye desturi za Kiyahudi zilizotolewa maelezo kwa ajili ya Wamataifa wasomaji. Marko anaonesha jinsi Yesu anavyotimiza unabii wa AK wa Masihi ajaye na, kama Marko anavyoeleza katika mistari ya kwanza kabisa ni, “Mwana wa Mungu.”

YALIYOMO

I. Utangulizi.....	75
A. Mukhtasari.....	75
B. Sehemu za kitabu.....	75
II. Ufanuzi wa Marko.....	77
8:27-33: Kuwekwa wazi kwa utambulisho wa maisha ya Yesu.....	77
9:1-13: Kubadilika sura.....	81
9:14-29: Yesu anamponya kijana aliyepagawa na pepo.....	83
9:30-50: Yesu anafundisha kuhusu kifo chake, ufufuo, na uanafunzi.....	84
10:1-12: Yesu afundisha kuhusu talaka.....	87
10:13-16: Yesu anawabariki watoto wadogo.....	88
10:17-31: Yesu na kijana tajiri.....	89
10:32-45: Kwa mara nyingine Yesu anazungumzia kufu na kufufuka kwake na asili ya uanafunzi.....	92
10:46-52: Yesu amponya Batimayo kipofu.....	94
11:1-11: Kuingia Yerusalem kwa ushindi.....	94
11:12-26: Ishara za Umasihi wa Yesu: Yesu analaani mtini na kulitakasa hekalu....	95
11:27-33: Asili ya mamlaka yaje yatiliwa shaka.....	98
12:1-12: Mfano wa mkulima wa zabibu.....	99
12:13-17: “Yaliyo ya Mungu, mpeni Mungu”.....	99
12:18-27: Maisha katika ufufuo.....	100
12:28-34: Amri iliyo kuu.....	101
12:35-37: Kristo ni Bwana.....	102
12:38-40: Onyo dhidi ya unafiki wa Waandishi.....	104
12:41-44: Senti mbili za Mjane.....	105
13:1-37: Hotuba ya Mlima wa Mizeituni.....	105
14:1-11: Yesu anapakwa marashai ya gharama.....	112
14:12-31: Chakula cha mwisho cha jioni.....	115
14:32-42: Katika Bustani ya Gethsemane.....	119
14:43-15:20a: Kusalitiwa kwa Yesu, kukamatwa, kusimama mbele ya baraza, Petro amkana Yesu, na kushitakiwa mbele ya Pilato.....	121
15:20b-47: Kusulubiwa, kufa, na kuzikwa kwa Yesu.....	128
16:1-8: Ufufuo.....	134
16:9-20: Kuonekana kwa Yesu baada ya kufufuka.....	136
BIBLIOGRAFIA.....	139
MWANDISHI.....	144

I. Utangulizi

A. *Mukhtasari*

Sehemu ya pili ya kitabu cha Marko, **8:27–16:20**, inaangalia safari ya kwenda Yerusalem na kuendelea. Inahusisha kuwekwa wazi utambulisho wa Yesu kama Masihi; utabiri kuhusu kifo chake, ufuluo, na kurudi kwake mara ya pili; Kubadilika sura; mafundisho na uponyaji; huduma yake kule Yerusalem; kusalitiwa; kukamatwa, kusulubiwa, kuzikwa, na kufufuka.

B. *Sehemu za kitabu*

Kitabu hiki kimepangiliwa katika sehemu zifuatazo:

I. Utangulizi (1:1-13)

- A. Huduma ya Yoh Mbatizaji (1:1-8)
- B. Ubatizo wa Yesu (1:9-11)
- C. Kujaribiwa na Shetani (1:12-13)

II. Huduma ya Yesu Galilaya (1:14–8:26)

- A. Kutangaza ufalme (1:14-15)
- B. Kuita wale kumi na wawili (1:16-20)
- C. Uponyaji na kutoa pepo (1:21-45)
 - 1. Yesu anafundisha katika sinagogi na kumponya mtu aliyejikuwa na pepo (1:21-28)
 - 2. Anamponya Mkwe wa Petro (1:29-31)
 - 3. Anaponya watu wengi waliopagawa na pepo na wagonjwa (1:32-34)
 - 4. Yesu anahubiri kule galilaya (1:35-39)
 - 5. Kuponywa kwa Mkoma (1:40-45)
- D. Kupingwa kwa Yesu kunaanza na kupata nguvu (2:1-3:6)
 - 1. Yesu anamponya aliyepooza (2:1-12)
 - 2. Kuitwa kwa Lawi (Mathayo) (2:13-17)
 - 3. Yesu na kufunga: umuhimu wa Kristo (2:18-22)
 - 4. Yesu na Sabato (2:23-3:6)
 - a. Kula masuke siku ya Sabato (2:23-28)
 - b. Yesu anaponya siku ya Sabato (3:1-6)
- E. Yesu anawaponya wengi waliokuwa hawawezi na wenye pepo wachafu (3:7-12)
- F. Kuchaguliwa kwa kumi na wawili (3:13-19)
- G. Kutokuamini, upinzani, na familia ya kweli ya Kristo (3:20-35)
 - 1. Familia ya kidunia ya Yesu wanafikiri ana wazimu (3:20-21)
 - 2. Waandishi wanamtuhumu Yesu kuwa amepagawa na pepo (3:22-30)
 - 3. Kristo anabainisha familia yake ya kweli (3:31-35)
- I. Yesu anafundisha kwa mifano (4:1-34)
 - 1. Mfano wa mpanzi na aina za udongo (4:1-20)
 - 2. Kilichofichika kitafunuliwa, na kwa kipimo upimacho utahukumiwa (4:21-25)
 - 3. Mfano wa mbegu, kukua, na mavuno (4:26-29)
 - 4. Mfano wa mbegu ya haradali (4:30-34)
- J. Yesu atuliza bahari (4:35-41)
- K. Kutoa pepo na uponyaji (5:1-43)
 - 1. Mgerasi mwenye pepo (5:1-20)
 - 2. Binti Yairo na mwanamke aliyetokwa damu (5:21-43)
- L. Yesu kule Nazareth (6:1-6)
- M. Wale kumi na wawili wanatumwa na kurudi (6:7-13, 30-32)
- N. Hatma ya Yoh Mbatizaji (6:14-29)
- O. Miujiza: kulisha watu 5,000; Yesu kutembea juu ya maji; na uponyaji (6:33-56)
 - 1. Kulishwa 5000 (6:33-44)
 - 2. Yesu kutembea juu ya maji (6:45-52)
 - 3. Uponyaji kule Genesareti (6:53-56)
- P. Mapokeo na utambulisho wa watu (7:1-23)
 - 1. Yesu anapingana na Mafarisayo juu ya mapokeo (7:1-13)
 - 2. Yesu anasema kuwa unajisi unatoka ndani (7:14-23)

Q. Anatambulisha huduma kwa mataifa (7:24–8:10)

1. Kumtoa pepo binti wa mama Msirofoenike kule Tiro (7:24-30)
2. Uponyaji wa Kiziwi Dekapoli (7:31-37)
3. kulishwa watu 4000 Dekapoli (8:1-10)

R. Kujaribiwa, kutokufahamu, na uponyaji (8:11-26)

1. Mafarisayo wanaomba ishara (8:11-13)
2. Wanafunzi washindwa kuelewa (8:14-21)
3. Kuponywa kwa mtu kipofu (8:22-26)

III. Utambilisho wa Yesu na hatma yake vinafunuliwa (8:27–9:13)

- A. Yesu ndiye Masihi (Kristo) (8:27-30)
- B. Yesu atauwawa lakini atafufuka tena (8:31-33)
- C. Gharama ya uanafunzi (8:34-38)
- D. Kubadilika sura (9:1-13)

IV. Njia ya kwenda Yerusalem (9:14–14:9)

- A. Yesu anamponya kijana aliyepagawa na pepo (9:14-29)
- B. Yesu anafundisha kuhusu kifo chake/ufufuo, uanafunzi, na talaka (9:30–10:16)
 1. Yesu atabiri kufa na kufufuka kwake (9:30-32)
 2. Nani aliye mkuu zaidi katika Ufalme (9:33-37)
 3. Asili ya uanafunzi (9:38-50)
 4. Yesu anafundisha kuhusu talaka (10:1-12)
 4. Yesu anawabariki watoto wadogo (10:13-16)
- C. Mtawala kijana tajiri (10:17-31)
- D. Mafundisho kuhusu kifo chake/ufufuo na uanafunzi (10:32-45)
 1. Kwa mara nyingine Yesu anatabiri kufa na kufufuka kwake (10:32-34)
 2. Yakobo na Yoh wanataka kupewa kipaumbele (10:35-40)
 3. Asili ya uanafunzi wa kweli na msingi wa kupata kipaumbele (10:41-45)
- E. Kuingia Yerusalem (10:46–11:11)
 1. Yesu amponya Batimayo kipofu akiwa njiani kuelekea Yerusalem (10:46-52)
 2. Kuingia Yerusalem kwa msafara wa ushindi (11:1-11)

V. Huduma ya Yesu kule Yerusalem (11:12–13:37)

- A. Ishara za umasihi wa Yesu (11:12-26)
 1. Kulaani mtini (11:12-14, 20-26)
 2. Kufukuza wabertilishi wa pesa hekaluni 1:15-19)
- B. Mamlaka ya Yesu, mifano, na mafundisho (11:27-12:44)
 1. Asili ya mamlaka ya Yesu yatliwa shaka (11:27-33)
 2. Mfano wa wakulima wa mizabibu (12:1-12)
 3. “Yaliyo ya Mungu Mpeni Mungu” (12:13-17)
 4. Ufufuo na ndoa katika ufufuo (12:18-27)
 5. Amri iliyo kuu (12:28-34)
 6. Kristo ndiye Bwana (12:35-37)
 7. Onyo dhidi ya unafiki wa waandishi (12:38-40)
 8. senti mbili ya mjane (12:41-44)
- C. Mafundisho katika mlima wa mizeituni (13:1-37)

VI. Maandalizi ya kufa; Kusalitiwa; kusulubiwa; na kufufuka (14:1–16:20)

- A. Yesu apakwa marashi ya gharama (14:1-9)
- B. Yuda kumsaliti Yesu (14:10-11)
- C. Chakula cha mwisho cha jioni (14:12-31)
- D. Katika Bustani ya Gethsemane (14:32-42)
- E. Kusalitiwa kwa Yesu na kukamatwa (14:43-52)
- F. Kushtakiwa mbele ya Sanhedrin na Pontio Pilato (14:53–15:20)
 1. Sanhedrin (14:53-72)
 2. Pontio Pilato (15:1-15)
 3. Kudhihakiwa na askari (15:16-20a)

- G. Kusulubishwa na kuzikwa (**15:20b-47**)
- H. Kufufuka (**16:1-8**)
- I. Kuonekana baada ya kufufuka (**16:9-20**)

III. Ufanuzi wa Marko

8:27-33:²⁷ *Akatoka Yesu na wanafunzi wake, wakaenda kwenye vijiji vyta Kaisaria-Filipi; na njiani akawauliza wanafunzi wake, akasema, Watu huninena mimi kuwa ni nani?*²⁸ *Wakamjibu, Yoh Mbati zaji; wengine, Eliya; wengine, Mmojawapo wa manabii.*²⁹ *Naye akawauliza, Na ninyi mnasema ya kuwa mimi ni nani? Petro akamjibu, akamwambia, Wewe ndiwe Kristo.*³⁰ *Akawaonya wasimwambie mtu habari zake.*

³¹ *Akaanza kuwafundisha kwamba imempasa Mwana wa Adamu kupatikana na mateso mengi, na kukataliwa na wazee, na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na baada ya siku tatu kufufuka.*³² *Naye alikuwa akinena neno hilo waziwazi. Petro akamchukua, akaanza kumkemea.*

³³ *Akageuka, akawatazama wanafunzi wake, akamkemea Petro, akasema, Nenda nyuma yangu, Shetani; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu*

³⁴ *Akawaita mkutano pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, Mtu ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike na msalaba wake, anifuate.*³⁵ *Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakaye iangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha.*³⁶ *Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake?*

³⁷ *Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake?*³⁸ *Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu, katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.”*

mst. 27-38—Kuwekwa wazi kwa Utambulisho na misheni ya Yesu

Katika kitabu cha Marko sehemu hii inaonesha umuhimu wa maelezo ya Yesu kuhusu hatma ya misheni yake. Kwa uwazi Mungu anawafunulia wanafunzi kwamba Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa, mwana wa Mungu. Hata hivyo, pamoja na ufunuo huo, wanafunzi hawaelewi misheni ya Masihi inahusu nini. Yesu anaelezea kwamba, kinyume na matarajio yao, alama kuu itakuwa ni pamoja na mateso, kukataliwa, na kifo chake, lakini baada ya hayo kufufuka na uhai mpya. Misheni hii, kwa upande mwingine ni kitovu cha maelezo yake katika **mst. 34-38** juu ya namna gani maisha yetu yanapaswa kuwa kama tunaweza kuwa wafuasi wake.

1. mst. 27-30—Yesu ndiye Masihi

Wakati tukio hili ndilo la kwanza katika sehemu ya pili ya kitabu cha Marko lina mengi yanayokwenda sambamba na kuponywa kwa mtu kipofu kulikotokea katika **mst. 22-26**: yote inaanza na kutaja mazingira (**mst. 22, 27**); mtu kipofu na watu waliokuwa na uwezo mdogo wa kuona au uelewa (**mst. 23-24, 28**; yaani, watu wanamfikiria Yesu kama nabii mku tu, lakini siyo Mwana wa Mungu); kipofu anapata kuona kikamilifu na wanafunzi nao wanaelewa vema kwamba Yesu ni Masihi (**mst. 25, 29**); wote, mtu aliyekuwa kipofu awali na wanafunzi wanaagizwa wasimwambie mtu kilichotokea na uzefu wao mpya. (**mst. 26, 30**).

Kaisaria Filipi ulikuwa mbali kaskazini mwa Galilaya, na “marabi waliuchukulia kama ndio mpaka wa nchi takatifu na nchi ya wamataifa” (Cole 1989: 201n.1). “Hapo awali mji huu uliitwa Paneas . . . kwa heshima ya mungu wa kirumi aliyeitwa Pan, ambaye kaburi lake lilikuwepo huko” (Wessel 1984: 692). Yesu alichagua mahali hapa kujifunua kwa wazi kama Masihi na Mwana wa Mungu, kwa kuwa “kwa lugha ya alama anatangazia wale waliokuwa na macho waone . . . kwamba anadai ubwana wake juu ya nguvu ya Wapagani na Wayahudi walioshindana na dunia” (Gruenler 1989: 781).

Yesu alipouliza, “*Watu wanadhani mimi ni nani?*” (**mst. 27**), majibu yalikuwa sawa na yale ambayo herode na wengine walifikiri Yesu ni nani (angalia **6:14-16**), wakimaanisha, nabii mkuu. Wakati ni kweli hasa kwamba Yesu alikuwa nabii, hakuwa nabii *tu*, wala hakuwa mtu *tu*. Herode na watu wengine walikosea katika kumfikiria Yesu kama kiongozi mwingine tu wakati yeye ndiye mwisho wa yote—ambaye waliomtangulia wote walimnena huyo. Ukiri wa Petro, “*Wewe ndiwe Kristo*” (**mst. 29**) unaonesha kuwa hatimaye wanafunzi walielewa Yesu alikuwa nani “Kristo” kwa Kigiriki ni sawa na neno la Kiebrania “Masihi.” Maelezo ya Mathayo juu ya hili anaongeza mambo kadhaa ya kina “Akawaambia, Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu, akamwambia, Heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni.” (**Mat 16:15-17**) Petro alikuwa anaonesha kumtambua Yesu Masihi

alikuwa zaidi ya mtu; alikuwa Mungu kabisa na pia mtu kabisa. Yesu alikuwa anaonesha kuwa maarifa aliyopata hayakuwa yake, lakini yalikuwa yamefunuliwa na Mungu. Yesu kuwaagiza katika **mst. 30** kwamba wasimwambie yeyote kwamba alikuwa Kristo huenda ilikuwa ni kwasababu ilikuwa dhahiri kwamba hawakujua misheni ya masihi duniani kama tutakavyoona katika **mst. 31-33**). Uelewa wenye makosa kuhusu Yesu ni nani na ufalme wake yote hupeleke matokeo yasiyo sawa na kumfuata kimakosa, kama Yesu atakavyoweka wazi katika **mst. 34-38**.

2. **mst. 31-33—Yesu atauwawa lakini atafufuka tena**

Mistari 31 ni mwenzake na **mst. 29; mst. 31** unealezea umasihi wa Yesu una sifa zipi: “*Akaanza kuwafundisha kwamba imempasa Mwana wa Adamu kupatikana na mateso mengi, na kukataliwa na wazee, na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na baada ya siku tatu kufufuka.*”⁴⁰ Kuna vitu vingi vya ushahidi katika AK kuhusiana na masihi atakuwa na sifa gani naye atatenda nini. “Wayahudi walimtarajia Masihi kuja kwa namna tatu: 1. Mfalme [wakinukuu **Yer 23:5-6; Zab 110:1-2**]. 2. Kuhani [wakinukuu **Zak 6:12-13; Zab 110:3-4**]. 3. Nabii [wakinukuu **Kumb 18:18-19**.]” (Abdul-Mohsin 2006: 95-97) Muhimu zaidi, Masihi asingekuwa “mfalme” tu lakini anayekwenda kuwa “mfalme”—mfalme wa mwisho wa dunia. “Katika mawazo ya kirabi, Masihi ni mfalme atakayewakomboa na kutawala Israeli katika kilele cha historia ya mwanadamu na ambaye kwa huyo ufalme wa Mungu utastawi” (Jacobs 2008: Messiah in Rabbinic Thought). Vifungu vingi vya AK vinaonesha kwamba Masihi atakuwa mwanadamu (mfano, **Mwa 3:15; Isa 11: 1-5; 42:1-6; 59:20; Yer 30:18-22; 33:14-15**); hata hivyo, vifungu vingine vinaonesha kuwa Masihi atakuwa wa kiungu (mfano, **Zab 2:6-12; 110:1-7; Isa 9:6; Yer 23:5-6; Mik 5:2; Zak 14:9**).⁴¹ Wayahudi wengi—pamoja na Petro—walimtarajia Masihi kuwa na sura ya kisiasa zaidi ambaye angewatoa Warumi na kuustawisha tena Yerusalem na hekalu katika utukufu kama kituo cha dunia mpya. Hakuna aliyekuwa na wazo la Masihi atakayekufa na kufufuka.

Alichosema Yesu kuhusiana na umasihi wake kilikwenda kinyume kabisa —na kilikwenda mbali zaidi—ya matarajio hayo yote. AJ linaonesha kwa wazi kwamba Yesu Kristo anatimiza matarajio ya Israeli ya mfalme na mwokozi atakayetumwa na Mungu (angalia, kwa mfano, **Mat 2:4-11; 16:16, 20; 21:1-11; 22:42-45; 26:63-64; Marko 8:29; 11:1-11; 12:35-37; 14:61-62; Luka 4:41; 19:28-40; 20:41-44; 22:67-70; 23:2-3, 39; 24:26, 46; Yoh 1:49; 4:25-26; 11:25-27; 12:12-16; 20:30-31; Mdo 2:30-36; 9:22; 17:3; 18:5, 28; 1 Yoh 2:22; 5:1**). Yesu pia ni kuhani mkuu kamili katika hekalu halisi (**Ebr 2:17; 4:14-5:10; 7:1-8:6; 10:11-22**). Mwisho, Yesu anatimiza unabii wa Musa kwamba Mungu angewainulia nabii mwingine kama yeche (angalia **Kumb 18:15, 18-19; Yoh 1:45; 6:14; Mdo 3:20-23**).

Hata hivyo, katika **mst. 31**, Yesu alikuwa anawaambia wanafunzi wake kwamba hakuja kuokoa watu kwa maana ya kisiasa bali kutoka katika utumwa wao wa dhambi. Hakuja kumshinda adui wa kikoloni wa Waisraeli, bali adui mkubwa zaidi ambaye watu wote wanakabiliana naye: dhambi; Shetani; na mauti yenye. Ni kwa namna gani atatekeleza hili hakuwepo yeyote aliyeota. Hivyo, katika **mst. 31** Yesu aliunganisha dhana ya mwana wa mtu (kutoka **Dan 7:13-14**) pamoja na mtumishi atakayeteswa wa **Isa 52:13-53:12**, jiwe lililokataliwa la **Zab 118:22** (ambalo litakuwa jiwe kuu la pembedi), na ufuluo siku ya tatu wa **Hos 6:2**.⁴² Rikk Watts anaonesha, “Katika kuunganisha maandiko haya mbalimbali na

⁴⁰ Hapa Yesu anasema, “*Baada ya siku tatu [ata] fufuka tena*” (**mst. 31**). Kifungu kinachokwenda sambamba na Mathayo kinasema, “*Siku ya tatu atafufuka*” (**Mat 16:21**). Katika muktadha mwingine alisema atakuwepo katika moyo wa dunia kwa “*siku tatu mchana na usiku*” (**Mat 12:40**). Ukweli kwamba Yesu alizikwa jioni ya Ijumaa (**Mat 57-60; Marko 15:42-46; Luka 23:50-56; Yoh 19:31, 38-42**) na kufufuka siku iliyofuata asubuhi (**Mat 28:1-6; Marko 16:1-6; Luka 24:1-6; Yoh 20:1**) haipingani na rejea ya “*mchana tatu na usiku tatu*.” Tamko hilo ni msemo. “*Talmud za Kibabyoni* (Mafafanuzi ya Kiyahudi) zinaleza kwamba, ‘sehemu ya siku ni sawa na siku nzima.’ *Talmud ya Jerusalem* (iliitwa hivyo kwasababu iliandikiwa Yerusalem) inasema, “*Tunalo fundisho, ‘usiku na mchana ni Onah na sehemu ya Onah nis sawa na sehemu nzima.’*” (McDowell 1981: 122) Kwa kuwa “hesabu za Kiyahudi zilifikiria sehemu ya siku ni sawa na siku nzima (cf. Mwa. 42:17-18; 1 Sam 30:12-13; Est 4:16; 5:1 [angalia pia 1 Falm 20:29; 2 Nyak 10:5, 12]), hivyo Yesu alikuwa kaburini Ijumaa, Jumamosi na Jumapili, na misamiati inakubaliana” (Osborne 2010: 486; angalia pia Delling 1964: 949-50). **Mat 27:63-64** inaonesha matumizi yasiyo na maana ya misamiati ya “siku tatu” kipekee ikihusishwa na maziko ya Yesu: Katika **27:63** Mafarisayo walikwenda kwa Pilato na kusema kwamba Yesu alikuwa amesema, “*Baada ya siku tatu ingenipasa kufufuka tena*.” Kwahiyoo, katika **27:64** waliomba kwamba Pilato “*atoe amri ya kulindwa kwa kaburi hadi siku ya tatu*.” “Kama maneno, ‘baada ya siku tatu,’ yasingekuwa yamebadilishwa na ‘siku ya tatu,’ Mafarisayo wangeomba ulinzi kwa siku ya nne” (McDowell 1981: 122). Hilo linathibitishwa katika **Yoh 2:18-19** ambapo Wayahudi pia walimuomba Yesu ishara. Yesu akajibu. “*Haribuni hekalu hili, na kwa siku tatu nitalismamisha*” (akimaanisha hekalu la mwili wake, **Yoh 2:21-22**).

⁴¹ Ona kuwa, tunapoweka **mst. 29, 31** na **Mat 16:15-17** pamoja, Yesu alikuwa akimlinganisha Masihi (Kristo) na “Mwana wa Mungu.”

⁴² Katika **Luka 24:46** Yesu anataja kwamba ufuluo wake kwenye “*siku ya tatu*” habari zake “zimeandikwa” katika AK.

kujiita ‘Mwana wa Mungu’, kunamuingiza Yesu katika kile kinachoonekana kuwa tendo la kitafsiri lisilotarajiwa na linawashangaza wanafunzi kama linavyowashangaza mashahidi katika Isaya . . . ingawa sehemu ya mteso ya Isa. 53 kwa mapana inaeleza, wakati mwininge, ikihusishwa na Musa . . . na huenda na yejote anayehusika kieskatolojia . . . hili halikuingia katika mwana wa Adamu au Masihi anayetajwa na Danieli, ambaye anapokeea utukufu na kuhesabiwa haki. Yesu kujengea utambulisho wake katika umasih na mwana wa Mungu katika Isa. 53 mteso hayakutarajiwa kabisa, kwa kuwa hayo yangekuwa ni matokeo yenye kumaanisha kuwa amani ya Israeli ingekuja kupitia uvumilivu, hadi kifo, majeraha ya kitorati na madhaifu ya kiuasherati ya hukumu ya Israeli uhamishoni [yaani, kujichukulia wenyewe laana ya sheria].” (Watts 2007: 181-82)

Hakika, wakati Yesu aliposulubiwa, hata wale waliokuwa wameamini alikuwa mkombozi aliyetarajiwa walipoteza tumaini lao kwasababu Masihi aliyesulubiwa ilionekana ni uhusiano unaopingana na matarajio yao (angalia **Luka 24:19-21**). Watu hawakuelewa kuwa kusulubiwa ilikuwa *njia* ambayo kwa hiyo wokovu kutoka dhambini ungekamilika.⁴³ Halafu yasiyotarajiwa yanatokea: Yesu anafufuka kutoka kwa wafu. Baada ya kufufuka kwake, Yesu aliwaelezea wanafunzi wake, “*Je! Haikumpasa Kristo [yaani Masihi] kupata mteso haya na kuingia katika utukufu wake?*” (**Luka 24:26**), na “*Ndivyo ilivyoadidika, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu*” (**Luka 24:46**). Kwahiyo Yesu alitimiza matarajio yote ya AK ya umasih, lakini alifanya hivyo kwa namna isiyotarajiwa. Kwa hivyo alileta maana kubwa na ya kina zaidi kuliko watu walivytarajia. Matokeo yake, AJ linamtangaza kama mwokozi ambaye pekee atawaokoa watu na dhmbi zao (**Mat 1:21; Luka 2:11; Yoh 1:29; 3:17; 4:42; Mdo 3:26; 4:12; 5:31; 13:23, 38-39; 15:11; 16:31; Rum 3:24-26; 4:25; 5:1, 6-11, 15-21; 8:2; 10:9; 1 Kor 1:30; 6:11; 15:17; 2 Kor 5:18-21; Gal 1:3-4; Ef 2:13-16; 4:32; 5:2, 25-26; Flp 3:20; Kol 1:12-14; 3:13; 1 Thes 1:10; 5:9-10; 1 Tim 1:15; 2 Tim 2:10; 3:15; Tit 1:4; 2:13-14; Ebr 2:17; 5:9; 7:25; 13:20; 1 Pet 1:18-19; 3:18; 2 Pet 1:11; 1 Yoh 3:5; 4:9-10, 14; Ufu 5:9; 14:4**).

Ni kile ambacho Petro na wanafunzi wengine hawakuelewa. Baada ya Yesu kuelezea kwamba angeteseka, angekataliwa, angeuwawa, na kisha angefufuka tena (**mst. 31**), **Mat 16:22** inatupa sababu za Petro kukemewa na Bwana, “*Hasha, Bwana, hayo hayatakupata..*” Alikuwa Shetani wa jangwani ambaye awali alimjaribu Yesu aachane na njia ya msalaba (**Mat 4:1-11; Luka 4:1-12**). Hivyo, katika **mst. 33** Kristo alimkemea Petro (na wanafunzi wengine akiwageukia wote akiwaambia), “*Nenda nyuma yangu, Shetani; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu.*”⁴⁴ Kama R. Alan Cole anavyoonesha, “mapendekezo ya Shetani siyo ya kukufuru au uovu wa wazi; ni laini, yanavutia na ya ‘asili’, yenye ushawishi kwa hisia za wanadamu wote. Ndiyo maana yalikuwa hatari kiasi hicho.” (Cole 1989: 206)

3. mst. 34-38—Gharama ya uanafunzi

Tayari Yesu amesha jitambulisha ni nani (**mst. 27-30**) na amesema wazi kwamba njia ya Masihi na Mwana wa Mungu ilihu mteso, kukataliwa na kufa (**mst. 31-33**). Sasa katika **mst. 34-38** anaweka wazi kwamba yejote anayetaka kumfuata lazima apite katika njia ile ile aliyopitia, ambayo, ni njia ya mteso, kukataliwa na kifo cha umimi. Petro alikuwa amemkemea Yesu na alitaka kumuepusha Yesu na msalaba. Sasa Yesu “siyo tu anarekebisha upinzani wa Petro wa umasih wa mteso, lakini anafanya mteso, kujikana, na kubeba msalaba nia muhimu kwa Petro na wanafunzi wote pia, kama wanataka kumpendenza Bwana wao na kuokoa nafsi zao” (Gruenler 1989: 783). Maneno ya Yesu, “*Mtu ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate.*” (**mst. 34**) ni wa kinabii, kwa kuwa yeje mwenyewe atawatangulia wanafunzi (na sisi) ikimaanisha kubeba msalaba wake. Hatudai jambo ambalo yeje mwenyewe hakulifanya. Vile Masihi alivyo kuwa ndivyo Wakristo inavyotupasa kuwa. Utambulisho kati ya Yesu na wanafunzi umekamilika. “Kuikana nafsi inamaanisha kwamba tunakatalia hisia zetu za asili kuhusu sisi wenyewe, yaani, haki zetu wenyewe, haki za kuendesha maisha yetu tutakavyo. Tunapaswa kukana kwamba sisi ni mali yetu wenyewe. Hatuna haki ya mwisho ya kuamua kile tunachokwenda kutenda, au tunakokwenda. Ilivyotamkwa katika maelezo yale, watu mara moja huhisi kwamba Yesu anasema jambo la msingi. Linachoma pale pale kwenye moyo wa uhai wetu, kwasababu jambo moja, sisi //

“Na bado ni mst.ari gani huo aliokuwa akiurejea? Wakati inawezekana kukawepo na sintofahamu kuhusu kisa cha Yona, rejea nyingine ya mbali inayowezekana ni Hosea 6:2 (‘baada ya siku mbili atatuhuisha, na siku ya tatu ataturejesha’). Kama ndivyo, Yesu atakuwa alichukua mst.ari ambao asili yake unahusu kurejeshwa au uamsho wa Israel na badala yake kuutumia mwenyewe kama Masihi wa Israeli. . . . Kama Dodd alivyo hitimisha kwa kusema: ‘ufufo wa Kristo *ni* ufufo wa Israeli ambao manabii waliuzungumzia’.” (Walker 1996: 285)

⁴³ Hawakuelewa hata kama AK lilishatabiri kwamba taji ya utawala ya Masihi na enzi yake itaangushwa (**Zab 89:39, 44**), maadui wake watafurahi (**Zab 89:42**), na atauwawa kama toleo la dhabihu (**Isa 53:1-12**).

⁴⁴ La kuvutia ni kwamba, neno “kemeo” (Kigiriki = *epitimaō*) ni neno lilelile lililotumika kunyamazisha au kukemea mapepo (angalia **Mat 16:22; Marko 1:25; 3:1; 8:32-33**).

kama wanadamu, tunalothamini na kutamani na kulinda kuliko yote ni haki ya kufanya maamuzi ya mwisho kwa ajili yetu wenyewe. Tunakataa kuwa chini ya chochote au ye yeyote, lakini tunatunza haki ya kufanya maamuzi ya mwisho kwa maisha yetu. Hiki ndicho Yesu anachozungumzia. Hazungumzii kuhusu kucha hiki au kile, lakini kujitoo sisi wenyewe.” (Stedman 2021b: n.p.) Asili muhimu ya kile anachosema Yesu, na jinsi ilivyo kinyume na wengi wetu tunavyofikiri na kutenda, ni maneno ya C. S. Lewis ambaye alisema, “Kuna aina tatu za watu duniani. Daraja la kwanza ni wale amba wanaishi kwa ajili yao wenyewe na raha zao. . . Katika daraja la pili ni wale wanaotambua madai mengine juu yao – mapenzi ya Mungu, daraja la walio wengi, au walio wema katika jamii – na kusema kweli wanajitahidi kufuatilia wanayovutiwa na hawataruhu zaidi ya madai haya. Wanajaribu kujitoa kwa madai ya juu zaidi ikiwa ni lazima, kama kulipa kodi, lakini kwa matumaini kama walipa kodi wengine, kwamba watakachobaki nacho kitawatosha kuendelea na maisha. . . Lakini kundi la tatu ni la wale amba wanaweza kusema kama Paulo kwamba kwao ‘kuishi ni Kristo [Flp 1:21]’. Watu hawa wameachana na shughuli ya kushindana na madai ya nafsi na Mungu kwa kukatalia madai yote ya nafsi. . . Mapenzi ya Kristo hayazui tena mapenzi yao; ni yao. Muda wao wote, unamhusu Yeye, unawahu wao pia, kwa kuwa ni mali yake.” (Lewis 1986: 21) Kwa kifupi, Kristo anasema kwamba, ili kumfuata, lazima tutambue ukweli kwamba “*Wala ninyi si mali yenu wenyewe;*” (**1 Kor 6:19-20**).

Rejea ya Yesu kwa “msalaba” inakazia kuikana nafsi, kwa kuwa msalaba ulikuwa ni zana ya kifo. Lakini msalaba ulikuwa zaidi ya hayo. “Ilikuwa ni mahali pa kudhalilika, ambapo alidhalilishwa na kudharauliwa. Na hivyo msalaba unasimama milele kama alama ya hali na matukio haya katika maisha yetu ambayo hutunyenyekesha, hutufunua, hukwaza kiburi chetu, hutuaibisha, na kufunua uovu wetu wa ndani. . . Hali ye yeyote, tukio lolote ambalo linatenda hayo kwetu, Yesu anasema, kama tu wanafunzi, tunapaswa kulikaribisha. Hiyo ndiyo maana yake. ‘Jitwike msalaba wako, upokee, ufurahie, ung’ang’anie, kwasababu ni kitu kizuri kwako. Utakushusha hadi mahali ambapo utakuwa tayari kupokea zawadi ya neema ya Mungu.’ Hii ndiyo maana msalaba ni wa thamani kiasi hicho.” (Stedman 2021b: n.p.) “Kumfuata” Yesu ina maana ya “kumtii”. “Sio jambo la kushangaza kwamba inatuchukua muda mrefu kuelewa kwamba kama uasi ni jina la mchezo kabla ya kuwa Wakristo, basi, kwa hakika kutii ni jina la mchezo baada ya kuwa Wakristo.” (Ibid.)

Maelezo mengine machache ya yale Yesu anayosema katika mistari hii yanapaswa kutajwa. Kwanza, kile anachosema kinamhusu “kila mmoja” (**mst. 34**) ambaye atamfuata. Kwa maneno mengine, hazungumzi na daraja fulani la Wakristo (yaani, “Wanafunzi” dhidi ya “Wakristo wa kawaida”) lakini kwa “*kila mtu*” anayetaka au anayedai kuwa ni Mkristo. Pili, Kile anachosema siyo swala la muda fulani lakini la wakati wote. Maelezo ya Luka kuhusiana na hili yanaweka wazi: “*Akawaambia wote, ‘Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate.’*” (**Luka 9:23**) Tatu, anachosema ni jambo muhimu sana duniani kwasababu linagusa vitu tunavyothamini zaidi tulivyo navyo—nafsi yetu—ambayo ina thamani kuliko dunia yote: “*Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake? Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake?*” (**mst. 36-37**) Nne, iwe tunamfuata Yesu kama alivyo eleza au la kutakuwa na matokeo ya milele: “*Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu, katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu*” (**mst. 38**).

Mwisho, kile Yesu anachotuambia katika mistari hii siyo swala dogo au la kuchagua. Ni kitovu chenyewe hasa cha Ukristo na, kimsingi kinaeleza nini maana ya kuwa Mkristo. Kwa hakika, kanuni iliyoelezwa katika **mst. 35**—“*Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakaye iangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha*”—inapatikana mara nyingi kuliko kanuni nyingine katika Injili. Inapatikana mara sita katika Injili zote nne, ikiwakilisha mazungumzo ya Yesu mara nne: **Mat 10:39; 16:35; Marko 8:35; Luka 9:24; 17:33; Yoh 12:25**. Kwahiyu tunahitaji kuchukua kile ambacho Yesu anasema hapa kwa kumaanisha sana, tutathimini maisha yetu, kwa nuru ya kile alichosema, na kufanya marekebisho katika maisha yetu ili kujileta katika kufanana naye.

MASWALI YA KUJADILI

1. Yesu alielezaje maana ya Masihi na Mwana wa Mungu?
2. Kwanini unadhani Petro alianza kumkemea Yesu (**mst. 32**)? Kwanini unadhani Yesu alikuwa na maneno makali katika kumkemea (**mst. 33**)?
 - Majibizano ya maneno kati ya Petro na Yesu yanatuambia chochote au kutupatia funzo lolote?

3. Kanuni iliyotajwa katika **mst. 35** inapatikana mara nyingi zaidi kuliko kanuni nyingine katika Injili zote—mara 6 katika Injili 4, ikiwakilisha jumbe 4 tofauti za Yesu za mwanzoni, katikati, na mwisho wa huduma yake ya hapa duniani: Hapa (pamoja na vifungu vinavyokwenda sambamba vya **Mat 16:25** na **Luka 9:24**); **Mat 10:39** (kutumwa kwa mitume 12); **Luka 17:33** (baada ya kubadilika sura lakini kabla ya kuingia Yerusalem); na **Yoh 12:25** (baada ya kuingia Yerusalem kwa mara ya mwisho). Yesu alieleza kinaga ubaga nini kinahitajika kama mtu anataka kuwa Mkristo. Eleza kwa maneno yako kile Yesu alichosema.

- Je hivi ndivyo kufanyika Mkristo au kuwa Mkristo kunavyoelezwa leo? Kama sivyo, kwanini?
- Kama gharama za kuwa Mkristo “zinaelezwa tofauti” na wachungaji, wainjilisti, na Wakristo wengine leo, Ni madhara gani (kama yapo) yanayoweza kuletwa na hilo?

4. Pitia Injili na tafuta sehemu zingine ambapo Yesu anataja kile anachotaka kama mtu anataka kuwa Mkristo.

- Tunawezaje kukabiliana na kile alichosema Yesu na matamanio yetu ya kawaida ya kupata “kilicho bora kutoka pande zote” (yaani, kile kinachopatikana humu duniani na mbingunu vile vile)?
- Kama kuna kuachana kati ya kile Yesu anachosema kuhusu kuwa Mkristo na kile tunachoelewa kuwa ndiyo kuwa Mkristo nini kifanyike (kinapaswa) tufanye?

9:1-13: ¹*Akawaambia, Amin, nawaambia, Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapouona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu.*

²*Hata baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yoh, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani, peke yao; akageuka sura yake mbele yao;* ³*mavazi yake yakimeta-meta, meupe mno, jinsi asivyoweza dobi duniani kuyafanya meupe.* ⁴*Wakatokewa na Eliya pamoja na Musa, nao walikuwa wakizungumza na Yesu.* ⁵*Petro akajibu, akamwambia Yesu, Rabi, ni vizuri sisi kuwapo hapa; na tufanye vibanda vitatu, kimoja chako wewe, kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya.* ⁶*Maana, hakuju la kunena, kwa kuwa waliingiwa na hofu nyingi.* ⁷*Kisha likatokea wingu, likawatia uvuli; sauti ikatoka katika lile wingu, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, msikieni yeye.* ⁸*Mara hiyo walipotazama huku na huku, hawakuona mtu pamoja nao ila Yesu peke yake.*

⁹*Na walipokuwa wakishuka mlimani aliwakataza wasimweleze mtu waliyoyaona, hata Mwana wa Adamu atakapokuwa amefufuka katika wafu.* ¹⁰*Wakalishika neno lile, wakiulizana wao kwa wao, Huko kufufuka katika wafu maana yake nini?* ¹¹*Wakamwuliza, wakisema, Mbona waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?* ¹²*Akajibu akawaambia, Ni kweli Eliya yuaja kwanza, na kurejeza upya yote; lakini, pamoja na haya, ameandikiwaje Mwana wa Adamu ya kwamba atateswa mengi na kudharauliwa?* ¹³*Lakini nawaambia, Eliya amekwisha kuja, nao wakamtenda yote waliyoyataka kama alivyoandikiwa.*

mst. 1-13—Kubadilika Sura

Petro, Yakobo, na Yoh waliruhusiwa kushuhudia Yesu akibadilishwa katika hali yake ya utukufu, kuona maono ya Musa na Eliya wakiwa na Yesu, na kusikia maneno ya Mungu kutoka mbinguni, “Huyu ni mwanangu ninayependezwa naye, msikieni yeye.”

1. mst. 1—Baadhi watauona Ufalme wa Mungu

Yesu mwenyewe alikuwa akitumia maneno yafuatayo kama maneno yenye maana sawa, Mwana wa Mungu, injili, na ufalme katika **8:34-38** (angalia pia **Mat 16:28**). Wasomi mbalimbali wanafikiri “*ufalme wa Mungu baada ya kuja katika nguvu yake*” (**Mat 16:28** inaweka maneno hayo hivi, “*kuja kwa Mwana wa Mungu katika ufalme wake*”); **Luka 9:27** yeye anasema tu, “*hadi watakapouona ufalme wa Mungu*”) akimaanisha kubadilika sura, ufufuo, Pentekoste na kuenea kwa kanisa la kwanza, mafundisho ya Yesu, na/au kuanguka kwa Yerusalem (angalia Bird 2003: 23-25; Cole 1989: 209). “Mojawapo au njia zote hizi, na bila shaka njia zingine pia, wale walio na macho yanayoona waliweza kuelewa kabla ya kufa kwamba Mungu ametawala kwa nguvu matukio na alikuwa anaandika historia. Hata kama baadhi ilikuwa wangekufa kabla haya hayajadhihirika wazi, mchakato ulikuwa umeanza, na mbegu ya haradali ilikuwa inakua. Hayo ndiyo yaliyomaanishwa na 9:1.” (France 2002: 345)

Mtume Petro anahusisha hili na kubadilika sura. Katika **2 Pet 1:16-18** anarejea “nguvu” na “kuja” kwa Bwana, anazungumza habari ya “mlima mtakatifu” kubadilika sura kulikotokea, na ananukuu sauti waliyosikia kutoka mbinguni: “¹⁶ Maana hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, tulipowajulisha ninyi nguvu zake Bwana wetu Yesu Kristo na kuja kwake; bali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake.” ¹⁷ Maana alipata kwa Mungu Baba heshima na utukufu, hapo alipoletewa sauti iliyotoka katika utukufu mkuu, Huyu ni Mwanangu, mpPENDWA wangu, ninayependezwa naye. ¹⁸ Na sauti hiyo sisi tuliiisikia ikitoka mbinguni tulipokuwa pamoja naye katika mlima ule mtakatifu.” **Mst. 1** unaunganisha kile ambacho Yesu alitokea kusema katika **Marko 8:38** (“atakapokuja katika utukufu wa Baba yake na malaika”) na kile kilichofuatia mara (kubadilika sura). Kwahiyoo inawezekana kwamba Marko alielewa kubadilika sura kama sura ya Kristo itakayodhihirika wakati wa kufufuka kwake, kupaa, Pentekoste, na kuja mara ya pili kulikodhihirisha (na kutakakodhihirisha) utukufu, nguvu na ufalme kwa wote.

2. mst. ya 2-8—Kubadilika sura

Mng’ao mweupe wa mavazi ya Kristo uliwakilisha usafi, haki na asili ya mbinguni (angalia **Dan 7:9; Ufu. 19:8**). Bila shaka mawingu yalikuwa ni utukufu wa shekina (angalia **Kut. 24:16; 40:38**). Kuna mfanano kati ya kubadilika sura na ubatizo wa Yesu. Katika ubatizo wa Yesu na kubadilika sura Baba ananukuu kutoka **Zab 2:7** na anatangaza, “Huyu ni mwanangu mpPENDWA” (**Mat 3:17; 17:5; Marko 1:11; 9:7; Luka 3:22; 9:35**). Kwa ubatizo na kubadilika sura kulikuwa na kulinganishwa kwa Yesu na Eliya (Yoh Mbatizaji wakati wa ubatizo; angalia chini kufananishwa huko). Ingawa Marko anasema Musa na Eliya walikuwepo na “walizungumza na Yesu” (**mst. 4**), hatuelezi walichokuwa wakizungumza. **Luka 9:31** inatuambia “walizungumzia kuondoka kwake, ambako kulikuwa kunakaribia kukamilishwa kule Yerusalem.” Jambo la kuvutia, neno la Kigiriki “kuondoka” ni “Kutoka.” Mwitikio wa Yesu unatuonesha kuwa hakuwa ameelewa kikamilifu Yesu ni nani na kwamba angelazimika kuteseka na kufa. Kwa kusema, “Turuhusu tujenge vibanda vitatu, kimoja chako, na kimoja cha Musa na komoja cha Eliya” (**mst. 5**), Hapo petro alikuwa, anamuweka Yesu katika nafasi moja na Musa na Eliya na alitaka kuongeza muda wa mukutano wao na kuwasiliana kwao na watu. Kuondoka kwa haraka kwa Musa na Eliya na maneno ya Mungu, “Huyu ni mwanangu mpPENDWA; msikilizeni yeye” (**mst. 7**) unaweka wazi kwamba Yesu ndiye hema ya kukutania ya Mungu ya kweli na kwamba misheni ya Masihi inatofautiana na kile Petro alichoomini.

3. mst. 9-13—Kushuka kutoka mlimani

Mistari 9-10 inatuonesha kuwa bado wanafunzi hawakuwa wameelewa kwamba Yesu angeuwawa na kufufuka kutoka kwa wafu, pamoja na kwamba alikuwa amewaeleza hivyo “wazi” katika **8:31-32**. Kama Wayahudi, wanafunzi walielewa dhana ya ufufuo, lakini ufufuo wa wote wakati wa siku za mwisho (angalia **Yoh 11:24**); wazo la kwamba mtu mmoja angelifufuka na kuingi katika uzima wa milele katikati ya historia halikutarajiwa na lilikuwa nje ya uelewa wao.

Uwepo wa Eliya katika hali ya kimaono kule mlimani kuliamsha swali kwa wanafunzi, “Si Eliya anapaswa kuja katika mwili kutangaza kizazi cha Kimasihi?” Yesu anakubaliana na ahadi hiyo, na jibu lake kwa swali hilo, Yesu anamtambulisha kuwa ndiye Yoh Mbatizaji. **Isa 40:3-11** na **Mal 3:1** imeandikwa Bwana atamtuma mjumbe wake mbele za Bwana kwa watu wake na kwa hekalu lake. Zakaria (baba yake Yoh Mbatizaji) alithibitisha kuwa kwa kutamka Mungu ameinua pembe ya wokovu kwa ajili yetu katika nyumba ya Daudi mtumishi wake” (**Luka 1:69**, akimaanisha Yesu). Kisha katika **Luka 1:76** alinukuu kutoka katika **Mal 3:1** akimaanisha Yoh Mbatizaji (“Nawe, mtoto, utaitwa nabii wake Aliye juu, Kwa maana utatangulia mbele za uso wa Bwana umtengenezee njia zake”). Yoh Mbatizaji mwenyewe alinukuu kutoka katika **Isa 40:3-5** na **Mal 3:1** kabla ya kubatizwa Yesu (**Mat 3:3; Marko 1:2-3; Luka 3:4-6; Yoh 1:23**). Yesu anathibitisha kwamba Yoh Mbatizaji alikuwa “mjumbe” aliyenewa na **Mal 3:1** (angalia **Mat 11:7-10; Luka 7:24-27**).⁴⁵ Hivyo, Yoh Mbatizaji na Yesu walitimiza unabii wa Isaya **Isa 40:3-11** na **Mal 3:1**. Mjumbe atakayekwenda mbele za Bwana nabainishwa katika **Mal 4:5**, inaposema kwamba Mungu atamtuma “Eliya nabii.” Yoh Mbatizaji anaelezwa kama ambaye alikuwa na roho ya Eliya kuwaandaa watu kwa ujio wa Bwana (**Mat 11:14; 17:10-13; Marko 9:11-13; Luka 1:13-17, 76**). **Mat 17:13** inasema kuwa “wanafunzi walielewa kuwa alikuwa anasema nao kwa habari ya Yoh Mbatizaji.”

Maneno ya Yesu katika **mst. 12**, “Eliya yu aja kwanza kurejesha yote sawa” ilimaanisha kuwa “wakati waliongojea kwa hamu ‘urejesho’ sasa ulikuwa katika mchakato wa kutekelezwa—lakini kimafumbo kwa njia ya ‘mateso’ ya ‘Mwana wa Mungu’ (Walker 1996: 43). Kwasababu wanafunzi bado hawakuelewa asili ya kuteswa kwa umasihi wake, Kwa mara nyingine tena Yesu alilazimika kukazia mateso yake, “Imeandikwa Mwana wa Adamu ya kwamba atateswa mengi na kudharauliwa?” (**mst. 12**). Ingawa walielewa kuwa Yoh Mbatizaji alikuwa Eliya aliyetarajiwa kuja, bado hawakuelewa kuwa “kama ambavyo

⁴⁵ Yesu mwenyewe ni “mjumbe wa agano” ilizungumzia sehemu ya mwisho ya **Mal 3:1**.

ujio wa Yoh ulikuwa ni kutangaza ujio wa Masihi, hivyo, kukataliwa kwa Yoh kulitangaza kukataliwa kwa Masihi: na wote walitimiza maandiko” (Cole 1989: 213).

MASWALI YA KUJADILI

1. Neno “kubadilika sura” (Kigiriki = *metamorphoō*) katika **mst. 2** (na katika kifungu kama hicho cha **Mat 17:2**) ni neno hilo hilo lilitotafsiriwa “kugeuzwa” (au ‘kubadilishwa’) katika **Rum 12:2** na **2 Kor 3:18**. haya ndiyo maeneo pekee katika Agano Jipyambapo neno hili limetumika, Hili linatuambia nini kuhusu maisha yetu katika Kristo?

- Lipi linabainishwa na ukweli kwamba wengi wetu hatuwezi kuona mabadiliko makubwa kwetu wenyewe (mawazo, maitikio ya nafsi, maneno na matendo)?

2. Unafikiri umuhimu wa uwepo wa Musa na Eliya ulikuwa na maana gani kule mlimani? au sauti kutoka mbinguni?

3. Tambua kwamba Yesu anajadili nafasi ya mateso na kifo (**mst. 12-13**) ikifuatiwa mara na utukufu wa kubadilika kwake sura kama mambo yanayohusiana na kile alichosema Petro kwake kama ndiye Kristo (**8:29-35**). Hili lina maana gani?

- Inakuwaje (kama basi) picha ya Masihi mtesekaji inabadili mtazamo wako wa kile kinachohusika na maisha ya Kikristo?

4. Katika kisa cha Martha na Mariamu (**Luka 10:38-42**) Mariamu “kukaa miguuni mwa Yesu” mara zote kunachukuliwa kama jambo la sifa, wakati huduma ya Martha haichukuliwi hivyo. Katika kifungu hiki, kwa upande mwingine, Petro anaeleza shauku ya kukaa na Yesu kule mlimani; hata hivyo, siyo tu kwamba hili halitokei, lakini shauku ya Petro haisifiwi, ama na ile sauti kutoka mbinguni, au na Yesu. Weka vifungu hivi pamoja na upate maelezo yanayogusa sehemu zote na uelezee nafasi ya mahusiano ya mafundisho yote mawili.

9:14-29: ¹⁴*Hata walipowafikia wanafunzi, waliona mkutano mkuu wakiwazunguka, na waandishi wakijadiliana nao;* ¹⁵*mara mkutano wote walipomwona walishangaa, wakamwendea mbio, wakamsalimu.* ¹⁶*Akawauliza, Mnajadiliana nini nao?* ¹⁷*Mtu mmoja katika mkutano akamjibu, Mwalimu, nimemleta mwanangu kwako, ana pepo bubu;* ¹⁸*na kila ampagaapo, humbwaga chini, naye hutoka povu na kusaga meno na kukonda; nikasema na wanafunzi wako wamtoe pepo, wasiweze.* ¹⁹*Akawajibu, akasema, Enyi kizazi kisichoamini, nikae nanyi hata lini? Nichukuliane nanyi hata lini? Mleteni kwangu.* ²⁰*Wakamleta kwake; hata alipomwona, mara yule pepo alimtia kifafa; naye akaanguka chini, akagaa-gaa, akitokwa na povu.* ²¹*Akamwuliza babaye, Amepatwa na haya tangu lini? Akasema, Tangu utoto.* ²²*Na mara nyangi amemtupa katika moto, na katika maji, amwangamize; lakini ukiweza neno lo lote, utuhurumie, na kutusaidia.* ²³*Yesu akamwambia, Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye.* ²⁴*Mara babaye yule kijana akapaza sauti, akasema, Naamini, nisaidie kutokuamini kwangu.* ²⁵*Naye Yesu akiona ya kuwa mkutano unakusanyika mbio, akamkemea yule pepo mchafu, akamwambia, Ewe pepo bubu na kiziwi, mimi nakuamuru, mtoke huyu, wala usimwingie tena.* ²⁶*Akalia, akamitia kifafa sana, akamtoka; naye akawa kama amekufa; hata wengi wakasema, Amekufa.* ²⁷*Lakini Yesu akamshika mkono akamwinua naye akasimama.* ²⁸*Hata alipoingia nyumbani, wanafunzi wake wakamwuliza kwa faragha, Mbona sisi hatukuweza kumtoa?* ²⁹*Akawaambia, Namna hii haiwezi kutoka kwa neno lo lote, isipokuwa kwa kuomba.*

mst. 14-29—Yesu anamponya kijana aliyepagawa na pepo

Kama ilivyokuwa katika matendo yake mengi, kutolewa kwa pepo na kuponywa kwa kijana huyu ni mfano ulioonesha hali (yetu) ya kibinadamu: kijana huyu “tangu utotonii” alitawaliwa na nguvu (kwa upande wetu, dhambi) hana uwezo kabisa wa kujibadilisha; watu wa dini ambao hawana msaada na ambao wanabishana wao kwa wao; watazamaji waliosubiri kuona nini kinatokea; na mahangaiko ya mmoja aliyempenda kijana. Nyuma ya swalii la Yesu na muitikio katika **mst. 16-19** ni kanuni muhimu ya kiroho: “Kwanza, wale walio na uhitaji lazima wakirii kupungukiwa, kisha ni lazima waletwe katika kuona nguvu ya Yesu inayokutana na uhitaji wao” (Cole 1989: 214).

Mistari 19 unaonesha uvumilivu mkubwa wa Yesu (“Enyi kizazi kisicho na imani, nitakaa nanyi

hata lini?”) na huruma zake kuu (“*Mleteni kwangu*”). Maneno ya baba katika **mst. 22**, “*Lakini kama unaweza kufanya chochote, tuhurumie na kutusaidia*” ni mlinganisho unaovutia ukilinganishwa na maneno ya yule mkoma katika **1:40**, “*Ukitaka, unaweza kunitakasa.*” Mkoma hakuhoji uwezo wa Yesu wa kumponya lakini alihoji huruma yake; hapa baba hakuhoji huruma za Yesu lakini alihoji uwezo wake. Changamoto ya Yesu kwa mtu huyu kumwamini iliamsha maneno ya pekee ya kutia moyo ambayo wengi wetu, mara kwa mara, tumekuwa tukiyaonesha: “*Naamini, nisaidie kutokuamini kwangu!*”

Katika **mst. 28-29**, wakati wanafunzi walipomwuliza Yesu kwanini hawakuweza kutoa yule pepo, Mathayo anaonesha Yesu alielekeza jibu katika imani: “*Akawaambia, kwasababu ya imani yenu haba. Amini, nawaambia, kama ukiwa na imani kama mbegu ya haradali, utaweza kusema kwa mlima huu, ‘toka hapa nenda kule,’ na utakwenda, na hakutakuwepo na jambo lisilowezekana kwenu.*” (**Mat 17:20**) Katika Marko, Yesu analenga shabaha katika kukosa kwao maombi: “*Akawaambia, namna hii haitoki isipokuwa kwa maombi*” (**mst. 29**).⁴⁶ Dhana hizi mbili zinakamilishana.

Maneno ya Yesu katika Mathayo na yale ya Marko **Marko 9:23** (“*Yote yanawezekana kwake aaminiye*”) yanaweza yakapelekea mtazamo potofu wa “kutaja na kudai” au “injili ya mafanikio” mtazamo wa imani ambako imani hugeuka na kuwa uchawi au “nguvu” isiyomhitaji Mungu. Hiyo siyo dhana ya kibiblia kabisa. Kinyume cha hayo, “Biblia inatufundisha kwamba imani ni kumtegemea mwagine kwa kujiamini. Badala ya kuwa ni kitu unachotakiwa kutenda, imani ya kibiblia inahusu pumziko. Thamani ya imani ni ya ndani. Siyo ya nje. Udhahiri wa imani unapatikana katika Mungu.” (Sarles 1986: 348) Katika Agano Jipyä lugha ya imani imetumiwa “kuonesha mamlaka ya kiroho ya Yesu kwa vitendo na pia kuonesha muitikio unaopaswa wa injili ambayo amekuja kuitangaza. . . Ni jambo la kujitoa linalobadilisha maisha, mwanzo wa mahusiano mabaya na Mungu. . . Mlengwa wa kuamini anaweza kuwa Yesu mwenyewe tu.” (France 1992: 223-25) Kadhalika, maombi yetu yanatarajiwa kuibukia kutoka katika maisha matakatifu ya msamaha (**Marko 11:25-26**). Nia yetu katika maombi haipaswi kuwa ya kibinaksi (**Yak 4:3**) na lazima iendane na mapenzi ya Mungu, na siyo yetu. (**Marko 14:36; 1 Yoh 5:14-15**).

Inaweza kuwa hivyo, kwasababu wanafunzi hapo awali walikuwa wamepewa mamlaka ya kutoa pepo (**6:7**), imani yao “ilikuwa imehama kutoka katika kuwa imani inayomwangalia Mungu na kuwa imani inayoangalia mchakato waliokuwa wakiufuata. Walifikiri kuwa kama ukisema maneno sahihi, na ukafuata desturi sahihi, kwamba mapepo yangelazimika kutoka. Bila hata wao kutambua hivyo, walikuwa wamehamisha imani yao kutoka kumwamini Mungu anayeweza kutenda, na kuiangalaia kanuni inayoweza kuleta matokeo hayo. Hivi ndivyo mara nyingi huwa tunafanya. Tunakuwa tukifkiria kuwa ni yale maneno tunayotamka, au namna tunavyoyatamka, au kile kinachotokea katika maisha yetu ambacho ndiyo sababu hasa ya yale yanayotendeka, badala ya Mungu atendaye. Yesu anawakemea kwa hili, akisema imani yao inapaswa kuwa katika Mungu mwenyewe, kama itabakia kuwa imani hai.” (Stedman 2021a: n.p.) Walter Wessel anaandika hivyo pia, “*kwa kudanganyika wamechukulia kwamba nguvu waliyopewa inajitegemea au wameamini kuwa itakaa ndani yao kama asili inayowategemea wao wenyewe. Hivyo hawahitaji tena kumtegemea Mungu kwa maombi, na kushindwa kwao kulionesha kutokuwa na maombi.*” (Wessel 1984: 704)

MASWALI YA KUJADILI

1. Angalia kifungu hiki kama “mfano wa kuigizwa.” Mfano huu uko kwa ajili ya nini? Elezea wahusika wakuu katika “mfano” huu na nini wanawakilisha.
2. Gundua kuwa Yesu hakumponya yule mvulana mara moja, bali alilingia kwenye mazungumzo na baba yake kwanza hata wakati pepo akiwa tayari anamgaragaza chini, akitokwa na mapovu. Unafikiri kwa nini Yesu alifanya hivi? Je hili lina fundisho muhimu kwa ajili yetu?
3. Katika **mst. 29** Yesu alisema “*Namna hii haitoki isipokuwa kwa kuomba [baadhi ya makabrasha ya zamani yana neno la ziada ‘na kufunga’].*” Yesu hakuomba wala kufunga. Hili linatufundisha nini kuhusu asili hasa na kusudi la maombi na kufunga?

9:30-50: ³⁰ *Wakatoka huko, wakapita katikati ya Galilaya; naye hakutaka mtu kujua.* ³¹ *Kwa sababu alikuwa akiwafundisha wanafunzi wake, akawaambia, Mwana wa Adamu yuaenda kutiwa katika mikono ya watu, nao watamwua; hata akiisha kuuawa, baada ya siku tatu atafufuka.* ³² *Lakini hawakulifahamu neno lile, wakaogopa kumwuliza.*

³³ *Wakafika Kapernaumu; hata alipokuwamo nyumbani, akawaauliza, Mlishindania nini njiani?*

⁴⁶ Baadhi ya maandiko ya zamani huongeza neno “na kufunga.”

³⁴ Wakanyamaza; kwa maana njiani walikuwa wakibishana wao kwa wao, ni nani aliye mkubwa.

³⁵ Akaketi chini, akawaita wale Thenashara akawaambia, Mtu atakaye kuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho kuliko wote, na mtumishi wa wote.³⁶ Akaatwaa kitoto, akamweka katikati yao, akamkumbatia, akawaambia,³⁷ Mtu akinipokea mtoto mmoja wa namna hii kwa jina langu, anipokea mimi; na mtu akinipokea mimi, humpokea, si mimi, bali yeeye aliyenituma.

³⁸ Yoh akamjibu, akamwambia, Mwalimu, tulimwona mtu akitoa pepo kwa jina lako, ambaye hafuatani nasi; tukamkataza, kwa sababu hafuatani nasi.³⁹ Yesu akasema, Msimkataze, kwa kuwa hakuna mtu atakayefanya mwujiza kwa jina langu akaweza mara kuninenea mabaya;⁴⁰ kwa sababu asiye kinyume chetu, yu upande wetu.⁴¹ Kwa kuwa ye yote atakayewanywesha ninyi kikombe cha maji, kwa kuwa ninyi ni watu wa Kristo, amin, nawaambia, hatakosa thawabu yake.

⁴² Na ye yote atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, afadhali afungiwe jiwe la kusagia shingoni mwake, na kutupwa baharini.⁴³ Na mkono wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili, na kwenda zako jehanum, kwenye moto usiozimika;⁴⁴ ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.⁴⁵ Na mguu wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima, u kiwete, kuliko kuwa na miguu miwili, na kutupwa katika jehanum;⁴⁶ ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.⁴⁷ Na jicho lako likikukosesha, ling'oe, ulitupe; ni afadhali kuingia katika ufalme wa Mungu, una chongo, kuliko kuwa na macho mawili, na kutupwa katika jehanum;⁴⁸ ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.⁴⁹ Kwa sababu kila mtu atatiwa chumvi kwa moto.⁵⁰ Chumvi ni njema; lakini chumvi ikiwa si chumvi tena, mtaitia nini ikolee? Mwe na chumvi ndani yenu, mkakae kwa amani ninyi kwa ninyi.

mst. 30-50—Yesu anafundisha kuhusu kifo chake, ufufuo wake na uanafunzi

Kama alivyofanya katika **8:31-38**, Yesu anaunganisha maisha ya wale ambao wangependa kuwa wanafunzi wake katika maisha yake ya mateso na kifo. Sehemu hii pia imeja kejeli na tena hufunua udhaifu wa wanafunzi.

1. mst. 30-32—Yesu anatabiri kifo na ufufuo wake

Mistari **30** unaanzisha safari ya mwisho ya Yesu kutoka Galilaya kwenda Yerusalem. Hii ni mara ya tatu (**8:31; 9:9** [kwa Petro, Yakobo, na Yohana]; na **9:31**) wakati Yesu anawaambia wanafunzi wake kuhusu mateso yake yanayokuja, kifo na ufufuo wake. Yesu “*akitiwa mikononi mwa wanadamu*” ina maana ya Mungu baba kumtoa, na siyo usaliti wa Yuda (angalia **Isa 53:10; Rum 4:25; 8:32**). Kwa mara nyingine tena, hawaelewi anapozungumzia ufufuo wake.

2. mst. 33-37—Nani aliye mkuu zaidi katika ufalme

Mistari **33-34** inaonesha kejeli ya kwanza: Ndio Yesu ametokea kuwaambia (tena) kwamba atateswa, atakataliwa, na kuuwawa (**mst. 31**), na wao “*wakaingia katika malumbano wao kwa wao nani mkuu kuliko wote*” (**mst. 34**). Siyo tu kwamba malumbano yao yanajipinga kwa Yesu (ambaye ndiye “mkuu kuliko wote”) na kwa misheni ya Masihi (kuteseka, kufa, na “*kutoa uhai wake kama fidia ya wengi*,” **Marko 10:45**), yanapingana pia na kile alichokuwa amewaambia katika **8:34**, “*Kama mtu akinifuata, ajikane mwenyewe na kuchukua msalaba wake na kunifuata*.” Ni kejeli pia katika hili kwamba wanafunzi ndio walikuwa wametokea kuonesha kutokujiamini kwao na kutokuwa na uwemo wa wa kutoa pepo kwa yule kijana katika **9:18, 28**, na sasa wanaonesha udhaifu wa kutoelewa na hofu (**mst. 32**), nabado wanabishana kuhusu nani ni mkuu kuliko wenzake!

Tamko la Yesu kwa wale kumi na wawili katika **mst. 35**, “*Kama mtu akitaka kuwa wa kwanza, lazima awe wa mwisho*,” lilikuwa linawaambia (na sisi) jinsi ya kuupata ukuu wa kweli machoni mwa Mungu. Sababu ni kwamba, kwa kufanya hivyo, wanafunzi (na sisi) tutakuwa tunamuiga Yesu mwenyewe, ambaye, “*hakuja kutumikiwa bali kutumikia*” (**Marko 10:45**). Maisha ya kutumikia wengine yanahitaji unyenyekevu wa kudumu, kinyume na hali ya kiburi waliyokuwa nayo wanafunzi na kutafuta hadhi ya juu. “Unyenyekevu huu, ambao ni sharia ya msingi katika ufalme, inadai kugeuza kabisa vipimo vyetu vya kimaadili, hali ambayo siku moja Mungu ataihesabia haki (10:31)” (Cole 1989: 221).

Kuwaita watoto waje kwake (**mst. 36**) ilikuwa ni mfano wa igizo lingine. Tamko lake katika **mst. 37**, “*Ampokeaye mtoto mmoja kama huyu kwa jina langu anipokea mimi, naye anipokeaye ampokea yeeye aliyenituma*,” unganisha unyenyekevu unaothibitishwa kwa mtoto, kwa kuwa inaoneshwa kuwa ukuu wa kweli ni kujishusha na kujali watu “*wanyonge*” kama watoto. Vifungu vinavyoenda sambamba vya **Mat 18:2-4** vinaunganisha mtoto na uwazi wa unyenyekevu: “²*Ni nani basi aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni?* Akaita mtoto mmoja, akamweka katikati yao,³ akasema, Amin, nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.⁴ Basi, ye yote ajinyenyekeshaye

mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni." Inawezekana kuna sababu kadhaa kwanini Yesu amuweke mtoto katikati yao; sababu mbili zinajitokeza:

- Siyo kwamba watoto "hawana hatia" (hapana). Badala yake, ni watu tegemezi wenyewe uwezo mdogo wa kurudisha fadhila. Usalama wao unatokana na mahusiano na imani yao kwa wazazi wao, ambao wanawategemea kwa kila kitu. Kristo aliwaita wanafunzi wake "watoto" (**Marko 10:24**). Wanafunzi (na sisi) tunahitaji kutambua kumtegemea Mungu kabisa katika Kristo, kama Yesu alivyosema katika **Yoh 15:5**, "*bila mimi hamwezi kufanya neno lolote.*" Hata hivyo, katika Kristo—kwa neema na nguvu zake—"naweza kutenda yote katika yeye anitiaye nguvu" (**Flp 4:13**). Sababu ni kwamba "*ni Mungu atendaye kazi ndani yako, kutaka na kutenda kusudi lake jema*" (**Flp 2:13**; angalia pia **Gal 2:20**).
- Sababu ya pili ni, Kristo anawafundisha wanafunzi wake dhana ya maadili ya ndani na yanayostahili. Mtoto huyu anapaswa athaminiwe sana kwasababu ya jinsi alivyo machoni mwa Mungu, wa thamani kwasababu ni kazi yake katika sura yake. Thamani ya mtoto huyu haihusiani na kile ambacho angeweza kuzalisha au namna ambavyo angeweza kuchangia, na kila kitu kilihuus alivyo machoni mwa Mungu. Ni pale tu tunapoelewa thamani yetu ya msingi, kustahili, kukubalika na kuthibitishwa mbele za Baba mbinguni ndipo tunaweza kuwa huru mbali na mfumo usio na msimamo wa maadili katika dunia hii ambao unategemea uzalishaji wetu na utendaji wetu. Hapo peke yake ndipo tunapokuwa huru kutumikiana kutoka katika nafasi hiyo kamili ya nguvu tuzipatazo kutoka kwa Mungu." (Mills 1986: 182-83)

3. mst. 38-50—Asili ya Uanafunzi

Sehemu hii in aanza tena na kejeli nyingine: ndio tu wanafunzi wametoka kuambiwa wawe "*watumishi wa wote*" na "*kumpokea mtoto kwa jina langu,*" nab ado walitaka kumkataza mtu aliye kuwa anatoa pepo kwa jina la Yesu (wakati wao wenyewe walikuwa wameshindwa)! Katika **mst. 39-40**, Yesu anaongezeka kivitendo. Swala lililoko katika **mst. 40** ("*aliye upande wetu hayuko kinyume chetu*") ni tofauti na swala la **Mat 12:30** ("*yeyote asiye upande wetu yuko kinyume chetu*"). Katika Mathayo, swala lilikuwa utu wa Yesu kama alikuwa amepagawa au la; hapa, swala ni mahusiano yetu na wengine ambao ni wafuasi wa Kristo. Maneno na maonyo ya Yesu **mst. 40-42** inafaa isikike na kusikilizwa na kila Mkristo na makanisa na madhehebu yote, ambayo mengi ya hayo hawawezi kushirikiana au kufanya kazi pamoja na waamini wa madhehebu tofauti na yao. Kama Royce Gruenler anavyosema, "Alichomaanisha Yesu katika maonyo yake katika mst.ari wa 42 ni kwamba wanafunzi, kwa kumkana mtu aliye kuwa na ukarimu wa Kristo, kwamba anasimama na ibilisi (kama Petro katika 8:33 ambaye anasimama kinyume na utumishi wa mateso wa Yesu) na anakuwa katika hatari ya kumzuia asitumike katika jina la Yesu (na hivyo kuhesabiwa anatenda dhambi). Hii ni kejeli, kwa kuwa wanafunzi wanakuwa katika hatari ya kuangamia, kama yule mtu aliyetupwa baharini akiwa amefungiwa uzito . . . kama wanaendelea katika ubiniasi wao na mawazo ya ukuu na marupurupu badala ya utumishi katika jina la Yesu (mada inayoleta pamoja ya 9:33-42)." (Gruenler 1989: 785)

Maneno ya Yesu katika **mst. 43-48⁴⁷** kuhusu kukata mkono au mguu au kung'oa jicho linalokufanya utende dhambi ni wazi hayakulengwa kuchukuliwa kama yanavyosema, lakini ni namna ya kutia chumvi sana au kukazia umuhimu wa kuishi maisha ya kweli ya Kikristo na kutokuwatoshwa wengine kwa mwenendo wetu. Katika **8:34-38** Yesu amezungumzia kuhusu kujikana mwenyewe, kubeba msalaba ili kumfuata, na mtu kupoteza maisha yake kwa ajili ya Kristo na injili. Katika **mst. 43-48** anakazia alichokisema pale, ni hapa tu ambako hazungumzii maisha mazima ya mtu, isipokuwa sehemu mojamoa! Anatumia lugha ya picha kama hiyo hapa kwasababu yay ale yanayotokea: kuna hatima mbili tu za milele zinazowasubiri wanadamu: ama "uhai" au "moto" yaani, moto usiozimika.⁴⁸ Lugha ya **mst. 48** inatoka kwa **Isa 66:24** ambako anasema, "*Nao watatoka nje na kuitazama mizoga ya watu walioniasi; maana funza wao hatakuifa, wala moto wao hautazimika nao watakuwa chukizo machoni pa wote wenyewe mwili.*" Kristo anatuambia kwamba maisha yetu, tunavyoyaendesha, na mahusiano yetu naye ni tunu na ya muhimu. Kwahiyo, ni lazima tudumu katika kukumbuka hili na kutathimini hali zetu za ndani, maneno yetu, na mwenendo wetu ili kuhakikisha tunabakia katika njia inayopeleka uzimani.

Mistari 49 unaunganisha **mst. 48** na **mst. 50**, kwa kuwa yote inabeba wazo la "moto" na "chumvi." Katika **mst. 33-50** Yesu amejadili ni namna gani tunapaswa kuishi kama wanafunzi wake, na amekazia matokeo yasiyo namwisheso kwetu kulingana na uchaguzi wetu. Hivyo, **mst. 49** unaonekana kubeba mambo ya mbele na matumizi ya wakati huu. Kama vile itakavyokuwepo hukumu hapo mbeleni ambapo matendo

⁴⁷ Mistari 44 na 46, ambayo inafanana na **mst. 48**, haipo katika magombo ya kale.

⁴⁸ Hili limejadiliwa kwa kina zaidi katika Menn 2017: 20-24.

yetu yote yatajaribiwa na kutakaswa kwa moto wa hukumu ya utakatifu wa Mungu (angalia **1 Kor 3:13**), tunawenza kutarajia dhiki, majaribu, na mateso katika maisha haya, kama njia ya Mungu ya kutuleta katika kumfanania Yesu Kristo (angalia **Rum 8:29**). **Mst. 50** inachukua sura ya chumvi na kuitumia katika maisha yetu ya sasa. Kama vile chumvi ilivyotiwa katika dhabihu za AK (angalia **Law 2:13**), tunapaswa “*kuwa na chumvi*” kwakuwa maisha ya Mkristo yanapaswa kuwa “*sadaka iliyo hai*” (**Rum 12:1**). Chumvi inafanya kazi ya kuhifadhi; hivyo, Mkristo mmoja mmoja na kanisa linapaswa kuhifadhi kile kilicho chema na cha kweli katika jamii kuzuia jamii isioze. Na kama chumvi inavyoleta ladha, Mkristo mmoja mmoja na kanisa wanapaswa kuleta ladha ya mbinguni. Lakini Kristo anawaonya wanafunzi wake, “*kama chumvi ikipoteza ladha yake, itatiwa nini hata ikolee?*” Kwa mara nyiningine tena anatuonya, kama alivyofanya katika **mst. 42-48**, kutukumbusha namna itupasavyo kuishi, kwa kuwa maisha yana thamani ya milele.

MASWALI YA KUJADILI

1. Kwanini unafikiri Yesu alichagua mtoto kama kielelezo cha kufundishia ukuu halisi katika ufalme?
 - **Mst. 42** unatuweka katika nafasi gani katika mahusiano yetu watu amba ni wadhaifu kuliko sisi?
 - Ingeleta maana gani kwako kuonesha mfano **mst. 35-37, 41-42** katika familia yako, kazini kwako kwa jirani yako?
 2. Kile alichosema Yesu katika **mst. 40** kina maana yejote kwa mtu yejote mmoja mmoja au kundi la Wakristo unaowasema vibaya au usio shirikiana nao? Kama ndivyo, ni mabadiliko gani (kama yapo) utayafanya katika mahusiano na watu au makundi kama hayo?
 3. Ipi ni mifano ya mkono, mguu, jicho lako linalokukosesha? unashughulikaje na hili? unapaswa kushughulika nalo kwa namna gani?
 4. Katika sehemu mbalimbali za Marko, Yesu ametuambia masharti ya uanafunzi katika kuwachukulia wengine na sisi wenyewe (mfano, **7:6-23, 8:34-35, 9:35-50**). Weka kwa kifupia nini maana ya uanafunzi na nini tunapaswa kufanya katika kuchukuliana na:
(A) wengine, na (B) sisi wenyewe. (Katika kutengeneza jibu lako unaweza pia ukarejea mistari yejote katika injili yejote ambako Yesu anajadili asili ya uanafunzi.)
- 10:1-12:** ¹ *Akaondoka huko akafika mipakani mwa Uyahudi, na ng'ambo ya Yordani; makutano mengi wakakutanika tena wakamwendea; akawafundisha tena kama alivyozoea.* ² *Basi Mafarisayo wakamwendea, wakamwuliza, Je! Ni halali mtu kumwacha mkewe? Huku wakinjaribu.* ³ *Naye akajibu, akawaambia, Musa aliwaamuru nini?* ⁴ *Wakasema, Musa alitoa ruhusa kuandika hati ya talaka na kumwacha.* ⁵ *Yesu akawaambia, Kwa sababu ya ugumu wa miyo yenu aliwaandikia amri hii.* ⁶ *Lakini tangu mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, aliwfanya mume na mke.* ⁷ *Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe;* ⁸ *na hao wawili watakuwa mwili mmoja; hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja.* ⁹ *Basi alichokiunganisha Mungu, mwanaadamu asikitiganishe.* ¹⁰ *Hata nyumbani tena wanafunzi wakamwuliza habari ya neno hilo.* ¹¹ *Akawaambia, Kila mtu atakayemwacha mkewe na kuoa mwingine azini juu yake;* ¹² *na mke, akimwacha mumewe na kuolewa na mtu mwingine, azini.*

mst. 1-12—Yesu anafundisha kuhusu talaka

Kwa kushuka kutoka Galilaya kuingia Yudea na kisha ng'ambo ya Yordani, Yesu alikuwa ameingia katika himaya ya Herode Antipa na Herodia. Kwahiyo inavutia zaidi kwamba Mafarisayo walimjaribu kwa swali kuhusiana na talaka, kwakuwa ni mahubiri ya Yoh Mbatizaji dhidi ya Herode Antipa kumtaliki mke wake na kumuoa mke wa ndugu yake ndiyo yaliyopelekea Yoh kukamatwa na hatimaye kuuwawa. Kinyume chake, Mafarisayo wanaonekana kuvutiwa na upekee wa kanuni ya uaminifu kati ya mume na mkewe kuliko uaminifu wenyewe. Hili ni muhimu mara dufu zaidi kwa kuwa wanazungumza Bwana harusi mwenyewe (**Mat 9:15; Marko 2:19-20; Luka 5:34-35; Yoh 3:29; Ufu 22:17**) anayewaita Israeli katika ndoa nao tena (**2 Kor 11:2; Ef 5:25-27; Ufu 19:7**). Mafarisayo, hata hivyo, wanawaongoza watu katika uzinzi wa kiroho kwa kumkataa Yesu, kama viongozi wa Israeli walivyokosa uaminifu kwa Mungu katika siku za Hosea (angalia **Hos 2**). Royce Gruenler analiweka hili hivi, “kama ambavyo Herode na Herodia walivyotenda uzinzi katika viwango nya kimwili na kiroho na kumuua nabii pekee ambaye angeliwaokoa, kadhalika Mafarisayo wanatenda uzinzi kwa kumkataa bwana harusi pekee ambaye anaweza kuwaokoa, Yesu aliye Masihi” (Gruenler 1989: 786).

Mistari 3-4 inarejea kwa **Kumb 24:1-4**, iliyoruhusu mume kumtaliki mkewe “*kama asipopendezewa naye*” (**Kumb 24:1**). Mambo yaliyohusika na “kutokupendezewa” yamezaa shule za mawazo tofauti tofauti. Wake Israeli hawakuruhusiwa kataliki waume zao, ingawa angeweza kwende mahakamani na kumlazimisha amtaliki kwasababu mbalimbali (angalia Lane 1974: 358n.19; Wessel 1984: 711).

Jibu la Yesu kwa Mafarisayo na maelezo yake ya faragha kwa wanafunzi wake vinafanya mambo mawili. Kwanza, anarudi nyuma hadi mwanzoni, kabla ya Musa, akirejea **Mwa 1:27** na **2:24**. Anaonesha kuwa talaka yejote ni matokeo ya “*ugumu wa miyo*” (**mst. 5**) nan i kinyume na mapenzi ya Mungu, kwa kuwa Mungu aliumba wanadamu mume na mke, akaanzisha ndoa, akitamanikwamba wanandoa wawe na umoja (“*mwili mmoja*”), na akitaka ndoa iwe ni ya kudumu (**mst. 6-9**). Yesu alikuwa anarudi nyuma katika mapenzi ya Mungu kuhusiana na ndoa, kwasababu ndoa hatimaye ni ya kiroho. Ndoa—kama Mungu alivyoiweka inapaswa—kuakisi upendo wa kina na mshikamano wa utatu wenyewe. Mshikamano na utakatifu wa ndoa unaakis mahusiano ya Kristo na bibi harusi wake, kanisa (**Ef 5:25-32**; angalia pia **Yoh 17:21**). Matokeo yake, Wakristo lazima waelewe umuhimu na maana ya ndoa zao na kufanya wanachowenza kufanya ili kuifanya iwe ya furaha, muunganiko wenye matunda ambao Mungu aliuukusudia. Pili, katika kuelezea kwake kuhusu talaka, Yesu aliinua heshima na hadhi ya mwanamke.⁴⁹ ⁴⁹ Kwa sharia za Kiyahudi, mke kukosa uaminifu ilikuwa ni uzinzi dhidi ya mumewe; kama mume angefanya uzinzi na mke wa mtu mwingine, anakuwa amefanya uzinzi dhidi ya huyo mume mwingine, lakini “mume kamwe asinghesabiwa kufanya uzinzi dhidi ya mke wake, bila kujali amefanyaje” (Wessel 1984: 712). Kwa kusema “*yeyote anayetaliki mkewe na kuoa mwingine afanya uzinzi dhidi yake*” (**mst. 11**), Yesu alikuwa anamuweka mume chini ya wajibu ule ule wa kimaadili kama mke, na hakuinua heshima na hadhi ya mwanamke. Na kwa kusema “*kama akimaliki mkewe*” (**mst. 12**), alikuwa anaweka haki ya wake na waume kuwa na haki sawa katika kupata talaka, hivyo, kuinua heshima ya mwanamke.

MASWALI YA KUJADILI

1. Katika **Marko 2:19-20**, Yesu anajieleza kama bwana harusi; na sisi ni, bibi harusi wake. Kuna funzo gani au umuhimu gani wa maelezo ya Yesu kuhusu ndoa na talaka kwetu kama Wakristo? Kwa namna gani (au tunapaswa) kuathiriwa na namna tunayoishi maisha yetu?
2. Unafikiri ni kwa namna gani Yesu angeitikia kama angeulizwa swali kuhusiana na talaka kama angeulizwa na mtu aliyekuwa na nia ya dhati ya kujua kwa kuwa alikuwa amenasa katika mahusiano ambayo yenye matatizo na udhalilishaji?

10:13-16: ¹³ *Basi wakamletea watoto wadogo ili awaguse; wanafunzi wake wakawakemea.* ¹⁴ *Ila Yesu alipoona alichukizwa sana, akawaambia, Waachen i watoto wadogo waje kwangu, msiwazie; kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao.* ¹⁵ *Amin, nawaambieni, Ye yote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa.* ¹⁶ *Akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, akawabarikia.*

mst. 13-16—Yesu anawabariki watoto wadogo

Katika **9:37** Yesu aliwaambia wanafunzi wake, “*Ampokeaye mtoto kama huyu kwa jina langu anipokea mimi, na hanipokei mimi bali baba aliyenitura.*” Sasa, la kushangaza, wanafunzi bado hawajajifunza lakini wanawakemea watu walioletea watoto wao ili Yesu awabariki! Kisha, kinyume chake, Yesu anawaambia wanafunzi wake kwamba lazima *wawe* kama watoto kama wanataka kuingia katika ufalme wa Mungu. **Mistari 14** ni mahali pekee katika Biblia ambapo Yesu anatajwa kuwa “alikasirika,” jambo ambalo ni hisia kali za kutokupendezwa na jambo au mtu ambaye hatendi haki au anaudhi. Hapa anawakasirikia wanafunzi wake kwasababu, kwa maneno na matendo yao, wana mtazamo potofu juu ya kustahili kwa watoto (angalia majadiliano **9:36-37**, hapo juu), na hapo wanawasilisha isivyo asili ya ufalme, wanawasilisha isivyo gharama za kuingia katika ufalme, na hivyo kumuwasilisha Yesu Kristo mwenyewe

⁴⁹ Rikk Watts anaongeza maoni haya mawili: “Kwanza, kama tamko la mwisho la Yesu (10:9) litachukuliwa kuwa linamaanisha ‘hakuna talaka’ kwa hali yejote ile, basi litakuwa jambo lisilofaa siyo kwa Musa tu, lakini hata kwa Mungu mwenyewe, ambaye wakati fulani yeeye mwenyewe alilazimika kumpa talaka Israeli (i.e., ufalme wa kaskazini) (Yer. 3:8). Ukweli kwamba Yesu hasemi chochote kuhusu talaka isiyo ‘na kasoro’ uenda ikaeleweka vema kama kukubaliana na vigezo viliviyotajwa katika Kut. 21:10-11 (na kisha kuleta upekee wa Mat. 19:9 na maagizo ya Paulo katika 1 Kor. 7:10-16). Lakini, pili, kwa kufuata lielelezo cha Yahwe, talaka hata katika misingi hiyo siyo lazima, na kupatana na kusameheana yafaa kupendelewe zaidi.” (Watts 2007: 199)

na injili isivyo sawasawa.

Hili, kwa mara nyiningine tena, ni igizo la mfano wa injili na ufalme. Yesu kuwachukua watoto mikononi mwake na kuwabariki (**mst. 16**) inaonesha kuwa ufalme ni kitu kinachopokelewa, siyo kitu kinacho fanyiwa kazi ili kukipata. Wakati **mst. 16** unasesma kwamba “*akawabariki*,” neno la Kigiriki lililotumika ni (*kateulogeji*) halikutumika pengine katika Agano Jipyä na lina nguvu yenye maana ya “aliwabarikia kwa moyo wake kabisa, akirudia rudia” (Swift 1970: 872). Hili pia laonesha asili ya Yesu, Injili, ufalme, na upendo wa Kristo kwa watu wake.

MASWALI YA KUJADILI

1. “*Kupokea ufalme wa Mungu kama mtoto*” (**mst. 15**) kuna maana gani? Ni sifa zipi za mtoto Yesu alikuwa anaziibua?

2. Unafananaje na mtoto katika kifungu hiki?

- Unafananaje na wanafunzi?
- Nini katika maisha yako kinakuzuia usipokee utimilifu wa ufalme wa Mungu sasa?

10:17-31: ¹⁷*Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mtu mmoja akaja mbio, akampigia magoti, akamwuliza, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?* ¹⁸ Yesu akamwambia, Kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu. ¹⁹ *Wazijua amri, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, Usidanganye, Waheshimu baba yako na mama yako.* ²⁰ Akamwambia, Mwalimu, haya yote nimeyashika tangu utoto wangu. ²¹ Yesu akamkazia macho, akampenda, akamwambia, Umepungukiwa na neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate. ²² Walakini yeeye akakunja uso kwa neno hilo, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyangi.

²³ Yesu akatazama kotekote, akawaambia wanafunzi wake, Jinsi itakavyokuwa shida wenye mali kuingia katika ufalme wa Mungu! ²⁴ Wanafunzi wakashangaa kwa maneno yake. Yesu akajibu tena, akawaambia, Watoto, jinsi ilivyo shida wenye kutegemea mali kuingia katika ufalme wa Mungu! ²⁵ Ni rahisi ngamia kupenya katika tundu ya sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. ²⁶ Nao wakashangaa mno, wakimwambia, Ni nani, basi, awezaye kuokoka? ²⁷ Yesu akawakazia macho, akasema, Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyo; maana yote yawezeekana kwa Mungu.

²⁸ Petro akaanza kumwambia, Tazama, sisi tumeacha vyote tukakufuata wewe. ²⁹ Yesu akasema, Amin, nawaambieni, Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu, na kwa ajili ya Injili, ³⁰ ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele. ³¹ Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho; na wa mwisho watakuwa wa kwanza.

mst. 17-31—Yesu na kijana tajiri

Katika **mst. 17-18** wakati mtu yule alipopiga magoti mbele ya Yesu na kumuuta “mwalimu mwema,” na Yesu kujibu “*Kwanini unaiita mwema? hakuna mwema isipokuwa Mungu peke yake,*” hakuwa anakana kuwa yeeye siyo Mungu. Badala yake, alikuwa anathibitisha uungu wake kwa kumuuliza swali ambalo halikuhitaji jibu. Kutokana na hilo, alikuwa anawaambia, “hivi unajua hasa ni nani unaongea naye?” Kama Victor Babajide Cole anavyooleza, “Yesu hakuwa anakana kuwa hakuwa “Mungu.” Badala yake, alikuwa anataka yule mtu aweze kuona maana ya kumuuta “mwema”, yaani yeeye ni Mungu!” (Cole 2006: 1189)

Kama ilivyo kwa wengi waliokutana na Yesu, kuna kejeli hapa. Kwanza, ni lile swali la mtu yule, “*Nifanye nini kuurithi uzima wa milele?*” “hurithi” kitu kwa “kufanya” kitu; urithi ni zawadi ambayo siyo malipo. Jibu la Yesu kwa swali la mtu yule linatolewa kutoka katika amri ya pili, yaani mahusiano yetu na watu wengine. Yesu alikuwa ameweka kwa kifupi mafundisho yote ya sheria katika amri mbili: “NAWE UTAMPENDA BWANA MUNGU WAKO KWA ROHO YAKO YOTE, NA KWA MOYO WAKO WOTE, NA AKILI ZAKO ZOTE. Hii ndiyo amri iliyo kuu. Na ya pili yafanana nayo, UTAMPENDA JIRANI YAKO KAMA NAFSI YAKO. Katika hizi torati yote na manabii hukaa.” (**Mat 22:36-40**; angali pia **Marko 12:28-31**) “*Nawe utampenda jirani yako kama nafsi yako*” inaitwa “sheria ya ufalme” (**Yak 2:8**) na inakamilisha sheria yote (**Rum 13:8-10; Gal 5:14**). Sababu ya Yesu kunukuu amri ya pili ni kwamba watu wote wameumbwa kwa sura ya Mungu; namna tunavyoitendea sura ya Mungu inaonesha tunavyofikiri kuhusu Mungu. Kwa maneno mengine, tunayofanyia watu ni kipimo na uthibisho wa uhalisia na ukweli wa imani yetu kwa Mungu. Mtume Yoh anaandika hivi, “*Mtu akisema, ‘Nampenda Mungu,’ naye anamchukia ndugu*

yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezu kumpenda Mungu ambaye hakumwona.” (1 Yoh 4:20).

Yesu alimpeleka mtu huyu kwenye sheria kumuonesha (na sisi) kwamba sheria haiwezi kukuokoa au kukupa uzima wa milele. Mtu yule alisema kwamba ametunza kila kitu katika sheria ambayo Yesu ameisema, nab ado alijua anapungukiwa na kitu. Ukweli kwamba sheria haiwezi kutuokoa, au kutufanya wenyе haki, au kubadilisha miyo yetu limewekwa wazi katika AJ lote (angalia, kwa mfano, **Rum 3:20; 4:14-15; 7:14-24; 8:1-4; Gal 2:16; 3:1-25; 4:4-5; Ebr 7:19; 10:1-4**). Hii ndio maana Yesu aliwaambia, “*Umepungukiwa na kitu kimoja: nenda, ukauze vyote ulivyo navyo na kuwapa maskini, na utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate.*” Kimsingi, jibu lote la Yesu lilikuwa linamhusu yeye mwenyewe kama “mwema,” Yaani, Unasema umeitii sheria yote—lakini sheria haiwezi kukuokoa na kukupa uzima wa milele, na unatambua hivyo—hivyo sasa, utaweza kunipa nafasi ya kwanza na kunifuata, kwasababu ni mimi tu niwezaye kukupa uzima wa milele.” Injili—na wokovu wa watu—ina msingi katika kile ambacho Kristo ametenda; wokovu si “mapato” kwa kutenda “matendo mema.” Badala yake, wokovu *unatolewa* kwa watu na Mungu kama *zawadi ya neema* yake; *unapokelewa* na watu kwa *imani* tu katika Kristo.⁵⁰ Kama **Ef 2:8-9** inavyosema, “*Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.*” Kuokolewa maana yake ni kutubia dhambi zetu, kupokea kwa imani kile ambacho Kristo ametenda kwa ajili yetu, na kumgeukia Kristo kama Bwana wa maisha yetu (**Mat 11:28; Marko 1:14-15; Yoh 1:12; 3:16; 17:3; Mdo 26:20; 1 Yoh 1:8-9**). *Ukiri wa Imani wa Westminster* (1646) unaandika kwa mukhtasar: “Tendo kuu la imani iokoayo ni kukubali, kupokea, na kujichia kwa Kristo peke yake atuhesabie haki, na uzima wa milele” (Westminster 1646: XIV:2).

Siyo tu kwamba Yesu alikuwa anamkabili mtu yule na ukweli kwamba sheria haiwezi kutuokoa lakini pia alikuwa anamkabili kwa atathimini kile ambacho hasa ndicho muhimu kwake. Katika hili, ilikuwa ni pesa na mali zake. Huyu mtu alimkimbia Yesu, akapiga magoti mbele yake, akamtambua kuwa ni mwema, alitamani uzima wa milele, na alitambua hali yake ya ndani ya kutokutoshalezw. Jambo moja—muhimu—ambalo hakuwa tayari kutii lilikuwa *kumtii* Yesu. Bila kumtii, alikuwa anaweka wazi kwamba hakuwa akimwabudu (liche ya alama za nje za ibada [kupiga magoti]). Kile tunachofanya na pesa zetu ni alama za nje za zinazoonekana za kile hasa kilicho muhimu kwetu, yaani, nani ambaye hasa ndiye Bwana wetu. Ni kweli, hakika, mtu kuuza vitu vyake vyote na kuwapa maskini ni kujitoa kusiko kwa kawaida, na kungeweza kuathiri wanafamilia ambao huenda walimtegemea. Hata hivyo, Elisha alijitoa kiasi hicho kumfuata Eliya (**1 Fal 19:19-21**) na wengine wengi katika historia yote. Mtu huyu tajiri anawakilisha watu wote wanojaribu kupata thamani yao usalama wao kutoka katika vitu vya dunia. Kama Yesu alivyosema kwa kanisa la Laodikia, “*Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi.*” (**Ufu 3:17**). Yesu alikuwa anamwambia mtu yule, kama alivyoliambia kanisa la Laodikia, “Hakika unaweka thamani na usalama wako katika pesa na unavyomiliki, badala ya kuweka kwangu. Nitumainie. Nastahili kutumainiwa na nitathibitisha hivyo kwa kwenda msalabani kwa ajili yako. Mali zako ziwe nzuri kiasi gani, zitatoweka kufumba na kufumbua na haizitakuokoa, wakati ukitii na kunifuata mimi, utakuwa na *hazina mbinguni* (**mst. 21**) itakayodumu milele.” Mtu yule (na sisi) tunahitaji kutambua kile alichosema Agustino, “Wewe ndiwe uliyetuumba kwa ajili yako, na mioyo yetu isiyotulia hupata pumziko kwako” (Augustine 1942: 1.1.1) Blaise Pascal anaeleza kitu kama hicho, “Kuliwahi kuwepo na furaha ya kweli kwa mtu ambapo sasa kwake kumesalia alama tu na utupu, ambao bila mafanikio anajaribu kuijaza kutoka katika yale yanayomzunguka, akitafuta kutoka kwenye vitu ambavyo havipo msaada asioweza kuupata katika vitu vilivyopo? Lakini yote hayo hayatoshi, kwasababu shimo lisilo na mwisho linaweza kujazwa tu na vitu visivyo na mwisho, hii ni kusema, ni Mungu tu mwenyewe.” (Pascal 1958: VII.425)

Katika **mst. 23-27**, maneno ya Yesu juu ya ilivyo vigumu kwa mtu tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu yalivyoamsha mshangao kwa wanafunzi kwasababu walifikiria utajiri kuwa alama ya kibali na Baraka ya Mungu. Wakati ni kweli kwamba Mungu “*hututajirisha kwa kila kitu ili tufurahi*” (**1 Tim 6:17**), Yesu anatambua kwamba kuna hatari kubwa ya kiroho katika mali (angali **Mith 30:8-9**). Wale walio na vingi hujitumainia wenyewe, wanategemea pesa na mali zao, wakiogopa kupoteza pesa na mali zao, na kukana kumtegemea Bwana. Mtu yule tajiri aliyemjia Yesu alikuwa amebeba hali zote hizo. Katika **mst. 27** Yesu anaweka wazi kwamba wokovu ni kazi ya Mungu kwa asilimia 100%, siyo kazi ya mtu.

Jibu la Petro kwa Yesu katika **mst. 28** kwamba “*tumeacha vyote na kukuftuwa wewe*” una umuhimu mkubwa: “*Yesu akasema, Amin, nawaambieni, Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu*

⁵⁰ Ona kwamba katika sehemu hii yote, “uzima wa milele,” “kuwa na hazina mbinguni,” “kuingia katika ufalme wa Mungu,” na “wokovu” yote yanatumika kwa kubadilishanwa kama maneno yenye maana moja.

wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu, na kwa ajili ya Injili,³⁰ ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele.³¹ Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho; na wa mwisho watakuwa wa kwanza.” (**mst. 29-31**) Wengi mionganoni mwa wale wanaoitwa wahubiri wa “injili ya mafanikio” huchukulia neno utarudishiwa “mara mia”njie ya muktadha halisi na kuwaambia watu wapande “mbegu ya imani,” wakidai, “Kila dola (faranga, shilingi, n.k.) utakayota katika huduma hii, Mungu atakurudishia mara 100.” Yesu hasemi chochote cha aina hiyo. Muktadha wa kifungu hicho hauhusiani kabisa na watu “kupanda mbegu ya imani” kwa kutoa kwa huduma ya mtu fulani. Hakika, wala pesa haitajwi katika kifungu hicho. Badala yake, kinaangalia wale amba “*wameacha kila kitu na kumfuata*” [Yesu][”] (**10:28**). Yesu ndio ametokea kumwambia yule mtu tajiri “*nenda ukauze vyote ulivyo navyo na uwape maskini*” (**10:21**). Yesu hakumuahidi mtu yule kwamba kama akiiza mali zake na kuwapa maskini atapata pesa zaidi hapa duniani. Badala yake, Yesu alisema kwamba “*utakuwa na hazina mbinguni*” (**10:21**). Hakika, mbali na kumuahidi mtu kwamba kutoa kutampatia pesa na utajiri, Yesu anaonya, “*Jinsi gani ni vigumu kwa wenye mali kuingia katika ufalme wa Mungu! . . . ni rahisi kwa ngamia kupenya katika tundu la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu.*” (**10:23, 25**).

Muktadha ulihusiana na maandalizi ya Yesu kwa wanafunzi wake kwa huduma yao ya kitume katika dhiki. Hivyo, sehemu ya yale ambayo Yesu aliahidi kama ni “malipo” kwa kujitoa kwake ni “dhiki” (**10:30**). Mada ya dhiki na unyenyekevu inaendelezwa katika **10:32-45**. Yesu anazungumzia kuhusu mtu atakayeiacha nyumba yake *au ndugu wa kiume au wa kike au mama au baba au watoto au ardhi, kwa ajili yake na injili* ambaye hatapokea “*mara mia sasa wakati huu, nyumba na ndugu waume na ndugu wa kike na mama na watoto na ardhi, pamoja na dhiki, na katika ufalme ujao uzima wa milele*” (**mst. 29-30**). Yesu anasema nini hapa? Jibu ni kwamba anarejea waamini sasa kuwa *familia mpya* katika Kristo. Tunapokuwa tumeokolewa, Mungu anatuasili katika familia yake (angalia **Rum 8:15-17; Ef 1:5**). Kanisa kipekee linaitwa “*kaya [au, familia] ya Mungu*” (**1 Tim 3:15**; angalia pia **1 Tim 5:1-2**). Dhati Lewis anatuonesha, “Kanisa siyo *kama* familia; *ni* familia. . . . Hili linawezza kuonesha na ukweli kwamba neno *mwanafunzi*, lililokuwa limezoleka sana wakati wa sehemu ya kwanza ya kanisa la Agano Jipy, linapotea baada ya kitabu cha Matendo. Linawakilishwa na neno “*ndugu*” hadi mwisho wa biblia.” (Lewis 2015: n.p.) Kama Sarles navyooleza, “Wanafunzi walipopoteza nyumba zao kwa ajili ya injili, waliweza kupewa nafasi katika nyumba za waamini wenzao amba walizitumia katika kuzunguka kwao wakihubiri injili. Kadhalika wakati wanafunzi walipoacha familia zao kwa ajili ya Yesu, waliingia katika ushirika mpya katika familia ya Mungu ambayo ilikuwa mara mia zaidi kwa ukubwa.” (Sarles 1986: 338) La kuvutia, hata hivyo, Yesu *hazungumzii* mtu kuacha mke wake au mume. Katika nuru ya kile alichosema katika **10:7-9**, Yesu anasema kwamba ni kifo tu—siyo Yesu na injili—kinachowenza kutenganisha muunganiko wa ndoa. Hakika, Petro na wanafinzi wengine walisafiri na wake zao (**1 Kor 9:5**).

Mwisho, **mst. 31** (“*wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, na wa mwisho wa kwanza*”) unarejea kwenye hukumu “Mungu atakapopima maisha ya watu na maadili ya wanadamu yatakobadilishwa. Wakati huo wale wenye vyeo na nafasi hawatakuwa navyo, na wale wasio na vyeo sasa watakuwa navyo. Haya yanaweza kuwa kama mukhtasari wa mafundisho ya Yesu katika mst. 17-31.” (Wessel 1984: 717) Yanaweza pia kuwa maonyo kwa wanafunzi katika nuru ya kuwa “*wameacha vyote na kukufuata*” (**mst. 28**) kwamba “haiwapasi kuelewa uanafunzi wao kama malipo. Uanafunzi unabeba mateso na kutumikia; lazima kuuingia kwa upendo na kujitoa kwa Yesu, siyo kwasababu ya kile tunachotaraja kupokea kutokana na kazi hiyo ama katika maisha haya au katika uzima wa milele.” (Ibid.)

MASWALI YA KUJADILI

1. Kwanini Yesu aliguswa kuongelea nano “mwema” (**mst. 17-18**)?
2. Kwanini Yesu katika kujibu swalii la yule mtu la nifanyeje nipate kuurithi uzima wa milele alimpeleke kwanza kwenye amri kumi? Ona kwamba kipekee amri zote alizonkuu Yesu alizitoa katika sehemu ya *pili* ya amri kumi za Mungu (mahusiano yako na wengine), na siyo katika sehemu ya *kwanza* ya amri kumi za Mungu (mahusiano yako na Mungu) Kwanini alifanya hivyo?
3. Ni kwa namna gani kifungu hiki kinahusu namna tunavyopaswa kuchukulia pesa na mali *zetu*? Kutokana na hili, pitia injili zote na tafuta mahali pengine Yesu alizungumza kuhusu pesa na mali.
4. Tunaazima mbinu za Shetani katika uinjilishaji kwasababu tunashauku sanaya kuona mtu anasema “maneno ya kichawi” ya “sala ya toba” kiasi kwamba hatutangulii kutaja maana na gharama ya kuwa mwongofu na kuwa mwanafunzi katika maisha ya mtu? Matokeo ni nini kwa njia kama hiyo katika

uinjilishaji?

5. Katika **mst. 29-30** Yesu anatumia lugha ya *familia kujadili jamii ya Kikristo* (*yaani, Kanisa*). Yapi yapo (au yanapaswa kuwa) maana ya yale anayosema kwetu kama Wakristo mmoja mmoja na kama makanisa katika mahusiano yetu na waamini wengine?

10:32-45:³² *Nao walikuwako njiani, huku wakipanda kwenda Yerusalem; na Yesu alikuwa akiwatangulia, wakashangaa, nao katika kufuata wakaogopa. Akawatwaa tena wale Thenashara, akaanza kuwaambia habari za mambo yatakayompata,*³³ *akisema, Angalieni, tunapanda kwenda Yerusalem; na Mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa wakuu wa makuhani na waandishi, nao watamhukumu afe, watamtia mikononi mwa Mataifa,*³⁴ *nao watamdhihaki, na kumtemea mate, na kumpiga mijeledi, na kumwua; na baada ya siku tatu atafufuka.*

³⁵ *Na Yakobo na Yoh, wana wa Zebedayo, wakamwendea, wakamwambia, Mwalimu, twataka utufanyie lo lote tutakalokuomba.*³⁶ *Akawaambia, Mwataka niwafanyie nini?*³⁷ *Wakamwambia, Utujali sisi tuketi, mmoja mkono wako wa kuume, na mmoja mkono wako wa kushoto, katika utukufu wako.*

³⁸ *Yesu akawaambia, Hamjui mnaloliomba. Mwaweza kunywea kikombe ninyweachoo mimi, au kubatizwa ubatizo nibatizwao mimi?*³⁹ *Wakamwambia, Twaweza. Yesu akawaambia, Kikombe ninyweachoo mimi mtakinywea, na ubatizo nibatizwao mimi mtabatizwa;*⁴⁰ *lakini habari ya kuketi mkono wangu wa kuume au mkono wangu wa kushoto si langu kuwapa, ila wao watapewa waliokekewa tayari.*⁴¹ *Hata wale kumi waliposikia wakaanza kuwakasirikia Yakobo na Yoh.*⁴² *Yesu akawaaita, akawaambia, Mwajua ya kuwa wale wanaohesabiwa kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha.*⁴³ *Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu anayetaka kuwa mkubwa kwenu, atakuwa mtumishi wenu,*⁴⁴ *na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu, atakuwa mtumwa wa wote.*

⁴⁵ *Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.”*

mst. 32-45—Kwa mara nydingine tena Yesu anatabiri kifo na ufufuo wake na asili ya uanafunzi wa kweli

Matukio haya yanabeba hali ya kufanana ya kipekee na **9:30-37**. Bado wanafunzi hawaeliewi misheni ya Yesu, nab ado wana mitazamo ya kidunia ya hadhi na upendeleo badala ya unyenyekevu na utumishi.

1. mst. 32-34—Kwa mara nydingine tena Yesu anatabiri kifo na ufufuo wake

Kama ambavyo mara kwa mara amekuwa akifanya katika kitabu cha Marko, Yesu anawatenganisha wanafunzi na makutano ili awafundishe. Utabiri huu wa nne (mara tatu kwa wale kumi na wawili na kwa Petro, Yakobo na Yoh) kuhusu mateso na kifo chake hapa kinaleezwa kwa kina na kwa uwazi zaidi. Anatambulisha kuwa Yerusalemu ndipo mahali usaliti utakapofanyikia (**mst. 33**). Anaonyesha siyo tu kwamba makuhani wakuu na waandishi watamkataa Masihi, lakini pia kwamba atatiwa mikononi mwa “*Wamataifa*” (**mst. 33**). Kama vile ambavyo wote Wayahudi na Wamataifa watakavyohusika katika mateso na kifo chake, ndivyo ufalme wa Mungu unavyofunguliwa kwa Wayahudi na Wamataifa. Kisha anatoa maelezo ya kina yasiyopendeza kuhusu kile kitakachompata: “*Watamdhihaki na kumtemea mate, na kumpiga kwa mijeledi na kumuua*” (**mst. 34**). Kifungu kama hicho katika Mathayo kinarejea kwa hakika kwamba atauwawa kwa kusulubiwa (**Mat 20:19**). Katika mafundisho haya, alikuwa akirejea **Zab 22:6-7** na **Isa 50:6; 52:14; 53:5**. Kilele chake ni kwamba “*baada ya siku tatu atafufuka*” (**mst. 34**).⁵¹ Marko haandiki muitikio wa wanafunzi kuhusiana na hili, lakini katika injili nydingine ya Luka inasema, “*Lakini hawakuelewa na mambo haya. Mambo haya yalifichwa kwao, na hawakuelewa anasema nini.*” (**Luka 18:34**) Hivi ndivyo ilivyokuwa, kwa kuwa hata baada ya Yesu kukamatwa, kuhojiwa, kutiwa hatiani, kuhukumiwa kifo, kudhilihakiwa, kutemewa mate, kupigwa mijeledi na kusulubishwa, hakuna mwanafunzi hata mmoja aliyeonekana kukumbuka kuwa Yesu pia alisema angefufuka tena baada ya siku tatu.

2. mst. 35-45—Asili ya uanafunzi wa kweli

La kushangaza, Yakobo na Yoh walielewa kwamba Yesu alikuwa Masihi lakini bado hawakuelewa misheni yake ilikuwa nini. Hawakuwa wamejifunza chochote kutoka katika kile ambacho Yesu alikuwa ametoka kuwaambia kuhusu mateso ambayo muda si mrefu atakabiliana nayo au kutoka katika yale aliyokuwa amewaambia katika **9:30-37**, wakati wao na wanafunzi wengine walipokuwa wanajadili nani atakayekuwa mkubwa. **Mst.ari wa 41** unatuonesha kwamba wanafunzi wengine kadhalika hawakuwa wamejifunza chochote, kwa kuwa walikuwa wamejisikia vibaya na kwa vyovyyote waliridhika kuwa “nafasi ya pili bora” licha ya kuwa “*wadogo*” au “*wa mwisho*.”

⁵¹ **Mat 20:19** inasema “*naye atafufuka siku ya tatu.*” Kwa majadiliano ya hakika ya namna maneno haya “siku tatu” yanavyotumika na kumaanisha kitu kile kile, angalia n.40, hapo juu.

Matamshi ya Yesu kwao katika **mst. 43-45**, “⁴⁵*Na mkono wako ukikukosesa, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili, na kwenda zako jehanum, kwenye moto usiozimika; ⁴⁴ ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.*⁴⁵ *Na mguu wako ukikukosesa, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima, u kiwete, kuliko kuwa na miguu miwili, na kutupwa katika jehanum*” kwa mara nyine tena anaelezea asili ya uanafunzi. Ni kulingana na jinsi alivyolezea uanafunzi wa kweli katika **8:34-38** alipotangaza kwa mara ya kwanza kuwa angeteseka na kufa. **Mistari 40-44** anaeleza kwamba, wakati *kuingia* katika ufalme ni zawadi, kutakuwepo na *nafasi* mbalimbali na *thawabu* katika ufalme ambazo zitategemeana na uaminifu katika utumishi (angalia Mat 6:20-21; 10:42; 19:21; 25:14-29; Marko 10:21; Luka 12:33-34; 19:12-26; 1 Tim 6:17-19). **Mistari 38-39** na **45** (kama alivyofanya katika **mst. 38**) akiunganisha maisha yake na maisha ya wanafunzi. Ni maneno yale yale “*Mwanafunzi hampiti mwalimu wake, wala mtumishi kwa bwana wake*” (Mat 10:24; angalia pia Yoh 13:16; 15:20). Wanafunzi wanapaswa kuishi kwa maadili yale yale ya “kitumishi” kama Yesu alivyoishi na kutarajia kutendewa kama aliviotendewa. Yote, “*kikombe*” na “*ubatizo*” vilikuwa ni alama za kustahimili matatizo, ikiwa ni pamoja na ghadhabu ya Mungu (angalia Zab 69:1-2, 15; 75:8; Isa 51:17; angalia pia Marko 14:36; Rum 6:3).

Sehemu ya mwisho ya **mst. 45** (“*kutoa maisha yake kama fidia ya wengi*”) kunaingia katika moyo wa injili. Kuwa “fidia” kwa watu ni kulipa bei ya ukombozi au kufunguliwa na inaonesha kuwa tulikuwa tumefungwa utumwani (kwa dhambi zetu ibilisi, na mauti) lakini sasa tumewekwa huru. Rejea kwa “wengi” inatupeleka katika **Isa 53:11-12** (angalia pia **Rum 5:15; Ebr 9:28**). Yesu alitambua kwamba msamaha mara zote ni mateso yenye gharama kubwa” (Keller 2008: 193). Wakati mtu fulani anapokuwa amekosewa na kuumizwa, jambo linalokuja kwanza ni kudai [mkosaji] aliye uharibifu aliouleta. La pili ni kumkatalia kulipa chochote. . . . Gundua kwamba kila uchaguzi una gharama ya uharibifu na ni lazima ibebwe na *mtu fulani*. Ama wewe au abebe gharama za yaliyotendwa, lakini deni kwa namna fulani halipotei hewani. . . . [Kumsamehe mtu maana yake ni kwamba] *wewe unachukua lile deni, unabeba gharama zote mwenyewe* badala ya kuziweka kwa mtu *mwingine*” na pia ina maana siyo tu kwamba unapata hasara lakini pia unakataa mkosaji kulipa alichoharibu. (Ibid.: 187, 189, emph. added) Hivyo, misamaha yote inahusisha kuteseka—na kadiri kosa na jeraha lilivyo kubwa, ndivyo gharama na mateso yanavyokuwa kwa anayesamehe.

Ughali wa dhambi zetu na nini kilimgharimu Mungu kutusamehe (yaani, “*Mwanawe pekee,*” **Yoh 3:16**) unafunuliwa na Yesu pale msalabani. Kile alichofanya Yesu msalabani ilikuwa ni kupokea hukumu , kulipa gharama, na kuchukua ju yake mwenyewe adhabu iliyopaswa wanadamu kuichukua: “Katika Mathayo 10:28 Yesu anasema kwamba hakuna uharibifu wa kimwili unaoweza kulinganishwa na uharibifu wa kiroho wa kuzimu, wa kupoteza uwepo wa Mungu. Lakini hili hasa lilimtokea Yesu pale msalabani-aliachwa na Baba (Mathayo 27:46). . . . Alipolia kwa sauti kwamba Mungu wake amemuacha alikuwa akipitia mateso ya kuzimu yenye. Lakini fikiria—kama deni letu la dhambi ni kubwa kiasi hicho kwamba halikulipwa kikamilifu pale, lakini kuzimu yetu inaendelea milele, basi nini tutahitimisha kutokana na ukweli kwamba Yesu alisema malipo “yalikamilika” (Yoh 19:30) baada ya masaa matatu tu? Tunajifunza kwamba msalabani alijisikia vibaya sana na kwa kina stahili yetu yote ya kuzimu ukiiweka pamoja. . . . Wakati Yesu alipotenganishwa na Baba alikwenda chini sana shimoni na kwenye moto wenye nguvu, mkali kuliko tunavyoweza kuwaza. Alipita katika ghadhabu kamili ya Baba. Na alifanya kwa hiari, kwa ajili yetu.” (Keller 2009: sec.4)

MASWALI YA KUJADILI

1. Uelewa wa Yesu kuhusu ukuu ulikuwaje? Unaulinganishaje na ule wa wanafunzi kuhusu ukuu?
2. Unafikiri swal la Yakobo na Yoh kwa Yesu (**mst. 37**) na muitikio wa wanafunzi kwa Yakobo na Yoh ulimfanya Yesu ajisikieje? (**mst. 41**)
 - Inamfanya Yesu ajisikieje, na kwani tuna uzuri gani wa kirho, *tunaposhindania heshima, nafasi, utajiri na mamlaka?*
 - Vipi kuhusu kushindania kuwa “kama Yesu” au kufanya mambo “kwa ajili ya Yesu” *kwa kusudi* la kupata “*thawabu*” inayofikiriwa au “*taji*” au heshima mbinguni katika umilele?
3. Kama kweli tumezaliwa mara ya pili, na tuna Roho Mtakatifu ndani yetu akituongozza na kutuelekeza, kwanini dhana hii yote ya kuwa “*mtumwa wa wote*” tunashindwa kuikubali?

- Nini tunaweza kufanya kurejesha muitikio wetu na vitendo vyetu katika “mtindo wa Yesu” wa unyenyekevu na utumishi?

10:46-52: *⁴⁶Wakafika Yeriko; hata alipokuwa akishika njia kutoka Yeriko, pamoja na wanafunzi wake, na mukutano mkubwa, mwana wa Timayo, Bartimayo, yule mwombaji kipofu, alikuwa ameketi kando ya njia.* ⁴⁷Naye aliposikia ya kwamba ni Yesu Mnazareti, alianza kupaza sauti yake, na kusema, *Mwana wa Daudi, Yesu, unirehemu.* ⁴⁸Na wengi wakamkemea ili anyamaze, lakini alizidi kupaza sauti, *Mwana wa Daudi, unirehemu.* ⁴⁹Yesu akasimama akasema, *Mwiteni. Wakamwita yule kipofu, wakamwambia, Jipe moyo; inuka, anakuita.* ⁵⁰Akatupa vazi lake, akaruka, akamwendea Yesu. ⁵¹Yesu akamjibu, akamwambia, *Wataka nikufanyie nini? Yule kipofu akamwambia, Mwalimu wangu, nataka nipate kuona.* ⁵²Yesu akamwambia, *Enenda zako, imani yako imekuponya. Mara akapata kuona; akamfuata njiani.*

mst. 46-52—Yesu amponya Bartimayo Kipofu

Wakati huu Yesu anakaribia Yerusalem kwa mara ya mwisho ambapo ataiakamilisha injili. Bartimayo anampazia sauti Yesu, akimuita “*Mwana wa Daudi*” (**mst. 47-48**). Mungu alikuwa amefanya agano na Daudi la kuinua uzao wa Daudi, kustawisha ufalme wake, kuwa baba kwake, naya atakuwa mwana kwa Mungu (**2 Sam 7:12-14a**). Zaidi ya hayo, **Isa 9:1-7** inaahidi kwamba wokovu utaletwa na mwana wa Daudi aliyeahidiwa, ambaye atastawisha ufalme wa milele (**Isa 9:7**). Kwahiyo, “*Mwana wa Daudi*” ni cheo cha kimasih (angalia pia **Isa 11:1, 10; Yer 23:5-6; Ezek 34:23-24; Marko 12:35**). Hata kabla Yesu hajazaliwa Malaika Gabriel alirejea **2 Sam 7:12-13** na **Isa 9:6-7**, na akasema kuwa Yesu angekamilisha Agano la Kidaudi, alipomwambia Mariamu kwamba Yesu “atakuwa mkuu na ataitwa mwana wa Mungu aliye juu, na Bwana atampa kiti cha enzi cha Daudi Baba yake; na atakamiliki nyumba ya Yakobo na ufalme wake hautakuwa na mwisho” (**Luka 1:31-33**). Mathayo alianza injili kwa kumwelezea Yesu kama: “*mwana wa Daudi, mwana wa Abrahamu*” (**Mat 1:1**). Wengine waliotambua nguvu ya Yesu na upkee wake walitumia maneno “*Mwana wa Mungu*” kumtambilisha (**Mat 9:27; 12:23; 15:22; 20:30-31; 21:9; Marko 10:47-48; Luka 18:38-39**). Yesu mwenyewe alitumia maneno hayo (**Marko 12:35-37**). “Kwa kumponya yule mtu kipofu kutoka Yeriko ambaye alimtaja kama Mwana wa Daudi, Yesu alitambua nafasi hiyo waziwazi” (Goppelt 1982: 87).

Marko anasema, matokeo ya Bartimayo kupaza sauti, “*wengi walimkemea, wakimwambia anyamaze*” (**mst. 48**). Maeleo ya Luka kuhusu hili anasema, “*Wale waliokuwa mbele walimkemea, wakimwambia anyamaze*” (**Luka 18:39**). Hili linaashiria kuwa ilikuwa wanafunzi ndio waliomkemea Bartimayo na kumwambia anyamaze. Bado walikuwa hawajajifunza. Kejeli ikiwa imefungamana na hilo. Wale walioweza kushuhudia kwa macho walikuwa vipofu kiroho, na wale walikuwa vipofu kimwili waliweza kuona kiroho. Hata hivyo, pamoja na kwamba Yesu alikuwa anakaribia kilele cha misheni yake, alisimama na kutumia muda kumponya aliyekuwa na haja. Kwa kejeli, Yesu katika **mst. 51** anamuuliza Bartimayo swali lile lile alilomuuliza Yakobo na Yoh katika **mst. 36**, “*Unataka nikutendee nini?*” Bartimayo alipokea jibu tofauti na lile alilopokea Yakobo na Yoh. Sasa, kwakuwa misheni yake ni kufikia kilele chake, Yesu hamuamuru Bartimayo kukaa kimya au kwenda nyumbani; badala yake, Bartimayo “*anamfuata njiani*” (**mst. 52**).

MASWALI UA KUJADILI

1. Kwanini unafikiri Yesu hakuamuru Bartimayo kunyamaza kama alivyofanya katika matukio mengine ya uponyaji?
2. Yasu amenukuliwa mara mbili aliuliza swal, “*Unataka nikutendee nini?*” (**mst. 36** kwa Yakobo na Yoh na **mst. 51** kwa Bartimayo). Ungeitikiae kama angekuuliza wewe swal hilo?

11:1-11: *¹Hata walipokaribia Yerusalem karibu na Bethfage na Bethania, kukabili mlima wa Mizeituni, aliwatuma wawili katika wanafunzi wake, ²akawaambia, Nendeni mpaka kile kijiji kinachowakabili; na katika kuingia ndani yake, mara mtaona mwana-punda amefungwa, asiyepandwa na mtu bado; mfungueni, kamleteni.* ³Na mtu akiwaambia, Mbona mnafanya hivi? Semeni, Bwana anamhitaji na mara atamrudisha tena hapa. ⁴Wakaenda zao, wakamwona mwana-punda amefungwa penye mlango, nje katika njia kuu, wakamfungua. ⁵Baadhi ya watu waliosimama huko wakawaambia, Mnafanya nini kumfungua mwana-punda? ⁶Wakawaambia kama Yesu alivyowaagiza, nao wakawaruhusu. ⁷Wakamletea Yesu yule mwana-punda, wakatandika mavazi yao juu yake; akaketi juu yake. ⁸Watu wengi wakatandaza mavazi yao njiani, na wengine matawi waliyoyakata mashambani.

⁹Nao watu waliotangulia na wale waliofufuata wakapaza sauti, Hosana; ndiye mbarikiwa ajaye kwa jina la Bwana;

¹⁰umebarikiwa na ufalme ujao, wa baba yetu Daudi. Hosana juu mbinguni.

¹¹Naye akaingia Yerusalem hata ndani ya hekalu; na alipokwisha kutazama yote pande zote, kwa kuwa ni

mst. 1-11—Kuingia Yerusalemu kwa msafara wa ushindi

Yesu kuingia Yerusalemu, kama matendo yake mengine, kulikusudiwa kufunue alikuwa nani. Katika uingiaji wake Yerusalemu kwa ushindi alikuwa akitimiza matarajio ya AK kwamba “YHWH anarudi Sayuni. Atafanya tena kile alichofanya katika Kutoka, anakuja kukaa katikati ya watu wake [Isa 4:2-6; 24:23; 25:9-10; 35:3-6, 10; 40:3-5, 9-11; 52:7-10; 50:15-17, 19-21; 60:1-3; 62:10-11; 63:1-9; 64:1; 66:12-19; Ezek 43:1-7; Hag 2:7-10; Zak 2:4-5, 10-12; 8:2-3; Mal 3:1-4].” (Wright 1996: 616) “Ndani ya muda na utamaduni wake, kuendesha punda katika mlima wa mizeituni, kupertia Kidroni, na kupanda hadi mlima wa hekalu kulikuwa na ujumbe mkubwa zaidi kuliko ambavyo maneno yengeweza kudhahirisha madai ya kifalme. Rejea kwa Zakaria (pamoja na vifungu vingine) ni wazi [Zak 9:9-10; angalia pia Mwa 49:8-12; Zab 72:8; Isa 63:2-6]. kuhusu kile kinachoitwa ‘kuingia kwa ushindi’ ni wazi kulikuwa kwa kimasih.” (Ibid.: 490-91) Yesu anaweza akawa alipanga mapema na mwenye punda ili kutimiza unabii wa **Zak 9:9**. Makutano walipaza sauti zao kwa maneno ya **Zab 118:25-26** (“*Hosana! Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana!*”) na “*Umebarikiwa usalme ujao wa baba yetu Daudi!*” (**mst. 9-10**) yalikuwa ni kumtambua Yesu kama Masihi; “hosanna” ni tafsiri ya neno la Kiebrania la **Zab 118:25** (“*tuokoe*”) likiwa na maana ya “*okoasasa*” (Swift 1970: 875). Wakati huo, wanafunzi, na huenda hata makutano, hawakuelewa maana kamili ya kile kilichokuwa kinaendelea na ujumbe gani ulikuwa unatolewa (angalia **Yoh 12:16**).⁵² Hata hivyo, Mafarisayo walitambua maana ya sauti zilizokuwa zikipazwa na makutano na, kwasababu hiyo walimwambie Yesu akemee watu wake (**Luka 19:39**). Lakini Yesu alijibu, “*Nawaambia, kama hawa wakinyamaza, mawe yatapaza sauti*” (**Luka 19:40**).

MASWALI YA KUJADILI

1. Wayahudi walitarajia mkombozi wa kisiasa; walielewa vibaya asili ya Masihi wao wenyewe na asili ya ufalme wake. Tunamtafsirije Yesu au kujaribu kumtumia (au Neno lake) kwa ajili ya hatma zetu? Jaribu kulenga maelezo maalumu (na uwazi).
2. Sauti zilizopazwa za “hosanna” (“*tuokoe sasa*”) zilibadilika na kuwa “msulubishe” kwa muda usiozidi juma moja. Mawazo na hisia zako kuhusu Mungu zimewahi kubadilika wakati changamoto zilipobadilika? Lini? kwa namna gani?
- Hilo linakuambia nini?
3. Katika **mst. 11** Yesu aliingia katika hekalu *kwa kificho* kukagua kile kilichokuwa haki yake. (Aliporudi kwa mara nyingine [**mst. 15**] alikuja kuhukumu kile alichokuwa amekiona wakati wa ukaguzi wake.) Ni lini anakuja kwa *kificho* kwetu?

11:12-26:¹² *Hata asubuhi yake walipotoka Bethania aliona njaa.*¹³ *Akaona kwa mbali mtini wenye majani, akaenda ili labda aone kitu juu yake; na alipoufikilia hakuona kitu ila majani; maana si wakati wa tini.*¹⁴ *Akajibu, akauambia, Tangu leo hata milele mtu asile matunda kwako. Wanafunzi wake wakasikia.*

¹⁵ *Wakafika Yerusalemu, naye akaingia ndani ya hekalu, akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuba na kununua ndani ya hekalu, akazipindua meza za wabadili fedha, na viti vyao wauzao njija;*¹⁶ *wala hakuacha mtu achukue chombo kati ya hekalu.*¹⁷ *Akafundisha, akasema, Je! Haikuandikwa, Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote? Bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi.*¹⁸ *Wakuu wa makuhani na waandishi wakapata habari wakatafuta jinsi ya kumwangamiza; maana walimwogopa, kwa sababu mkutano wote walishangaa kwa mafundisho yake.*¹⁹ *Na kulipokuwa jioni alitoka mjini.*

²⁰ *Na asubuhi walipokuwa wakipita, waliuona ule mtini umenyauka toka shinani.*²¹ *Petro akakumbuka habari yake, akamwambia, Rabi, tazama, mtini ulioulaani umenyauka.*²² *Yesu akajibu, akamwambia, Mwaminini Mungu.*²³ *Amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.*²⁴ *Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba*

⁵² Baada ya uasi wa Wamakabayo (167-160 KK) kurejesha hekalu, “maneno yaliyokuwa yakisemwa kwa krudiwa Hossana—‘tuokoe!’—yalikuwa yamechukua maana nyingine. Kabla ya kuimbwa katika kukumbuka ukombozi wao kutoka Misri na kama maombi ya kusamehewa na mvua kwa ajili ya mavuno ya mwaka uliofuata. Sasa yamekuwa pia maombi, kususihii kwa kina, kwa ukombozi wa kisiasa, kitu ambacho jamii ya Kiyahudi hawakukijua zaidi ya miaka 500.” (Vander Laan and Markham 1996: 117)

*mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*²⁵ *Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu.*²⁶ *Lakini kama ninyi hamsamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu.]*

mst. 12-26—Ishara za Umasihi wa Yesu: Yesu aulaani mtini na kutakasa hekalu

Kama ilivyokuwa katika matendo yake mengine, Yesu kuulaani mtini na kutakasa hekalu ilikuwa ni “mfano wa kuigiza” uliodhihirisha utambulisho wake; pia ilikuwa ni wa kinabii.

1. mst. 12-14, 20-26—Yesu aulaani mtini

Katika **Luka 13:6-9** Yesu alitoa mfano uliohusu mtini tasa. Mfano huo uliohusu kuja kwake mwenyewe kwa Israeli, akitafuta matunda, asipate kitu. Sasa, katika **Marko 11:12-14**, Yesu anaigiza mfano ule na kutoa ishara ya kukataliwa kwake na taifa la Israeli kwa kuulaani mtini (**Mat 21:18-22; Marko 11:12-14, 20-24**).⁵³ Mtini ulikuwa ni alama kwa taifa la Israeli (**Hos 9:10; Nah 3:12; Zak 3:10**). Katika kuulaani mtini, Yesu alikuwa akihukumu dini ya nje “kujionesha” ambayo haikuwa na ukweli na matunda halisi. Hata hivyo, alikuwa anatenda jambo ambalo ni zaidi ya hapo. **Yer 5:17, 8:13; Hos 2:12; Amos 4:9**, na **Mik 7:1-6** wote wanazungumza kuhusu hukumu juu ya mtini kama sehemu ya hukumu ya Mungu kwa Israeli. “Kifungu kinachokuja akilini kutokana na kisa hiki ni Mik 7:1-6, ambapo nabii anahuzunika juu ya uovu wa Yuda unaoelezewa kama kushindikana kupatikana ‘tini za kwanza zilizoiva ninazozitamani.’ Ukifuatia maneno ya wazi kwamba Yesu alikuwa na njaa katika mst. 18, kushindwa kwake kupata tini za mwanzo za kula kunazungumza kwa nguvu jinsi ambavyo maono ya kinabii yanavyotimia katika kushindwa kwa Yerusalem na hekalu lake kwa wakati ule.” (France 2007: 793) Yesu anaunganisha kulaani kwake mtini na tamko, “*yeyote asile kutoka kwako tena*” (**Marko 11:14**; angalia pia **Mat 21:19**). Kwa maneno hayo Yesu hakuwa anashambulia unafiki wa kidini tu (kwa kuwa wanafiki wanawenza wakatubu na kubadilika). Badala yake, alikuwa akidhihirisha kuwa *taifa* kama chombo cha kueneza ufalme wa Mungu limekataliwa kabisa na kutupwa nje. Vivyo hivyo, baada ya kuwashambulia Mafarisayo, Yesu alikuwa amesema, “*Kila mti asioupanda Baba yangu utang’olewa*” (**Mat 15:13**).

Katika **mst. 20-26** wanafunzi waliona kuwa mtini ambaa Yesu ameulaani umenyauka. Walipoanza kuuzungumzia, Yesu alishughulika na imani, na akasema, “*Amini, nawaambia, atakayeumbia mlima huu, ‘ng’oka ukatupwe baharini,’ wala asiwe na shaka katika moyo wake, bali aamini kuwa yale asemayo yatatokea, atatendewa*” (**mst. 23**). Kiini cha kukataliwa Israeli ni kukataliwa kwa Hekalu. Hilo linathibitishwa na maneno ya Yesu kuhusu kuutupa “*mlima huu*” baharini. “Mlima” huenda ulimaanisha mlima lilikokuwemo Hekalu, kwakuwa huo ulikuwa mlima muhimu kule Yerusalem na Hekalu lilikuwa lilitajwa kwa kubadilishanwa na mlima liliokuwa limejengwa. “Msemo huu siyo nyongeza ya maneno ya ziada kuhusu namna maombi na imani vinavyoweza kufanya mambo kama vile kuulaani mtini. Ni maneno maalumu ya hukumu: Mlima wa Hekalu, kwa kuuzungumzia kimfano, ubebwe na kutupwa baharini.” (Wright 1996: 422)

Yesu anaendelea kusema, katika **mst. 23b-26**, anaongeza kwa upana zaidi kuhusu uhusiano kati ya imani na maombi. Waalimu wa “Mafanikio” mara nyingi wanaonesha kuwa kama mtu akiomba utajiri wa kimwili Mungu analazimika kumpa. Wanasihamia katika kile alichosema Yesu katika **mst. 23**. Mst.ari huo hautetei au hauna uhusiano na mafundisho ya mafanikio. Kwa vyovyote, muktadha, unagusa hukumu ya Yesu kwa taifa la Israeli na hekalu. (**mst. 15-19**). Kifungu kinazungumzia kuhakikisha kuwa tunapata shabaha inayostahili na maadili sahihi na mtindo wa maisha. Hata matumizi yake mapana kuhusu imani na maombi yalihusiana na kukataliwa kwake na Israeli, kwa kuwa kumkataa Yesu, kulidhihirisha kuwa hawakuwa ama na imani kwa Mungu au maadili sahihi na mtindo wa maisha ambaa ungewawezesha kufanyika chombo cha Mungu cha kueneza ufalme wa Mungu. Vivyo, Yesu anakazia kwa wanafunzi (na kwetu) kwamba shabaha ya imani yetu inapaswa kuwa Mungu, na siyo utajiri wa mali za kimwili (**mst. 22**; angalia pia **Yak 4:3**). Hakika, maombi pekee yenye matokeo ni yale yanayofanywa na “*kulingana na mapenzi yake*” (**1 Yoh 5:14**; angali pia **1 Yoh 3:22**). Zaidi ya hayo, maombi yetu yanapaswa yaibukie kutoka katika maisha matakatifu ya msamaha, na siyo tamaa ya mali (**mst. 25-26**). Katika **mst. 25-26**, Yesu alikuwa anarudia hali aliyokuwa amesema kuhusiana na “Sala ya Bwana” (**Mat 6:14-15**).

⁵³ Wakati alipoukaribia mtini, **mst. 13** unasema, “*hatukukuta kitu isipokuwa majani, kwasababu hayakuwa majira ya tini.*” Hii haimaanishi kuwa Yesu kuulaani ule mtini halikuwa jambo la busara, kwasababu “mtini kule Palestina hutoa mazao ya awali yasiyokomaa, kama vijitunda vidogo vya kijani, Ambavyo hutokea kabla ya majani. Haya yanajulikana kama *taksh* na ni chakula cha kawaida cha *fellahin*, au wakulima. Kutokuwepo kwake kulikuwa ni dalili ya wazi ya ugumba wa mtini.” (Smith 1970: 875)

2. mst. 15-19—Yesu anatakasa hekalu

Katika mistari hii, Yesu “alitakasa hekalu” kwa kuwatoa wanunuzi na wauzaji na waliobadilisha pesa (angalia pia **Mat 21:12-13; Luka 19:45-46; Yoh 2:13-16**). Katika kufanya hivyo, Yesu alinukuu kutoka katika **Isa 56:7** (“*nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala*”), ambayo ni sehemu ya unabii (**Isa 56:3-8**) kwamba Mungu atawavuta wamataifa kwake katika “hekalu” lake (“*mlima mtakatifu*”). Pia alinukuu kutoka katika **Yer 7:11** (“*pango la wanyang’anyi*”), ambalo ni sehemu ya neno kutoka kwa Bwana (**Yer 7:1-11**) kwamba Mungu ameona jinsi ambavyo Israeli ametenda udhalimu, amewaonea wageni na wasiojiweza, amemwaga damu isiyo na hatia, amegeukia miungu mingine. Kosa lilopelekeea kitendo hiki kimsingi lilikuwa dhidi ya Wamataifa, kwasababu Masadukayo walikuwa wameweka soko la kondoo mahali ambapo Wamataifa walikusanyikia kuabudu [yaani, ua wa Wamataifa]. Kwa kuwa Wamataifa wasingeweza kuingia katika nyua zingine, kwa kufanya hivyo, makuhani walikuwa wamejitwalia sehemu yao ya maombi. Mungu aliagiza kuwa Wamataifa waaminifu wapatiwe sehemu ya sala, lakini Masadukayo waliamua kwamba siku za kidini wao walihitaji soko zaidi.” (Vander Laan na Markham 1996: 158)

Jambo kuu kwa Yesu katika kutakasa hekalu ni kwamba kama Mungu alivyolikataa hekalu la kwanza katika mwaka wa 586 KK kwasababu lilikuwa limeharibiwa na uovu, hivyo, hekalu la kimwili kule Yerusalem nafasi yake yafaa ichukuliwe na “Hekalu” kuu zaidi kwasababu limenajisika na kusudi la kuwepo kwake halitimii. “Tukiongezea kwa Isaya na Yeremia, tukio zima linatoa sauti ya kuonekana, kama ambavyo waandishi mbalimbali wa hivi karibuni wanavyojadili, ndani ya muktadha wa kumtumia tena Zakaria. Kuingia kwa Yesu mjini katika fahari ya kifalme, na mamlaka ya Yesu ya kimasihii juu ya Hekalu . . . inaansha Zakaria 9.9 na 6.12; onyo la janga linaloitikia 14.1-5. Zaidi ya hayo, muktadha wote unazungumzia matendo makuu ambapo YHWH atasimamisha ufalme wake mara moja na kwa milele yote (14.9), ambapo Wamataifa watakuja kuabudu (14.16-19). Katika muktadha huu, inawezekana kuwa tukio linaloandikwa na Marko 11.16, ambapo Yesu alikataa yejete kuleta vyombo hekaluni (wakati fulani ilikatazwa pia katika maandiko ya kirabi), ilikuwa ni sehemu ya kisa cha ‘kutakasa’ na, muhimu zaidi, alama nyingine, ikionesha, kama kwa utajiri kile kinachozungumzwa na Zakaria 14.20f., kwamba hatimaye ‘siku’ imewadnia.” (Wright 1996: 422)

Kuwafukuza wabadilisha pesa kunaweza kukawa kulismamisha kwa muda utoaji dhabihu kwa kukwamisha utaratibu ambao wanyama walinunuliwa na kutolewa dhabihu. Kama hivyo ndivyo, ingeweza kuashiria pia kusudi la kuwepo kwa hekalu kwa ajili ya kutoa dhabihu lilikuwa katika mpito. “Bila kuwa na pesa halali, waabuduo wasingeliweza kununua wanyama kwa ajili ya dhabihu. Bila wanyama, dhabihu isingefanyika. Bila dhabihu, Hekalu lilikuwa linapoteza *raison d’être* [sababu ya uwepo wake] kwa ujumla. Ukweli kwamba Yesu alileta alisimamisha kwa muda dhabihu unaendana vema na wazo la tendo la kimfano. Hakuwa anajaribu kuleta mageuzi; alikuwa anaashiria hukumu. . . . Hatua ya Yesu iliashiria imani yake kwamba, katika kurudi Sayuni, YHWH hata hivyo hataaka katika Hekalu, akihalalisha utawala uliopo na nafasi yake na ndani ya karne ya kwanza ya ulimwengu wa Kiyahudi wa kimfano. . . . Kuvurugwa kwa muda kulikoletwa na Yesu dhidi ya taratibu za kawaida za shughuli za kuliashiria uharibifu ambao ungeikalia taasisi yote kwa kizazi kile.” (Wright 1996: 423-24)

Kwa nyongeza, katika sheria ya AK, yejete aliyekuwa na kovu mwilini hakuruhusiwa kutumika katika Hekalu (**Law 21:16-24**). **Isa 56:3-8** alitabiri kuwa kutakuwepo na watu wapya wa Mungu “*katika nyumba yangu*,” wakiwemo Wamataifa na wale wenye makovu katika miili yao. “Isaya alitangaza kwamba katika siku za mwisho, Mungu atakapofunua haki yake, udhaifu wa kibaolojia au kovu katika mwili [mfano, Wamataifa, Matowashi] hazitakuwa sifa tena zinazoamua uanachama kwa watu wake. Wageni ‘*watajungamanisha na Bwana, kumtumikia, kulipenda jina la Bwana, na kuwa watumishi wake*’ (56:7). . . . Vigezo vya kuwa sehemu ya mrejesho wa mbeleni na ustawi wa ufalme havitoki tena duniani bali katika roho iliyopondekana, moyo uliovunjika [57:15] na muitikio wa haki kwa mapenzi ya Mungu kwa upande wa wale ambao watakaokuwa mionganoni mwa mabaki ambao Mungu anawahurumia (58:7-14)—wale ambao wanamfanya YHWH kuwa ‘*kimbilio*’ watamiliki nchi na kurithi *mlima mtakatifu*’ [57:13], ‘*wote wa mbali na wa karibu*’ [57:19]. Hii ina maanisha kuwa katika unabii wa kiisaya kigezo cha uanachama kwa watu wa Mungu wa kieskatolojia kimebadilika sana: wakati YHWH atakaporejesha dunia, Wayahudi wanaotubu na Wamataifa watatengeneza watu wa agano.” (Schnabel 2002: 41) Wakati alipofukuza wabadilisha pesa, Mathayo anaandika kwamba “*vipofu na waliopooza walimwendea hekaluni, na akawaponya*” (**Mat 21:14**). Yesu kunukuu kutoka **Isaya 56** kunaleta maana kwamba alikuwa anaumba watu wapya wa Mungu na kutimiza unabii wa Isaya. Watu hawa wapya wa Mungu wanafanywa kwa usawa na Wayahudi na Wamataifa, wanaume na wanawake, na watu kutoka kila kituo cha maisha; wote sasa ni “makuhani” kwa namna mpya, ya kweli, nyumba ya Mungu (angalia **Mdo 8:26-38; Gal 3:28; Ef 2:11-22; Kol 3:10-11; 1 Pet 2:5, 9; Ufu 1:6; 5:9-10; 7:9**).

MASWALI YA KUJADILI

1. Kwanini Yesu alilaani mtini? Alikuwa ameukasirikia tu ule mtini kwasababu alikuwa na nja na haukuwa na tini, au alikuwa anawasilisha ujumbe fulani?
 - Kuulaani mtini kulihusianaje na kutakaswa kwa kanisa?
2. Kulaaniwa kwa mtini na kutakaswa kwa hekalu kunakuambia nini kuhusu kile kilichomkasirisha Yesu?
 - Hili linahusianaje na desturi zetu za kidini au matendo mengine?
3. Katika mwonekano wa kwanza, mazungumzo yanaanza katika **mst. 21** kwa namna fulani yanakuwa kama hayapendezi: Maneno ya Petro siyo swalililolo wazi, lakini Yesu “analijibu”; hadi hapo, jibu la Yesu halione kani kuhusiana moja kwa moja na kile Petro alisema. Unafikiri ni kwanini Yesu alijibu swalililolo kwa namna hiyo?
4. Zipi ni hali za msingi kwa maombi yenyeye matokeo alizozifundisha Yesu katika **22-26**?
 - Ipi kati ya hizo inakugusa zaidi?
 - Ni kwa namna gani kile alichosema Yesu kuhusu maombi kinahusiana na namna unavyoomba?

5. Ina maana gani kumsamehe mtu? kama tumesamehewa uasi wetu, dhambi, na deni tulilokuwa tunadaiwa na Mungu kwamba tusingeliweza kamwe kulipa jambo ambalo lingapelekeea maisha yetu kuishia motoni, lakini badala yake tumepewa kwa neema maisha mapya hapa na uzima wa milele ambaa itakuwa ni mahali pa furaha kamili, kwanini inakuwa vigumu kuwasamehe wengine yale ambayo wanaweza wakawa wametutenda, wametukwaza, wametuumiza, au kutudhuru kwa namna fulani?

11:27-33: ²⁷ *Wakafika Yerusalemu tena; hata alipokuwa akitembea hekaluni, walimwendea wakuu wa makuhani, na waandishi, na wazee,* ²⁸ *wakamwambia, Ni kwa mamlaka gani unatenda mambo haya? Naye ni nani aliyekupa mamlaka hii uyatende haya?* ²⁹ *Yesu akawaambia, Nitawauliza neno moja, nanyi mnijibu, kisha nitawaambia ni kwa mamlaka gani nayatende haya.* ³⁰ *Ubatizo wa Yoh ulitoka mbinguni, au kwa wanadamu? Nijibuni.* ³¹ *Wakasemezana wao kwa wao, wakisema, Kama tukisema, Ulitoka mbinguni, atasema, Mbona, basi, hamkumwamini?* ³² *Ila tukisema, Ulitoka kwa wanadamu, -- waliogopa watu; maana watu wote walimwona Yoh kuwa nabii halisi.* ³³ *Wakamjibu Yesu, wakasema, Hatujui. Yesu akawaambia, Wala mimi siwaambii ninyi ni kwa mamlaka gani nayatende haya.*

mst. 27-33—Asili ya mamlaka ya Yesu yatiliwa shaka

Swali la Yesu kwa viongozi wa dini, “*Ubatizo wa Yoh ulitoka mbinguni au kwa wanadamu?*” (**mst. 30**) unawaweka viongozi wa dini njia panda na pia kufunua unafiki wao. Kujibu “*ulitoka mbinguni*” kungehujumu upinzani wao kwa Yesu, kwasababu Yoh Mbatizaji alishuhudia kwamba Yesu alikuwa mkuu kuliko yeeye (**Marko 1:7-8**) na alikuwa mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu (**Yoh 1:29-34**). Hivyo, kama mamlaka ya Yoh yalitoka mbinguni, basi ni zaidi mamlaka ya Yesu yalitoka mbinguni, jambo ambalo lingemaanisha tu kwamba alikuwa masihi. Kama R. Alan Cole anavyooleza, “*Swali la Yesu kwao halikuwa mtego; ilikuwa ni fursa nyingine ya kutambua na kukiri upofu wao, na kuomba wapewe kuona. Dhambi yao ilikuwa haisameheki, kuendelea kupinga kwa makusudi na upofu ni dhambi dhidi ya Roo Mtakatifu (3:29).*” (Cole 1989: 258)

MASWALI YA KUJADILI

1. Kwanini jibu “*kutoka mbinguni*” kwa swalililolo kwa Yesu katika **mst. 30** limekuwa la hatari kubwa kwa upinzani wa viongozi wa Kiyahudi?
2. Ni kwa kiwango gani, au ni mambo gani, yanayokuzuia usiseme kweli au kutenda kile ambacho unajua unapaswa kutenda kwasababu ya kuogopa watu (ikiwa ni pamoa na hofu ya kuogopa watu watakfikiriaje)?

12:1-12: ¹ *Akaanza kusema nao kwa mifano; Mtu mmoja alipanda shamba la mizabibu, akazungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo, akajenga mnara, akapangisha wakulima, akasafiri.* ² *Hata kwa wakati wake akatuma mtumwa kwa wale wakulima, ili apokee kwa wakulima katika matunda ya mizabibu.* ³ *Wakamtwa, wakampiga, wakamtoa nje, hana kitu.* ⁴ *Akatuma tena kwo mtumwa mwengine, na huyo wakamtia jeraha za kichwa, wakamfanya jeuri.* ⁵ *Akamtuma mwengine, huyo wakamwua; na wengine wengi, hawa wakiwapiga na hawa wakiwaua.* ⁶ *Basi alikuwa na mmoja bado, mwana mpandwa wake; huyu naye akamtuma kwao mwisho, akisema, Watamst.ahi mwanangu.*

⁷ *Lakini wale wakulima wakasemezana, Huyu ni mrithi; haya, na tumwue, na urithi utakuwa wetu.*

⁸ *Wakamkamata, wakamwua, wakamtupa nje ya shamba la mizabibu.* ⁹ *basi atafanyaje yule bwana wa shamba la mizabibu? Atakuja na kuwaangamiza wale wakulima, na lile shamba la mizabibu atawapa wengine.* ¹⁰ *Hata andiko hili hamjalisoma, Jiwe walilolikataa waashi, Hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni.* ¹¹ *Neno hili limetoka kwa Bwana, Nalo ni ajabu machoni petu?*

¹² *Nao wakatafuta kumkamata, wakaogopa mkutano; maana walitambua ya kwamba ule mifano amewanenea wao. Wakamwacha wakaenda zao.*

mst. 1-12—Mfano wa mkulima wa zabibu

Katika kuingia kwake Yerusalem kwa mara ya mwisho, Yesu alitenda miujiza miwili “ya kimaigizo” ikimaanisha kukataliwa kwake na hukumu ya Israeli—kuulaani mtini na kulitakasa hekalu. Sasa, anatoa mfano kwa jambo lile lile, linalorejea historia ya mahusiano ya Mungu na kumalizia na hukumu ya Mungu. Kutokea kwa mfano huu kunarejea **Isa 5:1-7**, ambapo uharibifu wa unatabiriwa kutokana na dhulma yao, kutokutenda haki, na kushindwa kuzaa matunda mema. Katika hilo, Yesu anachukua kile alichosema Isaya kuhusu Israeli, na kukileta katika wakati uliokuwepo, na anasema mini kitafanyika dhidi ya hali hiyo. Katika mfano wa mkulima wa zabibu, mwenye shamba la mizabibu ni Mungu, shamba la mizazbibu ni Israeli, waliolikodisha ni viongozi wake, watumishi ni manabii, na mwana ni Yesu Kristo. Katika **Mat 23:29-35** na **Luka 11:47-51** Yesu pia anatajaa vitendo vibaya vya Israeli kwa manabii. Katika **mst. 8**, Yesu anasema, “*Wakamkamata, wakamwua, wakamtupa nje ya shamba la mizabibu.*” Hilo lilikuwa ni kivuli cha kusulubiwa kwake nje ya lango la mji (**Ebr 13:12**). **Mistari 9-11** ni kivuli cha kuharibiwa kwa Israeli na kuumbwa kwa kitu kipyta, Israeli wa kweli inayofanywa kwa haki sawa na—Wayahudi na Wamataifa—ambao wako “katika Kristo” (angalia **Rum 11:11-26; Gal 3:28; Ef 2:11-22; Kol 3:10-11; Ufu 5:9-10; 7:9**). Katika **mst. 10-11** Yesu ananukuu kutoka katika **Zab 118:22-23**, Zaburi ambayo watu walinukuu walipopaza sauti zao wakisema “*Hosana! Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana!*” wakatu wa Kristo kuingi kwa ushindi Yerusalem siku chache tu kabla. Mfano huu kusema kweli unatoa jibu la swali lililoul;izwa na makuhani wakuu, waandishi, na wazee katika **11:28**, “*Ni kwa mamlaka gani unatenda mambo haya, au nani amekupa mamlaka hii kutenda haya?*” Katika mfano huu Yesu anasema, “ninatenda mambo haya kwa mamlaka ya Mungu, kwa kuwa mimi ni mwanawe kama ilivyotabiriwa na Zaburi.”

MASWALI YA KUJADILI

1. Ni wahusika gani wanahusishwa na kila mfano uliotolewa (yaani, mmiliki wa shamba la mizabibu, shamba la mizabibu, waliolikodisha shamba la mizazbibu, watumishi, na mwana)? Ni kwa namna gani mfano huu ni wa kihistoria na kinabii?
2. Ni kwa namna gani **Zab 118:22-23**, aliyonkuu Yesu katika **mst. 10-11**, inahusiana na mfano huu?
3. Mfano huu unajibuje swali la waandishi katika **Marko 11:28**?

12:13-17: ¹³ *Wakatuma kwake baadhi ya Mafarisayo na Maherodi, ili wamnase kwa maneno.* ¹⁴ *Hata walipofika walimwambia, Mwalimu, twajua ya kuwa wewe u mtu wa kweli, wala hujali cheo cha mtu; kwa maana hutazami sura za watu; lakini katika kweli waifundisha njia ya Mungu. Je! Ni halali kumpa Kaisari kodi au siyo?* ¹⁵ *Tumpe, tusimpe? Naye, akijua unafiki wao, akawaambia, Mbona mmenjaribu? Nileteeni dinari niione.* ¹⁶ *Wakaileta. Akawaambia, Ni ya nani sanamu hii na anwani hii?* *Wakamwambia, Ni ya Kaisari.* ¹⁷ *Yesu akajibu, akawaambia, Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na yaliyo ya Mungu mpeni Mungu. Wakamst.ajabia sana.*

mst. 13-17—“Yaliyo ya Mungu mpeni Mungu”

Tangu mwaka wa 6 BK Warumi walikuwa wamewataka Wayahudi kulipa kodi ya kichwa; Wazelote walikataa kulipa, Mafarisayo walilipa kwa uchungu, Maherode walipenda kulipa (Wessel 1984: 734). Swali hili lilionekana kama la kumpinga Yesu katika kufanya maamuzi. Jibu rahisi la

“ndiyo” au “hapana” lingepelekeka kumuweka Yesu upande ama wa Maherode au Wazelote. Jibu la “ndiyo” lingemaanisha kuwa watu wengi wangemuondoa katika umasihi, kwasababu walifikiri masihi angeliwaokoa kutoka katika mamlaka ya Rumi. Jibu la “hapana” lingemuweka katika hatia ya uhaini dhidi ya Rumi. Unafiki uliokuwepo nyuma ya swali unashangaza. Maneno yao kwamba “*tunajua kuwa wewe u mtu wa kweli, wala hujali mawazo ya mtu*” yanaonesha unafiki wao, kwa kuwa wali “ogopa watu” (**12:12**). Zaidi ya hayo, Mafarisayo na Maherode walikuwa maadui lakini pamoja na hayo wakapatana.

Ukweli kwamba Yesu alilazimika kuwaomba dinari kunaonesha umasikini wake. Lakini pia iliwalazimisha kufunua unafiki wao kwasababu walikuwa na sarafu ya Kaisari na akaitumia. Hapo sasa, walikuwa wanajibu swali lao wenyewe. Jibu la Yesu lenye sehemu mbili, “*Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo yake*,” ni jibu lenye nguvu lililowafanya “wamshangae.” Jibu lake lilionesha kuwa alikuwa hachezi nafasi ya Masihi wa “kisiasa” aliyetarajiwa na wengi. Sehemu ya kwanza ya jibu inatambua kwamba serikali ina haki fulani kwetu kama rai, kwasababu inatupatia faida fulani. Katika hili haipingani na madai ya Mungu kwetu (angalia **Rum 13:1-7; 1 Tim 2:1-6; Tito 3:1-2; 1 Pet 2:13-17**). Hata hivyo, sehemu ya pili inaonesha kuwa wajibu wetu kwa serikali siyo wajibu kwa kila jambo. Mungu ndiye mamlaka yetu ya mwisho na yuko juu ya serikali. Ingawa dinari ilikuwa na chapa ya sura ya Kaisari, sisi—kila mwanadamu—tuna chapa yenye sura na mfano wa Mungu (**Mwa 1:26-27; 5:1; 9:6; Rum 8:29; 2 Kor 3:18; Ef 4:22-24; Kol 3:9-10; Yak 3:9-10**). Matokeo yake, amri ya kwanza na ilio kuu ni “*mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili yako yote na kwa nguvu zako zote*” (**Marko 12:30**; angalia pia **Mat 22:37; Luka 10:27**). Kipaumbele kisicho na mpinzani kwa Mungu katika maisha yetu kina maanisha kwamba kutakuwepo na tofauti katika namna tunavyotumia utii wetu kwa serikali dhidi ya utii kamili kwa Mungu. Wakati serikali inapochukua nafasi ya Mungu na kufanya utii wetu kwake kuwa ni jambo la kuvunja sheria, wajibu wetu ni lutokutii serikali, hata kama kufanya hivyo kutapelekeka kufungwa au hata kifo. Mitume walijifunza somo hili mapema (angalia **Mdo 5:17-42**). Kama Petro alivyosema, “*Yatupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu*” (**Mdo 5:29**).

MASWALI YA KUJADILI

1. Kwanini swali la “tunapaswa kulipa kodi kwa Kaizari au la?” liwe la hatari kiasi hicho?
2. Ni chapa ya sura ya nani *tuliyowekwa*? Hili lina maanisha nini kuhusu namna tunavyopaswa kuenendesha maisha yetu?
3. Siasa na uchumi wetu (na, hasa, maisha yetu kwa ujumla) yanapaswa kuwa matokeo ya theolojia yetu. Umewahi kukutana na hali ambapo theolojia yako inapingana na siasa yako au imani yako, au jamii ilikuomba au kukutaka jambo ambalo unaamini ni kinyume na theolojia yako?
 - Ulishughuhulikiae hali hiyo?
 - Ulipaswa kushughulikiae hali hiyo?

12:18-27:¹⁸ *Kisha Masadukayo, watu wasemao ya kwamba hakuna kiyama, wakamwenda, wakamwuliza na kusema,*¹⁹ *Mwalimu, Musa alituandikia ya kwamba ndugu ya mtu akifa, akamwacha mkewe wala hana mtoto, ndugu yake amtwa yule mkewe akampatie ndugu yake mzao.*²⁰ *Basi kulikuwa na ndugu saba, wa kwanza akatwaa mke, akafa, asiache mzao.*²¹ *Wa pili naye akamtwaakafa, wala yeeye hakuacha mzao. Na wa tatu kadhalika;*²² *hata na wote saba, wasiache mzao. Mwisho wa wote yule mwanamke akafa naye.*²³ *Basi, katika kiyama atakuwa mke wa yupi katika hao? Maana wote saba walikuwa naye.*²⁴ *Yesu akajibu, akawaambia, Je! Hampotei kwa sababu hii, kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu?*²⁵ *Kwa maana watakafufuka katika wafu, hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika walioko mbinguni.*²⁶ *Na kwa habari ya wafu ya kwamba wafufuliwa, hamjasoma katika kitabu cha Musa, Sura ya Kijiti, jinsi Mungu alivyomwambia, akisema, Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo?*²⁷ *Yeye si Mungu wa wafu, bali wa walio hai. Hivyo mwapotea sana.*

mst. 18-27—Maisha katika ufufuo

Swali la Masadukayo ni swali la dhihaka. Wanaanza na kunukuu **Kumb 25:5.**⁵⁴ Swali lao ni dhihaka

⁵⁴ Hii ilikuwa ni “ndo ya kumrithi mjane wa ndugu” (levirate marriage, *levir* kwa kilatini, “shemeji wa kiume”) na

kwasababu kimsingi linasema, “kwakuwa ndugu hawa wote saba hawawezi kuwa na mwanamke huyu wakati wa ufufuo, kwahiyu hakuna ufufuo.”

Jibu la Yesu linasema kwamba kuna mambo mawili ambayo ni ufunguo wa kutuwezesha kuelewa asili ya kweli ya halisia: (1) kuelewa maandiko, na (2) kuelewa nguvu ya Mungu (**mst. 24**). **Mst.ari wa 25** unatuonesha kuwa ndoa (hasa, mahusiano ya kujamiihana) ni muhimu tu hapa duniani na sasa, ambapo mauti inatawala, kwa kuwa kuzaliana ni muhimu kwa ajili ya kuendeleza uzao wa kibinadamu. Siyo lazima tena kule mbinguni au katika nchi mpya kwa kuwa wale wote ambao “*wanaofikiriwa kustahili kufikia umri huo na kufikia ufufuo . . . hawafi tena*”; hivyo, ndoa siyo lazima tena (**Luka 20:35-36**). Zaidi ya hayo, Masadukayo hawakujua ukweli huo kwamba ufufuo siyo kuigiza na kurudia hali zilizopo lakini na mabadiliko ya kuwa aina mpya ya maisha na hali, kama Paulo anavyoweka wazi katika **1 Kor 15:35-50**.

Katika **mst. 26** Yesu ananukuu **Kut 3:6** na anakazia wakati uliopo (“*Mimi ndiye Mungu wa. . .*” siyo “*Mimi nilikuwa Mungu wa. . .*”). Yesu anahoji kwamba hilo linamaanisha kuwa Abrahamu, Isaka, na Yacobo sasa wanaishi. Hili linawekwa wazi zaidi katika maelezo ya Luka. Hili pia ni kulingana na kile Yesu alisema katika **Luka 20:37-38** (angalia pia **Mat 22:31-32; Marko 12:26-27**), “*Lakini kwamba wafu wafufuliwa, hata Musa alioneshwa, katika kile kifungu kuhusu kichaka, ambapo anamuita Bwana Mungu wa Abrahamu na Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo. Sasa si Mungu wa wafu, bali walio hai, kwa kuwa wote katika yeye wanaishi.*” Neno lililotumiwa na Yesu “wafufuliwa” katika **mst. 37** ni *egeirō*, moja ya maneno ya msingi yaliyotumika katika AJ kumaanisha “ufufuo.” Jambo muhimu hapa ni kwamba Yesu alikuwa anatumia lugha ya wazi ya “ufufuo” kumuelezea Abrahamu, Isaka, na Yakobo *katika hali ile ya katikati*, siyo hali ya miili yao ya mwisho baada ya kufufuliwa. Kutumia lugha ya “ufufuo” kuongelea maisha yetu ya sasa katika Kristo (hapa dunini na mbinguni kabla ya uzinduzi wa mbingu mpya na nchi mpya wakati wa kuja Kristo) vile vile ikirejea ufufuo wa mwili utakaotokea kuhusiana na kurudi kwa Yesu mara ya pili unakuzwa katika AJ. kwa mfano, **Ef 2:5-6** inatumia maneno “*alituhuisha*,” “*alitufufua*” na “*alituketisha pamoja naye katika roho*” kurejea ufufuo wa kiroho pamoja na Kristo katika kizazi hiki, wakati ulioko (angalia pia **Yoh 5:24-29; Rum 6:4-5; Kol 2:12-13; Ufu. 20:4-6**).⁵⁵

MASWALI YA KUJADILI

1. Mfano wa kinafiki wa Masadukayo na swali lao vinakuwaje hija ya ufufuo?
2. Ni kwa namna gani **Kut 3:6**, ambayo Yesu alinukuu katika **mst.. 26**, inakuwa hoja ya uzima wa milele na ufufuo?
3. Katika jibu lake kwa Masadukayo, Yesu anaorodhesha mambo mawili ambayo ni muhimu kwa uelewa wetu kuhusu asili ya kweli ya mambo. Ni mambo gani hayo?
 - Kati ya hayo mawili, lipi unalijua zaidi au una uzoefu nalo, na unafikiri ni kwa namna gani inaweza kukua katika lile ambalo hulijui sana au huna uzoefu nalo?

12:28-34: ²⁸ *Na mmojawapo wa waandishi akafika, akawasikia wakisemezana naye, akatambua ya kuwa amewajibu vema, akamwuliza, Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza?* ²⁹ Yesu akamjibu, Ya kwanza ndiyo hii, Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; ³⁰ nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. ³¹ Na ya pili ndiyo hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi. ³² Yule mwandishi akamwambia, Hakika, Mwalimu, umesema vema ya kwamba Mungu ni mmoja, wala hakuna mwingine ila yeye; ³³ na kumpenda yeye kwa moyo wote, na kwa usahamu wote, na kwa nguvu zote, na kumpenda jirani kama nafsi yako, kwafaa kuliko sadaka nzima za kuteketezwa na dhahibu zote pia. ³⁴ *Naye Yesu, alipoona kwamba amejibu kwa busara, alimwambia, Wewe hu mbali na ufalme wa Mungu. Wala hakuthubutu mtu kumsaili neno tena tokea hapo.*

mst. 28-34—Amri iliyo kuu

Katika kujibu swali la waandishi, Yesu anaanza kwa kunukuu **Kumb 6:4-5**. Alianzia hapa kwasababu mistari hii ni ya msingi. Inatukumbusha Mungu ni nani na kwamba yeye ndiye aliye juu ya vyote. Inatukumbusha pia kuhusu umuhimu wa kupatana na Mungu kibinaksi, kumwangalia yeye, na kusikia na kuitikia neno lake kwa namna inayodhihirisha upendo na kumtumainia yeye. Upendo wetu kwa Mungu

iliikuwa imekusudiwa “kumlinda mjane na kumhakikishia uendelevu wa ukoo” (Wessel 1984: 735).

⁵⁵ Swala hili limejadiliwa kwa kina katika Menn 2017: 203-10.

unapaswa utushike utu wetu kabisa. Kwa amri ya pili, Yesu ananukuu **Law 19:18**. “*Mpende jirani yako kama nafsi yako*” ni muunganiko unaotiririka kutoka “*mpende Bwana Mungu wako kwa roho yako yote na kumpenda Bwana Mungu wako moyo wako wote na kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote.*” Kusema kweli, mtume Yoh anaonesha kuwa kutimiza amri ya pili (kumpenda jirani yako) ni ushahidi na mtihani wa kuonesha kama kweli unatimiza amri ya kwanza (kumpenda Mungu): “*Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezo kumpenda Mungu ambaye hakumwona.*” (**1 Yoh 4:20**) Sababu kwanini amri ya pili ni ushahidi na jaribio la amri ya kwanza ni kwamba watu wote wamefanywa kwa sura ya Mungu, kwahiyu namna tunavyoichukulia sura ya Mungu hudhihirisha tunamfikiria Mungu mwenyewe. Zaidi ya hayo, neno linalosimama kwa “upendo” kwa pande zote mbili ni *agapaō*, ambalo siyo tu la “kimhemko” bali ni kanuni hai inayoshika utu wote wa mtu” (Swift 1970: 877).

Kwasababu wengi wetu tunafahamu amri hizi zote mbili, huwa haturejei na kuona ni kiasi gani zina mashiko. Tunasema tunampenda Mungu, lakini je tunampenda kweli kwa roho yetu yote, kwa moyo wote, kwa akili zote, na kwa nguvu zote wakati wote? Na “kumpenda hasa jirani yetu kama tunavyojipenda wenyewe” ina maana kwamba ingetupasa kutumia muda kama ule ule, juhudzi zile zile na pesa katika kustawi kwa wengine kama ambavyo tunatumia katika kutafuta uastawi wetu binafsi. Kama Yesu alivyoweka wazi katika kisa cha msamaria mwema (**Luka 10:29-37**) na **Mat 5:43-48** (“*mpende adui yako*”) amri ya “kumpenda jirani yako kama nafsi yako” inamgusa kila mtu, wakiwemo wale wasiopendeka, wale tusiovutwa nao, maadui, wale wasiotupenda, wale wenye rangi tofauti nasi, madaraja tofauri, makabila tofauti, na mengine tofauti na sisi. Mtu anaweza kufikiria ulimwengu ungekuwaje kama Wakristo wangejari kufanya kazi amri hizi kwa kumaanisha na kwa kudumu.

MASWALI YA KUJADILI

1. Tafakari kifungu hiki cha maandiko, kwa kuwa ni moja kati ya vile vinavyogusakitovu cha yote yanayomhusu Yesu na ufalme wa Mungu. Tunajifunza somo gani kutokana na jibu la Yesu kwa Masadukayo?
2. Tamko la Yesu la kumpenda jirani yao “kama nafsi yako” linaathirije au kufafanua amri ya “mpende jirani yako?”
3. Ni kitu gani hiki kinachoitwa “upendo” (Kigiriki, *agapaō*, muundo wake wa nomino, *agapē*)? Kujibu hili ni lazima uende katika biblia yote kuona pale ambapo neno hili lilitumika, na uone namna linavyoelezeka, au lilivytumika mahali pengine.

12:35-37: ³⁵ *Hata Yesu alipokuwa akifundisha katika hekalu, alijibu, akasema, Husemajie waandishi ya kwamba Kristo ni Mwana wa Daudi?* ³⁶ *Daudi mwenyewe alisema, kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Bwana alimwambia Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwawekapo adui zako Kuwa chini ya miguu yako.* ³⁷ *Daudi mwenyewe asema ni Bwana; basi amekuwaje mwanaowe? Na mkutano mkubwa walikuwa wakimsikiliza kwa furaha.*

mst. 35-37—Kristo ndiye Bwana

Kufuatia kuingia kwa Yesu Yerusalem, viongozi wa kidini wamekuwa wakimuuliza maswali, mara nyingi wakijaribu kumtia hatiani, ukianzia na “*Ni kwa mamlaka gani unatenda mambo haya?*” (**11:28**). Pamoja na jibu lake kwa waandishi kuhusu ipi ni amri kuu, hata hivyo, “*hakuna aliyethubutu kumuuliza maswali zaidi*” (**mst. 34**). Kwahiyu, sasa Yesu anashika nafasi ya kimamlaka hekaluni na kuuliza maswali ambayo yanalenga kwenye kitovu cha yeye ni nani na asili ya mamlaka yake. Maelezo ya Marko yanaweka wazi kwamba maswali ya Yesu yalikuwa yameelekezwa kwa viongozi wa dini na waalimu wa sheria. **Mat 22:41** na **Luka 20:39-41** wanaweka wazi kwamba swali lake lilielekezwa kwa Mafarisayo na waandishi.

Hapo nyuma Yesu alikuwa ametambulishwa na Bartimayo (**10:47-48**) kama mwana wa Daudi wa kimasih. Sasa Yesu anachukua cheo hicho na kufunua kwamba Mwana wa Daudi ni zaidi ya mtu tu, bali ndiye Bwana mwenyewe. Anafanya hivyo kwa kunukuu **Zab 110:1**. Maelezo ya Mathayo kuhusu tukio hili yanatoe maelezo ya kina zaidi kuliko ya Marko. Mathayo anapoeleza, Yesu aliwaliliza Mafarisayo walifikiri nini kuhusu Kristo: “*Ni mwana wa nani?*” (**Mat 22:42**); waliitikia kwamba ni “*mwana wa Daudi*” (**Mat 22:42**). Kisha Kristo akanukuu **Zab 110:1** inayosema, “*Bwana alisema kwa Bwana wangu.*” Kisha aauliza, “*Kama Daudi [aliyeandika Zaburi] anamuita ‘Bwana,’ anakuwaje mwana?*” (**Mat 22:45**; angalia **Marko 12:37**). Yesu alikuwa akijifunua mwenyewe kama Masihi, “*Mtoto mkuu*” wa Daudi na

kwamba ni wa kiungu (angalia Goppelt 1982: 83 [“Neno ‘Bwana’ (*kurios*) linamfanya kuwa sawa na Mungu”]). Waandishi wa Agano Jipywa walielewa Yesu alikuwa anasema nini. **Zab 110:1** ilikuwa ndicho kifungu kinachotawala katika AJ (kuna nukuu 21 au yanayogusa kifungu hiki katika maadiko mengi ya AJ). Umuhimu wa hili kwa waandishi wa kwanza wa Kikristo, ni wa msingi, hasa ukizingatia muktadha wa wao wa kiyahudi wa kuamini Mungu mmoja. “[Zab 110:1] ingewezekana, kwa mfano, kusomeka kwa kumaanisha tu kwamba Masihi amepewa nafasi ya heshima kama jambo muhimu pembeni ya enzi ya kiungu, pale anapokaa akiwa hana cha kufanya anangojea kuzinduliwa kwa ufalme wake duniani. Hivi ndivyo marabi baadae walivyosoma. Ni wazi kabisa, hata hivyo, kwamba Wakristo wa kwanza walisoma tofauti andiko hilo: wakimweka Yesu katika nafasi ya kiti cha enzi chenyewe, akitawala kama Mungu mwenyewe juu ya kila kitu.” (Bauckham 1998: 29) Chunguza kuwepo kwa utatu katika **mst. 36**: Daudi, aliyeandika **Zab 110**, alikuwa katika “Roho Mtakatifu” na akasema, “Bwana” (yaani, Baba) alisema kwa “Bwana wangu” (yaani, Mwana).⁵⁶

Mwisho, Yesu kutumia **Zab 110:1** ni kama pazia au unabii usio wa moja kwa moja wa ufuluo wake unaokuja, kupaa, na kuinuliwa, kama sehemu ya tangazo lake kwamba yeye ndiye Mwana wa Mungu. Sababu inapatikana katika maelezo ya Paulo kuhusu ufuluo na kuja mara ya pili kwa Kristo (yaani, *parousia*) katika **1 Kor 15:20-57**. Katika kifungu hicho, **mst. 26** unatuambia kwamba “*adui wa mwisho atakayeangamizwa ni mauti.*” Mauti yenyewe itakomeshwa wakati wa *parousia* (**mst. 50-57**). Matokeo yake, Kristo lazima awe ameanza kutawala kabla, siyo baada, ya *parousia*.⁵⁶ Kwa hakika, “utawala” wa Kristo uliana na ufuluo wake na kupaa kwake; hivi sasa yuko mkono wa kuume wa Mungu akitawala katika nguvu (angalia **Marko 16:19; Luka 22:69; Mdo 2:22-36; 7:55-56; Rum 1:4; 8:34; Ef 1:20-22; Flp 2:9-10; 3:20-21; Kol 1:13; 3:1; Ebr 1:3; 8:1; 10:12; 12:2; 1 Pet 3:22; Ufu 1:5**; angalia pia Fee 1987: 747). Hili linaoneshwa na Paulo akinukuu au kuhusisha na **Zab 110:1** (“*BWANA alisema na Bwana, ‘Keti mkono wangu wa kuume hadi nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako*””) katika **mst. 25** na **Zab 8:6** (“*Umemfanya kuwa mtawala juu ya kazi za mikono yako na kuweka vitu vyote chini ya miguu yake*”) katika **mst. 27**.

Keener anazungumzia umuhimu wa **Zab 110:1** kwa muktadha huu: “mpango wa kieskatolojia wa Paulo hapa unategemeana na tafsiriyake ya Zab 110:1, ambayo inakuwa wazi katika 15:25. Kwasababu “Bwana” atatawala katika mkono wa kuume wa Mungu hadi maadui zake watakaptiishwa chini ya miguu yake (Zab 110:1), Lazima Kristo atawale akiwa mkono wa kuume wa Mungu kwa wakati uliopo hadi hapo maadui zake watakaponyenyekeshwa chini yake (15:25).” (Keener 2005: 127; angalia pia Bauckham 1998: 29-30; Hill 1988: 312-14; Smith 1999a: n.p.) Kristo ameinuliwa na anatawala kutoka mbinguni sasa katika awamu iliyopo ya ufalme wake. Hilo linaeleweka ukitumia vifungu vingine vinavyozungumzia utawala wa Yesu kwa wakati uliopo: “Katika Kol. ii. 15 [Paulo] anazungumzia kuwashinda *archai* [“watawala”] na *exousiae* [“mamlaka”] [yote yanatajwa katika **1 Kor 15:24**] kama mambo ambayo yamekwisha kamilishwa ktika msalaba wa Kristo. Katika Rum. viii. 38, 39 anachukulia kwamba hata sasa anatawala na kudhibiti mauti na uzima na wakuu wa anga na mamlaka ili kuwatenga Wakristo na upendo wa Mungu katika Yeye.” (Vos 1979: 245) Kulingana na **Zab 110:1**, Kristo ataendelea kutawala kutokea mbinguni *hadi* maadui wake wote wamenyenyekehwa. Ni *parousia* yenyewe ambayo inadhihirisha kikamilika kwa ushindi wa mwisho wa Kristo (yaani, kuingia katika utimilifu wa—“bado,” ya sehemu ya uzima wa milele wa ufalme). Gruenler anahitimisha kwamba, katika kifungu hiki kifupi, Yesu “siyo tu kwa namna ya fumbo anafunua asili yake ya kiungu na ya kibinadamu lakini pia unabii kupitia maneno ya Zaburi kuhusu ufuluo wake ujao na kuinuliwa hadi mkono wa kuume wa Baba. Kwasababu hiyo, ufalme wa Yesu wa kimasihii unazidi ule wa kisia wa Daudi na matarajio ya kitaifa dhidi ya adui zake. Vita yake inatuingiza katika anga la giza la nguvu za giza zinazoshikilia nafasi ya wanadamu na mataifa; hivyo lengo lake kama Masihi ni kuweka adui zake chini ya miguu yake (mst. 36). Tukiwa na ushahidi wa mst.ari huu uliojificha Yesu anafikia nafasi ya juu ya mamlaka katika majadiliano yake na watafsiri wa maandiko, akiwaweka chini ya miguu yake anapochukua nafasi ya yule mwenye mamlaka na nafasi ya kile ambacho hekalu la Agano la Kale kiliwakilisha.” (Gruenler 1989: 790)

MASWALI YA KUJADILI

1. Jibu la Yesu kwa swali la **mst. 37** lilikuwa nini (yaani, kama Daudi alimuita Kristo “Bwana,” Kristo anawezaje tena kuwa Mwana wa Daudi)?

⁵⁶ Neno la Kigiriki katika **mst. 26** linaonesha hivi. Neno lililotafsiriwa “kukomesha” (*katargeitai*) liko katika hali ya wakati uliopo unaoendelea. Grosheide anatoa maoni yake, “neno la wakati uliopo katika mst.ari wa. 26 linamaanisha kuwa mauti *ilikuwa inakomesha*. Tendo hilo limeshaanza tayari kwasababu Kristo amefufuka kama malimbuko.” (Grosheide 1953: 368; angalia pia Fee 1987: 757; Thistleton 2000: 1234-35).

2. **Zab 110:1**, ilinukuliwaje na Yesu katika **mst. 36**, kinabii nan i mambo gani yaliyokuwa yakinabiriwa?

- Ni kwa jinsi gani maandiko yanaonesha kwamba Yesu anatawala *sasa*?

12:38-40: ³⁸ *Akawaambia katika mafundisho yake, “Jihadharini na waandishi, wapendao kutembea wamevaa mavazi marefu, na kusalimiwa masokoni,* ³⁹ *na kuketi mbele katika masinagogi, na viti vya mbele katika karamu;* ⁴⁰ *ambao hula nyumba za wajane, na kwa unafiki husali sala nefu; hawa watapata hukumu iliyo kubwa.”*

mst. 38-40—Onyo dhidi ya unafiki wa waandishi

Onyo hili linakamilisha mwisho wa huduma ya wazi ya Yesu kule Yerusalem. Baada ya hili, mafundisho yake yatabakia kwa wanafunzi wake tu (na kwa Wayahudi na wakuu wa Kirumi baada ya kukamatwa kwake). Ni wazi kwamba mafundisho ya mwisho ya Yesu kwa watu wote yalihusiana na mambo ya mafundisho ya waandishi kuhusu tabia namtindo wa maisha. Cole anaeleza kwamba waandishi walikuwa “wamejitolea katika maandiko ya kibiblia zaidi ya wengine wachache waliojaribu; alikuwa watu wa kutunza mapokeo na kuheshimu njia yao kwa namna walivyojua. . . . Kwa wale wanaoipokea Bilia kama mtawala wa imani na mwenendo, hakuna udhuru kwa kutokuitii.” (Cole 1989: 270). Maneno ya Yesu kwamba watu kama waandishi “*watapokea adhabu kubwa zaidi*” (**mst. 40**) ni matumizi ya kile alichokisema katika **Luka 12:48b**, “*Na kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakwa vingi; naye waliyemwekea amana vitu vingi, kwake huyo watataka na zaidi.*” Maoni yake pia yanaakisi kile alichosema katika **Mat 6:2, 5, 16** kwamba wale wanajifanya watu wa dini ili waonekane na kuwatambuliwa na watu “*wamekwisha pokea thawabu yao.*” Kwa maneno mengine, kujifanya ni mtu wa Bwana ili uonekane na kutambuliwa na watu wameshapokea thawabu sasa na watakataliwa na kuhukumiwa baadaye.

Kujiweka katika nafasi mwenyewe na kutamani fedha za waandishi ni tatizo la wengi katika uongozi wa kanisa la leo. Biblia inafunua ni tabia gani, maadili, vipaumbele, nia, na mtindo wa maisha wa mkristo wa kweli unavyopaswa kuwa. Makabrasha ya zamani ya kanisa, yaitwayo *Didache* (c. 70-110), yanakazia umuhimu wa kutathimini nia ya mtu na mtindo wa maisha ili kubaini kama ni nabii au mtume wa kweli au wa uongo. Yanasema: “Sasa kuhusu mitume na manabii, watendeeni kama ipasavyo kanuni ya injili. Kila mtume anayekuja kwenu mkaribisheni kana kwamba angekuwa Bwana. Lakini asikae zaidi ya siku moja, isipokuwa kama kuna ulazima, ambapo anaweza kukaa siku nyingine. Lakini kama atakaa siku tatu, ni nabii wa uongo. Na mtume anapoondoka, asichukue kitu isipokuwa mkate hadi atakapofika sehemu yake ya pili ya kulala. Lakini kama akiomba pesa, ni nabii wa uongo.

Kadhalika, msimpime au kumtathimini nabii anayenena katika roho, kwa kuwa kila dhambi itasamehewa, isipokuwa dhambi hii haitasamehema. Hata hivyo, siyo kila anenaye katika roho ni nabii, isipokuwa anadhihirisha njia za Bwana. Kwa mwenendo wake, hivyo, nabii na mtume wa uongo watatambuliwa. Zaidi ya hayo, nabii ye yeyote anayeagiza chakula katika roho hatakula chakula hicho; kama akila, ni nabii wa uongo. Kama nabii ye yeyote anafundisha kweli, na haiishi yale anayofundisha, ni nabii wa uongo. Lakini kila nabii anayethibitika kuwa nabii wa kweli anayefanya jambo kwa mtazamo wa unaodhihirisha hali ya kidunia ya alama yenye maana ya kanisa (ilimradi hafundishwi na ninyi kutenda anayotenda) hapaswi kuhukumiwa na ninyi, kwa kuwa atahukumiwa na Mungu. Mbali na hayo, manabii wa zamani walitenda pia kama hivyo. Lakini ye yeyote akisema katika roho, ‘Nipe pesa,’ au kitu kingine, msimsikilize. Lakini akiwaambia mtoe kwa ajili ya wengine wenye mahitaji, mtu asimhukumu.” (*Didache* 1989: 11.3.-12)

Maarifa makubwa na nafasi kubwa hubeba uwajibikaji mkubwa na, kwasababu hiyo, kutoaji mkubwa wa hesabu. Shauku ya waandishi na viongozi wengi wa kanisa leo vinadhihirisha kuwa hawampendi wala kumwabudu Bwana kabisa. Kama Yesu alivyosema katika **Mat 6:1**, “*Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao; kwa maana mkifanya kama hayo, hampati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni.*” Nia zetu na shauku huonesha hali yetu halisi ya kiroho. Tunahitaji kutilia maanani katika mioyo yetu onyo la Yesu na siyo kufunika ulafi na ubinagsi wetu kwa “*maombi marefu*” (**mst. 40**). Hatuwezi kumdanganya Mungu.

MASWALI YA KUJADILI

1. Ni hali zipi za ndani ya moyo na nia ambazo zilipelekea vitendo vya Yesu kuhukumu katika **mst. 38-40**?

2. Ni kwa njia gani viongozi wa Wakristo wa leo wanaangukia katika tabia na hali kama hizo au zinazofanana na zile ambazo Yesu alizikataa katika kifungu hicho?

- *Wewe unafanyaje?*

3. Viongozi wa Wakristo *wanapaswa* kuishi kwa tabia zipi?

12:41-44: ⁴¹ *Naye akaketi kulielekea sanduku la hazina, akatazama jinsi mkutano watiavyo mapesa katika sanduku. Matajiri wengi wakatia mengi.* ⁴² *Akaja mwanamke mmoja, mjane, maskini, akatia senti mbili, kiasi cha nusu pesa.* ⁴³ *Akawaita wanafunzi wake, akawaambia, Amin, nawaambia, Huyu mjane maskini ametia zaidi kuliko wote wanaotia katika sanduku la hazina;* ⁴⁴ *maana hao wote walitia baadhi ya mali iliyowazidi; bali huyu katika umaskini wake ametia vyote alivyokuwa navyo, ndiyo riziki yake yote pia.*

mst. 41-44—Senti mbili za mjane

Maelezo haya ya Yesu yanalinganishwa na maoni yake kuhusu waandishi katika **mst. 38-40**.

Katika kulinganisha na waandishi waliokuwa wakijishuhudia wenyewe mambo mazuri, kwa kuleta picha duni kwa wajane, mjane hapa alikuwa akitoa kwa kujinyima kile ambacho alikihitaji na, kwa upendo alio nao kwa Mungu, alitakia ustawi mwema wa Hekalu la Mungu na wengine. Yesu aligundua kwamba hata zawadi ndogo ya sarafu ya shaba inaweza kuwa na maana kubwa kiroho kuliko maelfu ya shekel au talanta. Sababu yenewe ni kwamba, kulingana na kanuni ya kutoa dhabihu, jambo muhimu sana siyo ni kiasi gani mtu anatoa, lakini nia ya ndani ya utoaji huo nan i kiasi gani mtu amebakia nacho baada ya kutoa. Wakati huo huo, kama sehemu ya ngazi ya pili ya kifungu hiki “kinaweza kikaakisi maombolezo kuhusu mfumo wa *ulioruhusu* mwanamke kujifilisi rasilimali zaidi” (Blomberg 1999: 144-45).

Katika makanisa yetu yatupasa kuwa waangalifu tusiwayonye au kutumia hila kwa watu katika utoaji kiasi cha kuwasukuma watu maskini kuwa maskini zaidi. Kuna makanisa ambayo husifia wafadhili wanaotoa kiasi kikubwa cha pesa lakini hawawasifii watu maskini wanaotoa kiasi kidogo. Makanisa kama hayo yana mitazamo ya kidunia na hawatambui, kama Yesu alivyosema, kwamba machoni mwa Mungu wale wanaoweza kutoa kiasi kidogo tu wanaweza kuwa wakarimu kwa mbali sana kuliko wanaotoa kiasi kikubwa. Makanisani kwa hakika yatupasa kufundisha watu kuhusu kanuni za utoaji, lakini pia yatupasa kufundisha kuhusu namna ya kutunza pesa zao vizuri na kujitosheleza.

MASWALI YA KUJADILI

1. Yesu anatoa kanuni gani katika **mst. 43-44** kuhusu utoaji?

2. Lipi au yapi ya muhimu kwamba yatupasa tujifunze katika mlinganisha kati ya waalimu wa sheria (**mst. 38-40**) na maskini mjane (**mst. 41-44**)?

3. Tunawezaje kuthibitisha kitendo cha mjane na kukubaliana na sifa za Yesu kwake, lakini baadaye tusifuate mfano wake? Tunawezaje kurekebisha tatizo hili?

13:1-37: ¹ *Hata alipokuwa akitoka hekaluni, mmoja wa wanafunzi wake alimwambia, Mwalimu, tazama, yalivyo mawe na majengo haya!* ² *Yesu akajibu, akamwambia, Wayaona majengo haya makubwa? Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomolewa.* ³ *Hata alipokuwa ameketi katika mlima wa Mizeituni, kuelekea hekalu Petro, na Yakobo, na Yoh, na Andrea walimwuliza kwa faragha,* ⁴ *Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayu ni nini dalili ya wakati, hayo yote yatakapokuwa karibu kutimia?*

⁵ *Yesu akaanza kuwaambia, Jihadharini, mtu asiwadanganye.* ⁶ *Wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ndiye, nao watadanganya wengi.* ⁷ *Nanyi mtakaposikia habari za vita na uvumi wa vita, msitishwe; hayo hayana budi kutukia, lakini ule mwisho bado.* ⁸ *Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na matetemeko ya nchi mahali mahali; kutakuwako na njaa; hayo ndiyo mwanzo wa utungu.* ⁹ *Nanyi jihadharini nafsi zenu; maana watawapeleka ninyi mabarazani; na katika masinagogi mtapigwa; nanyi mtachukuliwa mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu, kuwa ushuhuda kwao.* ¹⁰ *Na sharti Injili ihubiriwe kwanza katika mataifa yote.* ¹¹ *Na watakapowachukua ninyi, na kuwasaliti, msitafakari kwanza mtakayosema, lakini lo lote mtakalopewa saa ile, lisemeni; kwa maana si ninyi msemao, bali ni Roho Mtakatifu.* ¹² *Na ndugu atamsaliti ndugu yake ili auawe, na baba atamsaliti mtoto, na watoto watashambulia wazazi wao, na kuwafisha.* ¹³ *Nanyi*

mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kusaburi hata mwisho, ndiye atakayeokoka.

¹⁴ *Lakini mlionapo chukizo la uharibifu likisimama pasipolipasa, (asomaye na afahamu), ndipo walio katika Uyahudi na wakimbile milimani;* ¹⁵ *na mtu aliye juu ya dari asishuke, wala asiingie kuchukua kitu nyumbani mwake;* ¹⁶ *naye aliye shambani asirudi nyuma kulichukua vazi lake.* ¹⁷ *Lakini ole wao wenye mimba, nao wanyonyeshao siku hizo!* ¹⁸ *Ila ombeni yasitokee hayo wakati wa baridi.*

¹⁹ *Kwa maana siku hizo zitakuwa na dhiki, jinsi isivyokuwa tangu mwanzo wa kuumba alipoumba Mungu hata sasa, wala haitakuwa kamwe.* ²⁰ *Na kama Bwana asingalizikatiza siku hizo, asingeokoka mtu ye yote; lakini kwa ajili ya wateule alioivateua amezikatiza siku hizo.* ²¹ *Na wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule, msisadiki;* ²² *kwa maana wataondoka Makristo wa uongo, na manabii wa uongo, watatoa ishara na maajabu, wapate kuwadanganya, kama yamkini, hata hao wateule.* ²³ *Bali ninyi jihadharini; nimekwisha kuwaonya yote mbele.*

²⁴ *Lakini siku zile, baada ya dhiki hiyo, jua litatiwa giza, na mwezi hatautoa mwanga wake.* ²⁵ *na nyota za mbinguni zitakuwa zikianguka, na nguvu zilizo mbinguni zitatikisika.* ²⁶ *Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu nydingi na utukufu.* ²⁷ *Ndipo atakapotumwa malaika na kuwakusanya wateule wake toka pepo nne, toka upande wa mwisho wa nchi hata upande wa mwisho wa mbingu.*

²⁸ *Kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake liishapo kuwa laini, na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno ni karibu;* ²⁹ *nanyi kadhalika, myaonapo mambo hayo yanaanza, tambueni ya kuwa yu karibu milangoni.* ³⁰ *Amin, nawaambieni, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatimie.*

³¹ *Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe.*

³² *Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba.* ³³ *Angalieni, kesheni, [ombeni], kwa kuwa hamjui wakati ule utakapokuwapo.* ³⁴ *Mfano wake ni kama mtu mwenye kusafiri, ameiacha nyumba yake, amewapa watumwa wake amri, na kila mtu kazi yake, naye amemwamuru bawabu akeshe.* ³⁵ *Kesheni basi, kwa maana hamjui ajapo bwana wa nyumba, kwamba ni jioni, au kwamba ni usiku wa manane, au awikapo jimbii, au asubuhi;* ³⁶ *asije akawasili ghafula akawakuta mmelala.* ³⁷ *Na hilo niwaambialo ninyi, nawaambia wote, Kesheni”*

mst. 1-37—Hotuba Mlima wa Mizeituni

Hotuba kenyé mlima wa mizeituni (angalia pia **Mat 24:1-25:46; Luka 21:5-36**) ndiyo hotuba ya Yesu ya kieskatolojia iliyofuata na muhimu zaidi na ya kina. Inaitwa hotuba katika mlima wa mizeituni kwasababu **Mat 24:3** inasema kuwa Yesu alikuwa ameketi katika mlima wa mizeituni wakati anaitoa. Ndani yake anashughulika na uharibifu utakaopata Yerusalem na hekalu ambaa ulitokea mwaka wa 70 BK, anazungumzia kurudi kwake mara ya pili, anawatia moyo wanafunzi wake kuhusiana na matukio haya ya kieskatolojia, na anahitimisha hukumu ya mwisho ambayo itatokea atakaporudi.⁵⁷ [jm1]

1. mst. 1-4—Muktadha wa hotuba kwenye mlima wa mizeituni

“Wengi wanakubali kwamba hotuba ya mlima wa mizeituni ina uhusiano na (a) Israeli kumkataa Kristo, (b) Kristo kumkataa Israeli, na (c) swalii la wanafunzi katika Mathayo 24:3 [**Marko 13:4; Luka 21:7**]” (Toussaint 2004: 474). Muktadha unaojitokeza mapema ulikuwa ule wa hekalu. Wakati Yesu alipoliachaa hekalu kwenda mlima wa mizeituni, wanafunzi wake walikuwa wametaja jinsi hekalu lilivyokuwa linapendeza na jinsi majengo yake yalivyokuwa ya kipekee. Yesu aliiptikia kwa kuwaambia, “*Wayaona majengo haya makubwa? Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomolewa.*” (**Marko 13:2**) Tamko hilo kuhusiana na hekalu Tamko hilo kuhusiana na hekalu liliamsha swalii lao la, “*Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayoo ni nini dalili ya wakati, hayo yote yatakapokuwa karibu kutimia?*” (**Marko 13:4**). Mathayo anaongeza kwamba wanafunzi waliongezea swalii lao, “*nayoo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?*” (**Mat 24:3**). Hotuba ya mlima wa mizeituni ni jibu la Yesu kwa maswali hayo.

2. mst. 5-13—Dalili ya wakati

Sehemu hii ya mazungumzo “Yesu anashughulika na mambo fulani ya dhahiri kipindi cha kipekee cha mbeleni. Tunakumbushwa katika [**mst. 7**] kwamba mwisho hauji mara moja, kwamba shughuli za mdanganyaji, na taarifa za vita na tetesi za vita, hazipaswi kuchukuliwa kama alama zenye nguvu za hakika ya mwisho wa dunia. (cf. Luk 19:11); na katika [**mst. 8**] kwamba vita, njaa, na matetemeko ya nchi ni mwanzo tu wa utungu.” (Murray 1977: 388) Rejea ya Kristo kwa wanafunzi wake kuhusu “*kuchukiwa na wote*” (**mst. 13**) na kuhubiriwa kwa injili “*kwa mataifa yote*” (**mst. 10**) ni mambo ya kutukumbusha

⁵⁷ Hotuba ya mlimali inachambuliwa kwa kina katika Menn, 2017, sura ya VIII.

“kuwepo kwa kipindi kirefu ambacho matukio ya kihistoria yatahitaji ili kutimia. Hata hivyo, sehemu hii ya mazungumzo inatuleta kwenye kile ambacho hakika ni kina msaada ule ule kama ‘mwisho wa wakati’ katika lile swalii la wanafunzi [**Mat 24:3**], yaani, “mwisho”—‘kisha ndipo ule mwisho utakapowadia’. Hivyo tunashawishilka kufikiria [**Mat 24:4-14; Marko 13:5-13; Luka 21:8-19**] kama, mukhtasari, habari za utabiri wa matukio ya mbeleni.” (Ibid.) Hivyo ndivyo *Didache* 16 (c. 70-110) inapoingia kuhusiana na sehemu hii ya mazungumzo.

3. mst. 14-23—Kuanguka kwa Yerusalem na maelezo ya marudio

Sehemu hii inaanza na kuanguka kwa Yerusalem katika mwaka wa 70 BK, halafu baada ya hapo marudio ya kipindi cha matukio yatakayotokea. Haiwezekani kuwa ni muendelezo, kwasababu [**mst. 10, 13**] imetufikisha mwisho. Lazima iwe, kwa sehemu, marudio ya maelezo. Bwana wetu alitabiri mambo fulani ya nyongeza ya kipindi cha mbele kwa wanafunzi wake ambacho kiliachwa katika [**mst. 5-13**], na kinatoa maonyo na ushauri unaoendana na matukio yatakayokuwepo.” (Murray 1977: 388)

“*Chukizo la uharibifu*” (**mst. 14**) liliwa linarejea katika **Dan 8:13; 9:27; 11:31; 12:11**. Katika mwaka wa 167 KK. Antiochus Epiphanes, mfalme wa Seleucid, alikuwa ametoa dhabihu ya nguruwe katika madhababu na kuifungia dini ya kiyahudi kisheria. Hilo liliamsha uasi wa Wamakabayo wa mwaka 167–164 KK. (Bartlett 1993: 476; Metzger 1957: 132) Katika 1 Mak 1:54, “*chukizo la uharibifu*” lilihusishwa na kunajisiwa kwa madhababu ya hekalu na Antiochus. Hata hivyo, katika karne ya kwanza wengi katika Israeli waliamini kwamba Antiochus hakuwa ametimiza kikamilifu unabii wa danieli wa “*chukizo la uharibifu*.” Desmond Ford anahuisha kwamba Daniel “alikuwa ameahidi kutokea kwa ufalme wa Mungu baada ya nyumba ya Mungu kunajisiwa kwa makusudi na mfalme. Lakini kwa hakika ufalme haukuwa umekuja na kule kuwekwa wakfu tena kwa hekalu mwaka wa 165 KK. Kwahiyo, walifikiri, ile ole chini ya Antiochus itakuwa imeashiria hali mbaya zaidi itakayokuja.” (Ford 1979: 157)

Katika mazungumzo ya mlimani, Yesu kadhalika anaziona nyakati za Antiochus kama picha ya mfano wa awali wa kile kilichoko mbele. Anatumia lugha ile ile ya kinabii na kujibu—au, basi anasema kwamba kutimia kwenyewe kunakohusiana na taifa kumkataa (linganisha na **Dan 7:13** na **Marko 13:26; Dan 8:13** na **Luka 21:24; Dan 9:27** na **Marko 13:14; Dan 11:31** na **Marko 13:14; Dan 12:1** na **Marko 13:19**). Hekalu litanajisiwa tena na hakika, litaharibiwa. Hilo lilitimia mwaka wa 70 BK wakati warumi walipoharibu hekalu kabisa kwa kulichoma moto. Baada ya ukweli huu, hivyo ndivyo mwanahistoria wa wa Kiyahudi wa kanisa la kwanza alivyoeleza: “Na hakika ilikuja kutokea, kwamba taifa letu lilikutana na mambo haya chini ya utawala wa Antiochus Epiphanes, kulingana na maono ya Danieli, na kwamba aliandika miaka mingi kabla hayajatokea. Kwa namna ile ile Danieli pia aliandika kuhusiana na serikali ya Kirumi, na kwamba nchi yetu inatakiwa kufanywa utupu na warumi.” (Josephus 1987a: 285 [*Antiquities*: 10.11.7]) Clement of Alexandria [c. 150-215] (1885: 1.21), Tertullian [c. 160-220] (1885: 8), na mwanahistoria wa kanisa la kwanza Eusebius [c. 263-339] (1988: 86 [*Ecclesiastical History* 3.5.4]) pia alichukulia maono ya Danieli hivyo.

Utambulisho maalumu wa “*chukizo la uharibifu*” haliko wazi lakini linahusiana na matukio ya mwaka wa 66-70 BK kule yerusalem na hekaluni. **Luka 21:20** (“*Lakini, hapo mtakapoona mji wa Yerusalem umezungukwa na majeshi, ndipo jueni ya kwamba uharibifu wake umekaribia*”) yanaungana na maneno ya Yesu katika **Mat. 23:38** kwamba “*Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa.*” Kitendo chenyewe cha majeshi kuzunguka siyo ishara ya “ukiwa” bali dalili kwamba “umekaribia.” Hilo linatuambia kwamba ukiwa ni kuharibiwa kwa hekalu na mji (angalia na Schnabel 2007: 376). Kwa nuru ya hapo juu, Rikk Watts kwa busara anatahadharisha, “Labda kujaribu kupita kisasi kutafuta usahihi wa utambulisho ni upotoshaji. Ingawa Marko 13, kwa wazi anarejea tukio la kihistoria, anafanya hivyo kwa kutumia “topoi” [maongezi au wazo la kiufundi] ya kinabii. Kama inavyokuwa kwa lugha zingine za kinabi, la kujali umuhimu wa tukio, siyo usahihi wa maelezo” (Watts 2007: 224).

Ijapokuwa baadhi ya watu wanachukulia “*chukizo la uharibifu*” kama alama inayomuonesha Mpinga Kristo wa “wakati wa mwisho,” sivyo ilivyo. Wosia wa Yesu kwa wanafunzi wake, “*Mtakapoona*” chukizo la uharibifu au Yerusalem imezungukwa na majeshi (**mst. 14**) inatuambia matukio ya mwaka wa 70 BK, kwa kuwa Yesu alikuwa akiongea na wanafunzi wake: “*Mta*” ambacho ni kiwakilishi cha wingi wa nafsi ya pili, na matukio ya mwaka 70 BK yalitokea katika kipindi cha maisha ya mitume. “Kwa hakika Yesu hakanushi hekalu la karne ya kwanza alipokuwa amesimama ([Matt] 24:1) kwa kulitangaza “ukiwa” ([Matt] 23:38), inatabiri kuharibiwa kwake kabisa ([Matt] 24:2), kisha akijibu swalii la ‘mambo haya yatatokea lini?’ na akionya kuhusu ‘chukizo la uharibifu’ (mst. 3), na akionya kuhusu ‘chukizo la uharibifu’ (mst. 15) akizungumzia tu uharibifu wa hekalu tofauti kabisa miaka elefu mbili baadaye!” (Gentry 1999a: 24)

Zaidi ya hayo, rejea zote katika **Dan 9:27** na **11:31** ambazo zinazungumzia mchochezi wa

machukizo, na historia ya kimakabayo, “inamuonesha mtu wa kihistoria, na siyo mtu ambaye ni zaidi yaapo” kama chukizo (Such 1999: 95). “Kwa hakika, ambaye anadhaniwa kuwa Mpanga Kristo hasa [mst. 14a] hatatoa nafasi ya ‘kristo wa uongo mwingine’ katika [v. 22]” (Ibid.: 96). Mwisho, kwasababu Israeli kama taifa na hekalu lao vilikuwa ni “aina,” “alama,” “vivuli,” “nakala,” au “mifano” ya uhalisia wa AJ (**Mat 5:17; 1 Kor 10:1-6; 2 Kor 3:12-16; Gal 3:23-4:7, 21-31; Kol 2:16-17; Ebr 1:1-2; 8:1-10:22**), hekalu na sadaka zake zilikuwa zimekamilishwa na kufunikwa na Kristo (**Mat 5:17; Marko 14:58; Yoh 2:18-22; 2 CKor 3:12-16; Gal 3:23-4:7; Ebr 4:14-5:10; 7:1-10:22**). Kwahiy, hata kama hekalu likijengwa upya kule Yerusalem litakuwa ni hekalu sanamu, likiwa halina tena maana ya kitheolojia kuzidi hekalu la kihindu au msikiti wa kiiislamu. Hakuna chochote ambacho kinaweza kutokea katika hekalu lililojengwa upya kinaweza kuwa “*chukizo la uharibifu*.”

Shauri linatisha kwa kutafsiri mausia ya kukimbilia Yudea (**mst. 14-18**) kama jambo la kieneo na kihistoria: “V. G. Simkhovitch wa zamani sana alijitosa katika moyo wa swala hili alipouliza ‘kama inamaanisha mwisho wa dunia, inaleta tofauti gani iwe kwamba mwisho huo unakuja wakati wa baridi au kiangazi?’ Na C. H. Dodd akifuatia mkondo huo huo anathabitisha kwamba uharibifu katika mistari hii unakubaliana vizuri kabisa na hali ya kuzingirwa. Isipokuwa kama mistari hii itakuwa inazungumzia kuharibiwa kwa Yerusalem na hekalu, Kristo atakuwa hajajibu kikamilifu kilichouliwa na wanafunzi wake ambaa ndio waliochokoza mada.” (Ford 1979: 65-66) Katika **Luka 21:20** wosia wa kukimbilia unaletwa na “*mtakapoona Yerusalem umezingirwa na majeshi*.” Katika **Marko 13:14** tukio linaloamsha mambo linaonekana katika “*mtakapoliona chukizo la uharibifu limesimama pasipolipasa*.” Kwa hakika, Yerusalem ulizingirwa na Warumi mata nyngi (katika mwaka wa 66, 68, na 70 BK) kabla ya kuharibiwa kabisa (Gentry 1999a: 48-50). Eusebius anatuambia kwamba kanisa kule Yerusalem lilikuwa limeamriwa kwa ufunuo wa kiungu ultiotolewa kabla ya vita [ushahidi wa mazungumzo ya mlimani] na hivyo wakatoka mjini na wakaishi katika mji wa Pella nyuma ya Yordani (Eusebius 1988: 86 [*Ecclesiastical History* 3.5.3]). Hilo laweza kuwa lilitokea katika mwaka wa 68 BK (Carson 1984: 501).

Mistari 19 unaturudisha kwa “*jinsi isivyokuwa tangu mwanzo wa kuumba alipoumba Mungu hata sasa, wala haitakuwa kamwe*.” Kumekuwa na idadi kubwa ya vifo, ikiwa ni pamoja na vifo vyta Wayahudi, kutohakana na vita tangu wakati huo (mfano, Vita kuu ya I na II, na mauaji ya Wayahudi yaliyochukua takribani Wayahudi milioni 6 katika vita kuu ya II). Kwahiy, watu wengi hawaoni ni kwa namna gani “*dhiki kuu*” inaweza kuhusishwa na matukio ya mwaka wa 70 BK. Kuna sababu nne kwa uchache kwanini “*dhiki kuu*” ihusishwe na matukio ya mwaka wa 70 BK, na siyo matukio fulani ya “mwisho wa nyakati” wakati wa kukaribia kurudi mara ya pili.

- **Muktadha wa mazungumzo katika mlima wa mizeituni**. Muktadha wa mazungumzo katika mlima wa mizeituni unatuwekeea msingi wa muktadha wa “*dhiki kuu*” katika mwaka wa 70 BK ambaa Kristo anauzungumzia. Maneno yote ya Kristo katika **Mat 23:38** kwamba “*nyumba yenu itaachwa ukiwa*,” na tukio lenyewe la mazungumzo katika mlima wa mizeituni (**Mat 24:1-3; Marko 13:1-4; Luka 21:5-7**) kimsingi yanaangalia kuharibiwa kwa hekalu na Yerusalem. Vivyo hivyo, muktadha unaofuatia *mara* wa Kristo kuhusisha “*dhiki kuu*” unaangalia matukio ya mwaka wa 70 BK. Kisarufi, **Mat 24:21** na **Marko 13:19** wote wanaunganisha kuhusiana na “*dhiki kuu*” kufuatia muktadha wa mwaka wa 70 BK. (yaani, kukimbilia Yudea) kwa kuwa mistari yote inaanza na neno “*kwa*” (Kigiriki = *gar*). Kwa maneno mengine, sababu za kukimbilia ni “*kwa [au kwasababu'] kutakuwa na dhiki kuu*” (**Mat 24:21**) au, kama Marko anavyooleza, “*kwa [au kwasababu'] siku hizo zitakuwa nyakati za dhiki*” (**Marko 13:19**). Kifungu kinachoendana na hiki katika Luka kina mpangilio tofauti wa maneno lakini kwa maana ile ile. **Luka 21:20-21** anabainisha muktadha wa wale watakao kuwa Yudea wakikimbilia milimani “*mtakapoona Yerusalem umezingirwa na majeshi*.” Sababu hasa yah ii “*dhiki kuu*” ilikuwa ni tukio la kieneo, tofauti na kuenea dunia nzima, tukio la nyakati za mwisho, ndicho kilichowawezesha wanafunzi wa Yesu kukimbilia.

- **Maneno ya Yesu ni sahihi**. Katika muktadha wa Israeli na Yerusalem, maneno ya Yesu kuhusu matukio ya mwaka 70BK kuwa ni matukio mawili ya dhiki yasiyofanana inathabitishwa na ushahidi. Mwanahistoria Myahudi wa karne ya kwanza Josephus anaoleza kwa kina ukatili, mauaji, magonjwa, njaa, watu kula watu, na vifo vyta wakazi milioni 1.1 na wafungwa wapatao 97,000 zaidi (Josephus 1987b: 719-20, 737, 749 [Vita: 5.10.2-5; 6.3.3-4; 6.9.3]). Anahitimisha, “Wala hapakuwepo na mji mwingine ule uliokumbana na mateso kama hayo wala hakuna wakati ulizalisha kizazi kilichokuwa na matendo ya uovu kama ilivyokuwa kwa kizazi hiki, tangu kuwepo kwa dunia” (Ibid.: 720 [5.10.5]). Carson anaongezea, “Kumekuwepo na idadi kubwa ya vifo—milioni sita kwa vifo vyta kambi za wanazi, na inakisiwa kama milioni ishirini chini ya Stalin—lakini haikufikia asilimia kiasi cha idadi kubwa ya wakazi wa mji kuuwawa kwa mateso na kufanywa watumwa kama wakati wa kuanguka kwa Yerusalem” (Carson 2010: 563). Zaidi ya hayo, katikamaana ya *theologia* hakika hii ilikuwa “*dhiki*

kuu” kwa Israeli kwasababu, kutokana na hiyo hawakuwa na hekalu tena kwasababu ndivyo sheria yao ilivyopitishwa” (Gentry 1999b: 198). Hatimaye, tangu mwaka wa 70 BK dini ya kiyahudi haijaweza kurejea katika desturi zinazolingana na AK.

- Umuhimu wa matukio baada ya “dhiki.” Maneno ya Yesu katika **mst. 19** yanataka kipindi irefu cha kihistoria *baada ya “dhiki”* ili maneno yake yalete maana. “Kwamba Yesu katika [mst. 19] naahidi kwamba ‘mahangaiko makubwa’ kama hayo hayatarajwi kulinganishwa kwamba hayahusiani na dhiki ya siku za mwisho; kama kilichotokea baada ya hapo ni milenia au mbingu mpya na nchi mpya, inaonekana ni ujinga kusema kwamba ‘mahangaiko makubwa, hayatatokea tena’ (Carson 2010: 563; angalia pia Lane 1974: 472; Schnabel 2011: 40n.30). Zaidi sana, “Bwana hahusishi na tukio la kurudi kwake mara ya pili, vinginevyo yatupasa kushangaa kwanini wanafunzi wake waombe kukimbilia kutoka Yudea ([Mat 24:16]:16): kukimbilia milimani wakati wa kurudi kwa Yesu kutasaidia nini? Kwanini ‘baridi’ iwe jambo la kuangaliwa wakati huo?” (Gentry 1999a: 53) Matokeo yake, nyongeza ya maneno “*wala haitatokea tena*” mwishoni mwa maneno ya Yesu kuhusiana na ukali wa “*dhiki*” inamaanisha kwamba kutakuwepo na dhiki kadhaa baada ya kuanguka kwa Yerusalem, “na kulingana na hayo nyongeza inaendana na ‘huo mwisho bado’ wa [mst. 7]” (Beasley-Murray 1993: 419).
- Matumizi ya Yesu ya lugha ya kinabii. Lugha ya Yesu inafanana na lugha ya kinabii inayoonekana mara nyingi katika matamko ya kibiblia ya hukumu, kwahiyu ni muhimu isichukuliwe kama lugha ya kawaida isiyo na fumbo. Lugha kama hiyo inapatikana ehemu zingine kuhusiana na matukio ya kimajanga. Katika kuzungumzia uteka wa Babeli na kuharibiwa kwa Yerusalem mwaka wa 587 KB, **Dan 9:12** anasema: “*chini ya mbingu zote halikutendeka jambo kama hili, iliviyotendeka juu ya Yerusalem.*” Katika unabii unaohusiana na tukio hilo hilo la mwaka 587 KK, **Ezek 5:9** anatumia lugha inayokaribiana sana na ya Kristo katika **Mat 24:21**: “*Kwa kuwa wakati huo kutakuwapo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe.*” **Ezek 7:5-6** inaendelea kuwaita Wababeli kuuchukua Yerusalem “*janga la kipekee*” na anasema “*mwisho umewadnia!*” Vifungu hivyo vilizungumza kuhusu “tukio la kipekee” ambalo litaikumba Yerusalem na halitatokea tena. Hata hivyo, Yesu alitumiaina *ile ile* ya lugha kuhusu hukumu *nyingine* ambayo ingekuja (na ilikuja) juu ya Yerusalem. Hivyo, ingawa wengine wanaweza wakafikiri kwamba “*dhiki kuu*” anayotaja Yesu ni tukio la mwisho wa wakati, kiuhalisia sivyo.

Ingawa rejea kuhusiana na “*chukizo la uharibifu*” na “*dhiki*” ina uhusiano na matukio ya mwaka wa 70 BK, kanuni hiyo hiyo au kivuli cha mambo ya mbeleni kinaweza kuhusishwa na matukio yatakayotokea baada tu ya kurudi kwa Yesu, kama vitendo vya Antiochus Epiphanes vilivyotabiriwa katika mwaka wa 167 KK viliashiria matukio ya Tito na Warumi mwaka wa 70 BK.

Mistari 20-23 inaonekana kurejea kipindi chote kabla Kristo hajarudi tena. Dhamira ya mateso na makristo wa uongo inabeba tabia za kipindi chote cha kabla ya Kristo kurudi tena, siyo tu kipindi kabla ya mwaka wa 70 BK. Mateso au dhiki inayotajwa katika **mst. 20** yalitajwa pia katika **mst. 7-9, 12**. Maonyo dhidi ya Makristo wa uongo na kupotoshwa (**mst. 21-22**) yalitolewa pia katika **mst. 5-6**. Mambo hayo yote ni sifa za kipindi chote cha katikati ya matukio mawili yanayomhusu Kristo. Zaidi, katika **mst. 20** Yesu anatumia maneno ya “*kama Bwana asingepunguza siku hizo, hakuna mwenye mwili angeokoka.*” Hilo linaonesha kitu fulani cha upeo mpana wa kidunia kutokea, siyo tukio la kieneo, kwasababu msingi amba maisha ya watu wa Mungu wataokolewa ni tofauti katika hali hizo mbili: katika mwaka wa 70 BK watu kule Yudea walitakiwa “*kukimbilia milimani*” ili kuokoa maisha yao (**mst. 14**); kabla ya Kristo kuja tena watu wanaokolewa kwa siyo kwa kukimbilia bali kwa kwa Mungu “*kupunguza*” siku. Kwa maneno mengine, dhiki itakuwa na sifa inayofunika kipindi chote cha kabla ya Kristo kurudi, na hata itakuwa mbaya zaidi karibu kabisa na kurudi kwake, lakini hataruhusu kizazi kujifanyia mambo, wanadamu kujiharibu wenyewe, au watu wake kufutwa katika uso wa dunia. “*Kupunguzwa*” kwa siku hizo “*kwa ajili ya wateule,*” hakukuhitajik katika mwaka wa 70BK kwasababu, kama ilivyotajwa hapo juu, Wakristo walikuwa wamekimbilia mahali salama. Watu wasioamini wasio wayahudi watakaosalia mjini watakuwa siyo “*wateule*” wa Mungu tena baada ya kumkataa Kristo (**Mat 13:10-17; 21:18-22, 33-46; Marko 11:12-14, 20-24; 12:1-11; Luka 20:9-18**). Mwisho, **mst. 24**, unaoanza na maelezo ya Kristo kuhusu kuja kwake mara ya pili (*parousia*) unaanza, “*Lakini katika siku hizo, baada ya dhiki.*” Hili tena lina onesha kwamba dhiki itakuwa na sifa ya kufunika dunia kipindi chote kabla ya Kristo kurudi mara ya pili. Mtume Yoh alitambua hili katika **Ufu 1:9**, aliijiita “*ndugu yenu na mshiriki mwenzenu katika dhiki na ufalme.*”

4. mst. 24-27—Kurudi kwa Kristo mara ya pili

Wakati Yesu anaposema kwamba, wakati wa kuja kwake, kutakuwepo na matukio ya angani yatakayohusisha jua, mwezi, na nyota, na nguvu za mbinguni (**mst. 24-25**), hayo yanaweza yakawa ni lugha ya picha. Manabii wa AK mara kwa mara walielezea hali mbaya za kisiasa na mabadiliko ya kitawala kwa

kutumia lugha ya mifano kama mvurugano wa angani au kutupwa kwa uumbaji wenyewe. Lugha ya Yesu inanukuu kutoka katika vifungu kadhaa nya AK vinavyotumia lugha kama hiyo kwa matukio ya kisiasa: mfano, **Isa 13:10, 13** (Wamedi kuwashinda Wababeli); **Isa 34:4** (hukumu dhidi ya Edomu); **Yer 4:23-28** (hukumu dhidi ya Babiloni); **Ezek 32:7-8** (Babeli kuishinda Misri); **Amosi 5:20; 8:9** (Israeli kushindwa na Waashuru). Kwa upande mwininge, alama za angani zinaweza kuwa kama zinavyotajwa. “Ni vigumu kuwa na uhakika ni kwa kiasi gani haya yatatimia kwa katika uhalisia unaotajwa, lakini inaonekana kuna kujengeka kutoka [**Luka 21:11-25**]” (Nolland 1993: 1007). Kwa nuru inayotokea kwenye maelezo ya ishara za angani, Carson anahitimisha kwamba ishara anazoorodhesha Yesu katika **Mat 24:29; Marko 13:24-25; Luka 21:25-26**, “huenda zilikusudiwa zieleweke kama zilivyo, kwasababu ya asili ya kihali ya Mwana a Adamu kujifunua mwenyewe” (Carson 1984: 505).

Rejea ya Yesu ya “*mwana wa Adamu akija katika mawingu*” (**mst. 26**) inarejea lugha ya AK ambapo mawingu yalisimama badala ya uwepo na utukufu wa Mungu (**Kut 16:10; 19:9, 16; 24:15-16; 34:5; Lev 16:2; Hes 10:34; 11:25; Zab 18:10-13; 97:2; 104:3; Isa 19:1**). Pia yana uhusiano wa kieskatolojia (**Isa 4:5; Ezek 30:3; Dan 7:13; Zef 1:15**). Rejea yake kuhusu “kutumwa kwa malaika na kuwakusanya wateule” (**mst. 27**) pia inaa kisi luga ya AK na yale aliyo sema awali kuhusiana na kurudi kwake mara ya pili. Katika mfano huu wa ngano na magugu (**Mat 13:24-30, 36-43**) Yesu alikuwa amesema, mwisho wa nyakati, “*Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.*” (**Mat 13:41-42**). Picha kama hiyo ya “*mfano wa mwana wa Adamu . . . ameketi mawinguni*” na kuivuna dunia kuhusiana na malaika inapatikana katika **Ufu. 14:14-20**, ambayo inarejea kwenye *parousia* na hukumu ya mwisho. Rejea ya “kuwakusanya wateule” inaweza kuchukua picha kama ile ya AK ya “kukusanyika kwa Israeli baada ya kutoka uhamishoni” vifungu kama vile vya **Kumb 30:3-4; Isa 27:12-13**, na “kukusanyika kwa watu wake kwa ajili ya hukumu” vifungu vya **Zab 50:5**. “*Pande nne za dunia*” (**mst. 27**) huenda ni picha ya **Zak 2:6**, na ina maanisha dunia nzima (angalia pia **Yer 49:36**). Kuto kana na hilo, Yesu, amechukua vifungu vya AK katika hali ya kuktadha wake wa asili wa AK kuhusiana na Israeli kurudi kutoka uhamishoni (**Kumb 30:3-4; Isa 27:12-13; Zk 2:6**), na kuzitumia kama “*kitu cha kufanana*” kilichomuelezea ye ye mwenyewe na *parousia*. Mfano wa ngano na magugu na maneno ya Yesu katika **Mat 16:27; Marko 8:38; Luka 9:26** kuhusiana na hukumu yanaakisiwa na maelezo ya Luka katika hotuba kwenye mlima wa mizeituni, kwamba Kristo atakapokuja ataleta hukumu kwa maadui zake na (**Luka 21:26**) na ukombozi kwa wale walio wake (**Luka 21:28**).

5. mst. 28-31—Mfano wa mtini

Mfano wa mtini unahu siana na ishara zitakazotufikisha kwenye uharibifu wa Yerusalem mwaka wa 70 BK, na hauhusiani kabisa na kuanzishwa kwataifa la leo la Israeli katika mwaka wa 1948, kama baadhi ya wanaoshikilia migawanya ya kihistoria wanavyodai (mfano, Lindsey 1970: 53). Kwa mukhtadha, mtini unahu siana na mambo ambayo yako “karibu,” ambayo wanafunzi wake watakao kuwa hai (yaani “wewe,” “*kizazi hiki*”) watayashuhudia.⁵⁸ Kifungu kama hicho katika Luka kinatuonesha kwa namna chanya kwamba Yesu hakuwa akitumia mfano wa mtini kama rejea ya kificho ya Israeli ya leo kwani katika **Luka 21:29** anasema, “*tazama mtini na miti yote*.” Mtini ulikuwa tu ni picha au kitu ambacho kilisaidia somo kwa kile Yesu alichokuwa anaelezea kuhusu yale yanayokwenda kutokeea mapema (Schnabel 2011: 132).

Kama maneno “*mambo yote*” (**mst. 30**) yanahu sisha “ishara za angani na *Parousia* yenyewe [**mst. 24-27**], basi [**mst. 28-30**] haina maana, kwasababu hali yoyote ya kutofautisha kati ya ‘mambo yote’ na ‘ni karibu’ itakuwa imeharibiwa. . . Njia ya kawaida ya kuchukua ‘mambo yote’ ni kuyaangalia kama yanahu siana na kupotea kwa utulivu katika [**mst. 5-23**], dhiki inayokuja kwa waamini katika kipindi chote kati ya kupaa kwa Yesu na Parousia.” (Carson 1984: 507)

Kisha Yesu anasema kwamba “*kizazi hiki*” hakitapita (**mst. 30**), ni wazi anarejea *kizazi cha wanafunzi* ambao wakati huo walikuwa hai. Tukichukulia tangazo la Yesukwamba ufalme wa Mungu ulikuwa umekaribia (**Marko 1:15**) tukiunganisha na unabii wake kuhusu ku haribiwa kwa hekalu, *kitheolojia* “*kizazi hili*” ingeweza *tu* kumaanisha *kizazi* kilichokuwa hai wakati Yesu anaongea maneno haya. Maana ya kitheolojia ya “*kizazi hiki*” katika kuhusiana na unabii wa Yesu na misheni yake ni marachache imetolewa maoni, lakini katika A.J. Wright anaona na kuelezea kwa wazi: “Kama nabii, Yesu aliweka msimamo wake katika unabii wa kuanguka kwa hekalu ndani ya *kizazi kimoja* [**Mat 21:33-45; 23:29-39; 24:1-2, 15-19, 32**-

⁵⁸ Gary DeMar anaeleza kwamba, siyo tu mtini katika mfano huu, lakini “kwa wakati huu ni kama mti pekee uliokuwa na majani katika injili ni ishara ya hukumu kwa Israeli, hukumu iliyokuja kudhihirika mwaka wa 70 BK” (DeMar 1999: 402). Katika **Mat 21:19; Marko 11:13-14** Yesu anaweka wazi ukeli kwamba taifa lilikuwa linakabiliwa na hukumu isiyokwepeka kwa kuulaani mtini pekee uliokuwa na majani (Ibid.: 397-405).

34; Marko 12:1-12; 13:1-2, 14-19, 28-30; Luka 11:45-51; 13:34-35; 19:41-44; 20:9-19; 21:5-6, 20-24, 29-32; kama na ikiwa itaangukia hapo basi atahesabiwa haki. . . . Kizazi kinachomkataa Yesu lazima kiwe cha mwisho ya kabla janga kuu. Hili haliwezi kuwa lingine, kwasababu kama lingekuwepo wangehitaji nabii mwingine wa kuwaonya; mara baada ya Baba kumtuma mwana katika shamba la mizabibu [**Mat 22:33-46; Marko 12:1-12; Luka 20:9-19**], hatamtuma mtu mwingine tena. Kumkataa mwana ni kukataa nafasi ya mwisho.” (Wright 1996: 362, 365) hata kama “*kizazi hiki*” kilimaanisha kizazi cha wanafunzi ambao walikuwa hai wakati Yesu anaongea, “haimaanishi kuwa Yesu kwa makosa alifikiri Parousia ingetokea ndani ya maisha ya wasikilizaji wake. . . . Yote hayo [**mst. 30**] madai yake ni kwamba kurugu ya [**mst. 5-23**], ikiwa ni pamoja na kuanguka kwa Yesrisalemu, kunatokea ndani ya maisha kizazi kilichokuwepo wakati huo. Hii *haina* maana kwamba vurugu lazima ikome ndani ya muda huo lakini kwamba tu ‘mambo yote’ yafanyike ndani yake.” (Carson 1984: 507)

6. **mst. 32-37—Kurudi kwa Yesu hakutabiriki kabisa**

Katika **mst. 32** Kristo analinganisha “*siku hiyo au saa hiyo*” (yaani, kurudi kwake mara ya pili katika utukufu wakati wa mwisho) ambao *hakuna ajuaye, hata malaika wa mbinguni, wala mwana, isipokuwa Baba peke yake*” kwa “*mambo haya*” (**mst. 29**, yaani, matukio yanayopelekea kuanguka kwa Yerusalem mwaka wa 70 BK), ambayo “*yanakaribia*” (**mst. 28**), ambayo “*mnayaona*” (**mst. 29**), na ambayo “*kizazi hiki*” kitashuhudia (**mst. 30**). Katika AJ “*siku hiyo*” ni alama ya kieskatolojia inayojieleza vema kutumika kama siku ya Bwana, siku ya mwisho (cf. Mat. 7:22; Luka 10:12; 21:34; 2 Thes. 1:10; 2 Tim. 1:12, 18; 4:8). Kama ndivyo ilivyo, kwamba maelezo ya ‘siku’ yamechukua maana wazi ya kiufundi (cf. Rum. 13:12; 1 Kor. 3:13; 1 Thes. 5:4; Ebr. 10:23; 2 Pet. 1:19).” (Murray 1977: 394-95; angalia pia Moore 1966: 100 [“‘Siku hiyo’ inabeba sauti ya Agano la Kale [kuhusu hukumu ya mwisho na *parousia*] ambapo ‘siku’ katika matumizi ya kisasa sivyo”]) Kama ilivyo kwamba “*siku hiyo*” ni “alama ya kieskatolojia inayojieleza vema kutumika kama siku ya Bwana,” kadhalika “*saa*” husimama katika nafasi ya kurudi mara ya pili katika **Mat 24:44; Luka 12:39-40; Yoh 5:25, 28; na Ufu. 3:3; 14:7, 15.**⁵⁹ ⁵⁹ Uhusiano wa “*siku*” na “*saa*” kama maneno ya kiufundi ya kuja mara ya pili yanaonekana pia katika **Mat 24:50; 25:13; na Luka 12:46**. Anaongezea kwamba “*hujui wakati atakaporudi*” (**mst. 33**) na “*hujui ni lini mkuu wa nyumba atakapokuja*” (**mst. 35**). Hilo limeakisiwa pia katika matumizi yake ya mara kwa mara ya “*unaona*” kuhusiana na matukio yanahusu kuharibiwa kwa Yerusalem (**mst. 14, 29**) linganisha na “*wataona*” kuhusiana na kurudi mara ya pili (**mst. 26**). Kwa kifupi, Yesu anasema kwamba wanafunzi wake wa karne ya kwanza wataweza kuelewa wakati hekalu litakapokuwa linaingia katika kuharibiwa, lakini hakunayeyote atakayeweza kutabiri lini atakuja tena.

7. **Hitimisho**

Watu wengi katika historia yote wamejaribu kupiga hesabu za lini Kristo atarudi, wakitumia matukio yanayotokea mashariki ya kati au mahali pengine duniani. Majaribio kama hayo siyo sahihi na yamekuwa yakishindwa vibaya. “Ishara” za kinabii hazikuwekwa kwa namna inayompa mtu nafasi ya kupatia wakati au namna tukio lililotabiriwa litakavyokuwa. Alisema wazi kabisa kwamba “*hakuna ajuaye, hata malaika wa mbinguni, wala mwana, isipokuwa Baba peke yake*” (**mst. 32**). Angeweza kuliweka hili wazi zaidi ya hapo? Zaidi ya hayo, “ishara za nyakati” kwa makusudi ni za ujumla na zilizo wazi mwishoni “Matetemeko, njaa, vurugu za kisiasa, masihi wa uongo, mateso na kuhubiriwa kwa injili, na kuanguka kwa Yerusalem—mambo hayo siyo aina ya matukio yatakayoonesha kabisa wakati maalumu wa kihistoria lini Mwana wa Adamu atakuja. Ni aina ya mambo yatakayokuwepo katika kipindi chote katika ya kuja mara ya kwanza na mara ya pili (ingawa kuanguka kwa Yerusalem mwaka wa 70 BK kulikuwa ‘tukio moja’ maalumu). Yesu aliwaonya wafuasi wake siyo kujua tarehe ya mwisho, bali kwamba waelewe asili ya upinzani utakaowakabili na hivyo wakae wakiwa wamejiandaa ili kustahimili.” (Travis 1982: 92) Wazo kwamba hatutaweza kujua “*siku hiyo au saa hiyo*” (**mst. 32**) lakini tunaweza kutabiri juma au mwezi au mwaka au muongo au karne halina maana. “Siku” na “*saa*” haviko katika kulinganishwa na juma, mwezi, mwaka, muongo, au karne, lakini zaweza kuwa ni “maneno ya sanaa,” yanayo maanisha *tendo lenyewe la kurudi mara ya pili*.

Mwisho, mazungumzo katika mlima wa mizeituni kwa ujumla wake yanakazia kuishi kwa uaminifu kwasababu *hakuna uwezekano* wa kujua ni lini Kristo atarudi. Ingawa mazungumzo ya mlima wa mizeituni

⁵⁹ Allen Kerkeslager anahoji kwamba “kila ‘saa’ lililofuatia katika ufunuo akihusisha na *parousia*” (Kerkeslager 1991: 5). Kwa kuongezea vifungu vilivyonukuliwa hapo juu, hilo linaonekana wazi sana katika vifungu hivyo vinavyozungumzia ufufuo wa wenye haki (**Ufu 11:11-13**) na hukumu ya haki (**Ufu 11:13; 18:10, 17, 19**) unaendana na *parousia*.

yanashughulika na kurudi mara ya pili, Yesu alilingiza mambo mengi hayana budi kutokea. “Tofauti na maandiko ya kiufunuo ya kiyahudi, sehemu kubwa ya Marko 13 imewekwa katika muundo wa maagizo. Kwa mfano: ‘Tazama’ (mistari ya 5, 9, 33). ‘Msifadhaike’ (mst.ari wa 7). ‘Msiwe na wasiwasi’ (mst.ari wa 11). ‘Mjilinde! nimeshawaambia kila kitu mapema’ (mst.ari wa 23). ‘Kesheni!’ (mistari ya 35, 37). Haya yanatusaidia kuona ukweli kwamba kusudi la Yesu ni kuwatia moyo siyo kudadisi bali kuwa macho—kuimarisha imani na kuwaonya wanafunzi wake yapi watakabiliana nayo kama wafuasi wake.” (Travis 1982: 92-93)⁶⁰ Somo lote la kutabiri mwisho waweza kutokea lini siyo sababu ya Yesu kutoa hotuba. Hivyo basi, kujaribu kutabiri mwisho kutokana na yale Yesu aliyosema ni kuyatumia mazungumzo kwa kusudi ambalo silo lililokusudiwa. Hilo litatuleta katika matumizi nje ya muktadha. Popote mtu anapochukua maandiko nje ya muktadha, anajifunga kufikia hitimisho lenye makosa. James Edwards anahitimisha, “hakuna anayetiwa moyo au kusifiwa kwa kujaribu kuwa mfumbuzi wa siri za kieskatolojia. Hayo ni makosa, kwani hata Mwana Adamu hajui Mwisho [Marko 13:32]. Sifa ya uanafunzi haiku katika kutabiri mambo ya mbele bali kuwa *mwaminifu kwa yaliyopo*, hasa katika majoribu, magumu na mateso.” (Edwards 2002: 386)

MASWALI YA KUJADILI

1. Kwa nini hekalu lilikuwa jambo muhimu kwa wanafunzi? Kuharibiwa kwake kungekuwa ni alama ya namna gani?
 - Kwanini unafikiri Yesu alitumia kuharibiwa kwa hekalu kuanza mazungumzo yake kuhusu mwisho wa nyakati?
2. **Mistari 9-13** inaelezea mateso ya kanisa ambayo kiuhalisia hayajawahi kutokea katika baadhi ya maeneo. Ni kwa namna gani kutokuwepo kwa mateso haya katika maeneo kama hayo kunaathiri Ukristo?
 - Kama kutokuwepo kwa mateso haya kumekuwa na madhara hasi, ni nini, kama kipo, tunaweza kufanya?
3. Kwanini unafikiri Baba aliweka wakati wa mwisho kuwa siri?
 - Ukichukulia ukweli kwamba hakuna yeyote isipokuwa Baba anayejua ni lini mwisho wa kizazi hiki utatokea, ina maana gani kwetu “*kukesha*” (**mst. 33-37**)?

14:1-11: *¹Baada ya siku mbili ilikuwa sikukuu ya Pasaka, na mikate isiyochachwa; wakuu wa makuhani na waandishi wakatafuta njia ya kumkamata kwa hila na kumwua.* ² *Kwa maana walisema, Isiwe kwa wakati wa sikukuu, isije ikatokea ghasia katika watu.*

³ *Naye alipokuwapo Bethania, nyumbani mwa Simoni mkoma, ameketi chakulani, alikuja mwanamke mwenye kibweta cha marhamu ya nardo safi ya thamani nyingi; akakivunja kibweta akaimimina kichwani pake.* ⁴ *Palikuwa na watu waliochukizwa katika nafsi zao wakisema, Kwani kupoteza marhamu namna hii?* ⁵ *Maana marhamu hii ingaliweza kuuzwa kwa dinari mia tatu na kuzidi, wakapewa maskini. Wakamnung'unikia sana yule mwanamke.* ⁶ *Yesu akasema, Mwachen; mbona mnamaabisha? Amenitendea kazi njema;* ⁷ *maana sikuzote mnao maskini pamoja nanyi, na kila mpendapo mwaweza kuwatendea mema; lakini mimi hamnami sikuzote.* ⁸ *Ametenda alivyoweza; ametangulia kuupaka mwili wangu marhamu kwa ajili ya maziko.* ⁹ *Amin, nawaambia, Kila ihubiriwapo Injili katika ulimwengu wote, na hili alilotenda huyu litatajwa kwa kumbukumbu lake.*

¹⁰ *Yuda Iskariote, yule mmoja katika wale Thenashara, akaenda zake kwa wakuu wa makuhani, apate kumsaliti kwao.* ¹¹ *Nao waliposikia walifurahi, wakaahidi kumpa fedha. Akatafuta njia ya kumsaliti wakati wa kufaa.*

mst. 1-11—Yesu anapakwa marashi ya gharama

Matukio matatu katika sehemu hii kwa mara nyingine tena yanaonesha mfano wa “sandwich”:

⁶⁰ Ford anaongezea hili kwa kuonesha jinsi ambavyo Kristo aliyaweka mafundisho yake wa mdomo: “Lakini lililoko tangu mwanzo kuisha ilikuwa ni maonyo, ushauri wa kutenda yaliyo sawa badala ya kujuu tu au kukirii. Maneno ya kwanza na ya mwisho ya Kristo yalikuwa *blepete* [“kesheni”; “zingatia”; “tazama”]: **Marko 13:5, 9, 23, 33**], na mambo ya lazimi yanafikia kumi na tisa. Ni wazi kabisa kwamba unabii wake umebeba kusudi la kimaadili, kama ilivyokuwa pia katika mengi yay ale yaliyobashiriwa wakati wa Agano la Kale.” (Ford 1979: 82)

kupakwa mafuta kwa Yesu na mwanamke kwa ajili ya maziko yake kunachanganywa na makuhani wakuu na waandishi kupanga njama ya kumkamata Yesu kwa Yuda kukubaliana na makuhani wakuu kumsaliti Yesu, yote hayo yanaturelekeea kwenye kifo na maziko yake.

1. mst. 1-2—Njama za makuhani wakuu na waandishi dhidi ya Yesu

Kama ilivyo katika sehemuzingine nyingi, mistari miwili ya kwanza inafunua dhihaka kubwa. Katika **13:32-36** Yesu alikuwa amewataka wafuasi wake kuwa macho kwa uaminifu. Hapa, makuhani wakuu na waandishi wanajipanga kumkamata Yesu na kumuua. Zaidi ya hayo, wanasema, “*Isiwe wakati wa sikuu, kusije kukatokea fujo kutoka kwa watu*” (**mst. 2**). Pamoja na hayo ilikuwa wakati hasa wa sikuu walipomua, hata kutumia desturi wakati wa sikuu (Pilato angelimtoa mfungwa mmoja ambaye watu walimtaka, **15:8, 15**) na kusulubisha Yesu.

2. mst. 3-9—Kupakwa mafuta kwa Yesu

Kupakwa mafuta kwa Yesu kumeelezwa pia katika **Mat 26:6-13** na **Yoh 12:1-8**. Yoh, hasa, anatoa maelezo yanyuma kwa kina yaliyoachwa na Mathayo na Marko. Kwanza, kupakwa mafuta ni kurudisha mkanda nyuma ambapo ilitokea “*siku sita kabla ya Pasaka*” (**Yoh 12:1**), ambapo njama za makuhani wakuu na waandishi anazoelezea Marko katika **mst. 1** zilifanyika “*siku mbili kabla ya Pasaka*.” Bila shaka Marko alitumia utaratibu huu “kuchanganya” kupakwa mafuta kwa Yesu “*kwa maziko*” (**mst. 8**) kati ya njama za makuhani wakuu na waandishi kumkamata Yesu na kumuua (**mst. 1-2**) na Yuda Iskariote kukubaliana na makuhani wakuu kumsaliti Yesu (**mst. 10-11**). Pili, Simoni mkoma kwa namna fulani alikuwa na uhusiano na Mariamu, Martha, na Lazaro, kwa kuwa Yoh anaelezea tena kwamba walikuwepo pale na Mariamu alikuwa akiwahudumia chakula cha jioni (**Yohan 12:1-2**). Tatu, Yoh pia anambainisha mwanamke aliyempaka Yesu mafuta kuwa ni Mariamu, dada yake Martha na Lazaro (**Yoh 12:3**). Nne, wakati Marko anasema tu kwamba “*walikuwepo baadhi yao*” waliokwazwa na marashi ya gharama kubwa namna hiyo kutumika kmpaka Yesu (**mst. 4-5**), Na Mathayo anasema kwamba “*wanafunzi*” walikwazika (**Mat 26:8-9**), Yoh anabainisha kwamba Yuda Iskariote alitoa sauti ya kukwazwa kwake kwasababu alikuwa mwizi aliyejichukulia kutoka katika mfuko wa fedha (**Yoh 12:4-6**).

Hii inaonekana ni kupakwa mafuta pekee kulikofanyiwa mwili wa Yesu kabla ya kuzikwa. Marko anaeleza kwamba Yusufu wa Arimathaya alipewa mwili, akauzinga na kitambaa cha Hariri, na kuuweka katika kaburi lake (**Marko 15:43-46**; angalia pia **Luka 23:50-54**). Hata hivyo, inadhaniwa kwasababu ya siku ilikuwa imeenda sana, hapakuwa na chochote kilichoonekana kuwa kingefanyika katika kuupaka mwili marashi, ingawa Yoh anasema kwamba “*Nicodemo pia, ambaye awali alikuwa amemjia Yesu usiku, alikuja akiwa amebeba mchanganyiko wa marhamu na marashi mengine, karibu uzito wa paundi sabini na tano*. *Hivyo waliuchukua mwili wa Yesu na kuufunga katika nguo ya kitani pamoja na viungo, kulingana na desturi za kiyahudi.*” (**Yoh 19:39-40**). Kwamba mwili wa Yesu haukuwa “umepakwa mafuta” wakati wa kuzikwa inaonekana kuthibitishwa na ukweli kwamba “⁵⁵*Na wale wanawake waliokuja naye toka Galilaya walifuata, wakalionna kaburi, na jinsi mwili wake ulivyowekwa.*” ⁵⁶*Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. Na siku ya sabato walistarehe kama ilivyoamriwa.* ⁵⁷*Hata siku ya kwanza ya juma, ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini, wakiyaleta manukato waliyoweke tayari.* ⁵⁸*Wakalikuta lile jiwe limevingirishwa mbali na kaburi,* ⁵⁹*Wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu.*” (**Luka 23:55-24:3**)

Yesu alisema mambo mawili kuhusu kile alichokuwa amefanya Mariamu: “*Amefanya jambo jema kwangu*” (**mst. 6**) na “*Amefanya kile alichoweza*” (**mst. 8**). matamko yote yana maana muhimu kwetu. Yesu Bwana wetu. Kila kitu tunachofanya kinapaswa kiwe ni kwa utukufu wake. Kama Paulo anavyosema katika **1 Kor 6:19-20**, “*Ninyi si mali yenu wenyewe, maana tulinunuliwa kwa gharama. Basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu*” (angalia pia **1 Kor 10:31**). Zaidi ya hayo, hata kama Yesu amepaa kurudi kwa Baba, kanisani mwili wake hapa duniani (**Rum 12:4-5; 1 Kor 10:17; 12:12-27; Ef 1:22-23; 2:16; 3:6; 4:4, 12, 15-16; 5:23, 30; Kol 1:18, 24; 2:19; 3:15**). Matokeo yake, kwa kuwasaidia ndugu zetu wa kike na wa kiume katika Kristo, tunamfanya Yesu jambo zuri sana. Paulo anaeleza kwa ufupia, “*Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio.*” (**Gal 6:10**). Kadhalika, Mariamu alifanya “*kile alichoweza*.” Siyo yeye au sisi tunaweza kufanya kila kitu, lakini wote tunaweza kufanya kitu fulani. Mjane katika **Luka 21:1-4** hakuweza kutoa zaidi, lakini alitoa “*kile alichoweza*.” Kwa namna hiyo, marashi yale yalikuwa ya ghali sana (kama dinari 300 ambazo zingeliweza kuwa mshahara wa mwaka mzima wa) na bado, kama mjane, Mariamu aliitoa yote, kwasababu alimpenda Yesu, na kuliko kukaa nayo kwa matumizi yake binafsi. Tumeitwa kufanya kile tunachoweza kufanya—siyo kile ambacho hatuwezi kufanya—kuonesha upendo kwa wengine, kujenga ufalme, na kumheshimu Yesu katika maisha yetu. Tunahitaji kujiuliza, “Tunafanya tunachoweza kufanya?”

Katika **mst. 5-8** malalamiko yalikuwa kwamba “*marashi haya yangeweza kuuzwa kwa zaidi ya*

*dinari mia tatu na wapewe maskini.” Na walimkemea. lakini Yesu akasema, “mwacheni. kwanini mnamsumbua? amenifanyia jambo jema. kwa kuwa maskini mnao siku zote, na wakati wowote mkitaka mwaweza kuwatendea mema. Lakini mimi hamtakuwa nami siku zote.” Rejea ya Yesu kwa maskini mara zote wapo nasi ni nukuu kutoka katika **Kumb 15:11**. Kwa kunukuu kumbukumbu la Torati, Yesu hakumaanisha kwamba tunapaswa kuukubali umaskini kama kitu kisichoepukika na kwahiyo hatuwezi kukifanyia chochote. Alikuwa akisema kwamba, katika ulimwengu ulioanguka mara zote watakuwepo watakaokuwa na mahitaji; hakika, umasikini (kwa sababu mbalimbali) ni moja ya ishara za anguko. Hivyo, kama waamini tunaweza na tunapaswa kufanya “kile tunachowenza” kujaribu kupunguza umasikini mionganoni mwa watu na kuondoa sababu za umasikini. Lakini akimsifia Mariamu kwa zawadi yake kubwa na maneno yake kwamba “mara zote hamtakuwa nami,” wakati huo huo akisema, “wakati wowote mkitaka, mwaweza kuwatendea mema [masikini],” yanatufikisha kwenye matumizi ya kile alichosema awali kilikuwa ni amri mbili kuu kuliko zote: “Nawe utampenda Bwana Mungu wako kwa roho yako yote na kwa moyo wako wote na kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote [na] utampenda jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe” (**12:30-31**). Upendo wetu kwa Bwana utatupelekea kuwapenda jirani zetu, kwa kuwa jirani zetu wamefanywa kwa sura ya Mungu. Mariamu alikuwa amelenga kuonesha upendo kwa Bwana kwa namna ya moja kwa moja, kwasababu alikuwa na fursa ya kufanya hivyo ambayo sisi hatufanyi. Tuna fursa—wakati wote—kuonesha upendo wetu kwa Bwana kwa kuwapenda jirani zetu, kuwasaidia masikini, na kujenga ufalme wa Mungu kwa njia zingine.*

3. **mst. 10-11—Yuda anakubali kumsaliti Yesu**

Yuda alichukua hatua ya kumsaliti Yesu kwa pesa. Kama ilivyoonekana katika matukio mengine, Marko anatuonesha zito na la ulinganisho: Zawadi ya Mariamu ya upendo usio na kipimo na kujitoa, iliyomgharimi mshahara wa mwaka mzima dhidi ya Yuda—mmoja wa wanafunzi—anayemsaliti Yesu Bwana wake mwenyewe kwa vipande 30 vya fedha (**Mat 26:15**). Hii inaonesha unafiki wa Yuda kwa kulalamika kwamba “*marhamu hii ingeliweza kuuzwa kwa kwa zaidi ya dinari mia tatu na wapewe masikini*” (**mst. 5**). Kulikuwa na sarafu mbalimbali za fedha zilizokuwa kwenye mzunguko wakati huo, hivyo ni vigumu kuamua kuwa ni kiasi gani Yuda alilipwa. “Wanaotuongoza katika kupata alicholipwa Yuda ni swala la Antioch, shekel ya Tiro au tetradrachem ya Kiptolemai ya Misri. Kulingana nan i sarafu ipi iliyotumika, katika thamani ya leo ya fedha, sarafu hizi zilizo julikana zingeweza kuwa na thamani kati ya \$250 na \$300.” (“Professing Faith” 2016: n.p.)

Kuna zaidi katika usaliti huu kuliko mlinganisha wake na kujitoa kwa Mariamu. “Kinachofunuliwa zaidi na kusudi la mwandishi wa Mathayo. Maneno aliyotumia, ‘vipande vitatu vya fedha,’ ni kuturudisha nyuma kwa kitabu cha Zakaria. Katika Zakaria 11 maneno haya yametumika kumaanisha thamani ya mtumwa katika misingi ya sheria za Kiyahudi. Kutoka 21:32 inasema: ‘Ng’ombe akimtumbua mtumwa mume au kijakazi; mwenye ng’ombe atampa bwana wao shekeli thelathini za fedha, naye ng’ombe atauawa kwa kupigwa kwa mawe.’ Nabi Zakaria aliwataka Waisraeli umlipa kwa kazi aliyokuwa amefanya katikati yao, hicho ndicho walichompa. Ilimaanishwa kuwa ni dhihaka; hawakuwa wamethamini unabii wake. Yehova alimwambia Zakaria kuweka malipo haya ya mtumwa kwenye chombo cha hazina (mbele ya macho yao). Hivyo wakati Mathayo inasema vipande 30 vya fedha na Yuda kuvitupa katika chombo cha hazina [**Mat 27:5**], ni picha ya kisa hiki cha Zakaria ambako Wayahudi wasio waaminifu walishindwa kuona thamani ya nabii wa Bwana kwa kuilinganisha na kiasi cha pesa ya dhihaka – kilicho pima thamani ya mtumwa. Mathayo anasema makuhani walikuwa tayari kutokulipa chochote kwa Yesu. Walimkasirikia Yesu kwa tukio aliklokuwa ametenda hekaluni kwa kupindua meza za wakopesha fedha na kuwakemea makuhani kuchukua faida iliyotokana na dhabihu ambazo watu walinunua kutimiza wajibu wao kwa Mungu. Vipande 30 vya fedha kwa makuhani, kwa Mathayo, kwa Zakaria, kisha ikawa ndiyo bei ya dharau.” (Soldaat 2020: n.p.)

MASWALI YA KUJADILI

1. Fikiria jinsi Yesu alivyokabiliana na usaliti na kifo alichojua ni lazima. Kwa namna gani na nani alitumia siku kadhaa za mwisho duniani?
 - Hii inakuambia nini kuhusu tabia, asili na maadili?
 - Tunaweza kujifunza nini kutokana na hili?
2. Elezea asili, sifa na/au kanuni za utoaji ambazo mwanamke alizionesha katika **mst. 3**.

- Kati ya mambo yote ambayo Yesu alisema kuhusu mwanamke huyu katika **mst. 6-9**, ni maneno gani ungependa aseme kuhusu wewe (na kwanini)?
3. Yuda Iskariote, katika **mst. 10-11**, anaonekana kudanganywa na kisha kuingia kwenye udanganyifu, *udhaifu* wake mkuu (ulafi wake – angalia **Yoh 12:6**). Kwa upande mwingine, Petro, katika **mst. 66-72**, anaonekana kuwa amejaribiwa, na kushindwa, katika mahali ambapo alikuwa na *nguvu* nydingi kabisa (ujasiri wake – lingenisha na **Marko 14:29-31** na **Yoh 18:10**). Kuna chochote twaweza kujifunza kutohaka na haya?
- Umewahi kukabiliana na majoribu katika maeneo yako ambako una nguvu au udhaifu?
 - Ulifanya nini kukabiliana na changamoto kwa ushindi katika matukio hayo ambapu hukujiachia na kubebwa jaribu (na njia uliyotumia kusimama imara ilikuwa sawa katika changamoto zote zamaeneo ambayo una nguvu na yale ambayo ni dhaifu)?

14:12-31: ¹² *Hata siku ya kwanza ya mikate isiyochachwa, walipoichinja pasaka, wanafunzi wake wakamwambia, Ni wapi utakapo tuende tukuandalie uile pasaka?* ¹³ *Akatuma wawili katika wanafunzi wake, akawaambia, Nendeni zenu mjini; atakutana nanyi mwanamume amechukua mtungi wa maji; mfuateni;* ¹⁴ *na po pote atakapoingia, mwambieni mwenye nyumba, Mwalimu asema, Ki wapi chumba changu cha wageni, niile pasaka humo, pamoja na wanafunzi wangu?* ¹⁵ *Naye mwenyewe atawaonyesha orofa kubwa, imeandikwa tayari; humo tuandalieni.* ¹⁶ *Wanafunzi wakatoka, wakaenda mjini, wakaona kama alivyowaambia, wakaandaa pasaka.*

¹⁷ *Basi ilipokuwa jioni yuaja pamoja na wale Thenashara.* ¹⁸ *Nao walipokuwa wameketi chakulani, wakila, Yesu alisema, Amin, nawaambia, Mmoja wenu, naye anakula pamoja nami, atanisaliti.* ¹⁹ *Wakaanza kuhuzunika, wakamwambia mmoja mmoja, Je! Ni mimi?* ²⁰ *Akawaambia, Ni mmoja wa hao Thenashara, ambaye achovya pamoja nami katika kombe.* ²¹ *Kwa maana Mwana wa Adamu aenda zake kama alivyoandikiwa; lakini ole wake mtu yule ambaye amsaliti Mwana wa Adamu; ingekuwa heri kwake mtu yule kama asingalizaliwa.*

²² *Nao walipokuwa wakila, alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa, akasema, Twaeni; huu ndio mwili wangu.* ²³ *Akatwaa kikombe, akashukuru, akawapa; wakakinywea wote.* ²⁴ *Akawaambia, Hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi.* ²⁵ *Amin, nawaambia ninyi, Sitakunywa tena kabisa uzao wa mzabibu, hata siku ile nitakapounywa mpya katika ufalme wa Mungu.*

²⁶ *Nao walipokwisha kuimba walitoka kwenda mlima wa Mizeituni.* ²⁷ *Yesu akawaambia, Mtakunguwazwa ninyi nyote kwa ajili yangu usiku huu; kwa kuwa imeandikwa, Nitampiga mchungaji, na kondoo watatawanyika.* ²⁸ *Lakini baada ya kufufuka kwangu, nitawatangulia kwenda Galilaya.* ²⁹ *Petro akamwambia, Hata wajapokunguwazwa wote, lakini siyo mimi.* ³⁰ *Yesu akamwambia, Amin, nakuambia wewe, Leo, usiku huu, kabla ya kuwika jogoo mara mbili, utanikana mara tatu.* ³¹ *Naye akazidi sana kusema, Ijaponipasa kufa nawe, hata hivyo sitakukana kamwe. Na wote wakasema vile vile.*

mst. 12-31—Chakula cha mwisho cha jioni

Chakula cha mwisho cha jioni kinahusisha matukio kadhaa: maandalizi; Pasaka; chakula chenyewe; Yesu kutabiri kusalitiwa kwake na wanafunzi kuhojiana wao kwa wao; kutangazwa kwa Agano Jipy; unabii wa kupigwa mchungaji na kutawanyika kwa kondoo; na Yesu kumwambia Petro kwamba atamkana mara tatu usiku ule.

1. mst. 12-16—Maandalizi ya chakula cha mwisho cha jioni

Misatari hii inaonesha kwamba Yesu alikuwa ameshapanga na yule mtu aliyejkuwa anamiliki chakula cha juu ambako chakula cha mwisho cha jioni kingesherehekewa. Hili linadhihirishwa hivyo na ukweli kwamba huyo mtu atakuwa anabeba mtungi wa maji kama kitambulisho (**mst. 13**, wanawake kwa kawaida walibeba mitungi ya maji), swali allilowaambia wanafunzi waulize wakikutana naye (**mst. 14**), na ukweli kwamba “*atawaonesha chumba kikubwa ghorofani kikiwa kimeandalisha tayari*” (**mst. 15**). Hali hiyo inafanana na kumchukua punda ambaye Yesu alimpanda wakati kudhirisha ushindi akiingia Yerusalem (**11:1-6**).

2. mst. 16-18, 22-23, 26—Pasaka na chakula cha Pasaka

Inaleta maana kwamba chakula cha misyo cha jioni kilikuwa chakula cha Pasaka. Vyote, sherehe ya Kiyahudi ya Pasaka na chakula chenyewe vilikuwa nya kinabii na vilikamilishwa na Kristo. Pasaka ilisherehekeza ukombozi kutoka katika kifunga cha Wamisri (yaani, malaika wa Mungu wa kuua “aliwapita” Waisraeli). Mwana kondoo alichinjwa, damu yake ilinyunyizwa katika mimo ya milango ya nyumba, na kisha ilibankwa na kuliwa na wanafamilia (**Kut 12:1-13, 21-27; Law 23:5; Hes 28:16; Kumb 16:1-8**). Kutoka kulikuwa ndio msingi wa sherehe ya Pasaka (**Kut 12:1-27**). alikuwa anarejea kutoka kwa Israeli katika maisha yake mwenyewe; hata katika mlima aliko badilika sura alizungumzia “*kutoka*” kwake mwenyewe [neno la Kigiriki lililotafsiriwa “*kutoka*”] (**Luka 9:30-31**). AJ linamuunganisha Yesu na mwana kondoo wa Pasaka. Mwanzoni mwa huduma ya wazi ya Yesu Yoh mbatizaji alimtambua Yesu alikuwa nani na kumbainisha kama “*mwana kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu*” (**Yoh 1:29, 36**). Kwa utambulisho huu, Yoh alikuwa akiunganisha Pasaka (iliyohitaji dhabihu ya mwana kondoo) na siku ya upatanisho (ambapo dhambi za waisraeli zilifunika). Kumuunganisha Yesu na mwana kondoo wa dhabihu kunadhibitishwa tena katika **1 Pet 1:19; Ufu 5:6, 8**. Kristo alisulubiwa wakati wa Pasaka ambapo mwanakondoo wa Pasaka alichinjwa (**Luka 22:1; Yoh 19:14, 31**).⁶¹ AJ linasema kwamba Pasaka ilikuwa inatabiri dhabihu ya Kristo. **Yoh 19:36** ananukuu **Kut 12:46** na **Hes 9:12** (ambapo inanenwa kuwa mifupa ya mwanakondoo isivunjwe) na inasema, “*mambo haya* [yaani, askari kutokuvunja miguu ya Kristo kama walivyofanya kwa wale waliokuwa wamesulubiwa pamoja na Yesu] *yalitimiza maandiko, ‘hakuna mfupa wake utakaovunjwa.’*” **1 Kor 5:7** pia inasema, “*Kristo Pasaka wetu pia ametolewa.*”

Chakula chenyewe kilikuwa Pasaka ya ‘Seder’ (neno seder lina maana ya “utaratibu” kama utaratibu wa huduma) (Litvin and Litvin n.d.: 4). Injili tofauti zinatoa maelezo ya kina mbalimbali kuhusiana na chakula. Kwa mfano, Pasaka Seder ilihuisha kunywa vikombe vine nya mvinyo. **Luka 22:17-18** inarejea: “¹⁷*Akapokea kikombe, akashukuru, akasema, Twaeni hiki, mgawanye ninyi kwa ninyi;* ¹⁸*Maana nawaambia ya kwamba tangu sasa sinywi mazao ya mzabibu hata usalme wa Mungu utakapokuja.*” Kikombe cha kwanza kilifuatiwa na kunawishwa mikono na mwenyeji. Hata hivyo, badala ya kuosha mikono, Yesu “aliosha miguu ya wanafunzi wake. Alifanya hivyo ili kutoa funzo kwamba ‘aliye mkuu miongoni mwenu awe mtumishi wa wote.’” (Litvin na Litvin n.d.: 10; angalia **Yoh 13:4-17**) Baada ya kuosha, kila mshiriki alikuwa na mbogamboga ambazo alizichomva kwenye bakuli lenye maji ya chumvi. Hili linatajwa na katika **Mat 26:21-23**: “²¹*wangali wakiwa wanakula, akasema, amini, nawaambia, mmoja wenu atanisaliti,* “Wakati huo katikati ya chakula, Yeshua [Yesu] alimpa bakuli la chumvi Yuda ili achomvye mboga zake.

Ndipo bakuli lingeweza kuzungushwa mezani kwa kila mtu aliyeo mezani kama desturi. Sababu moja wanafunzi wengine hawakutambua kwamba aliyekuwa ametambulishwa ni Yuda Iskariote ni kwasababu wangeweza wote kuchomva mboga zao katika bakuli lile. Kuna kitu ambacho hakiko wazi hapa. Lakini . . . Yuda alikuwa ndiye pekee aliyekuwa amechomvya katika bakuli pamoja na Yeshua lilipokuwa limempitia kwa mara ya pili.” (Ibid.: 12) Baada ya kikombe cha pili cha mvinyo (kilichojuikana kama kikombe cha tauni) mchanganyiko wa matzah (mkate usiotiwa chachu) na horseradish [“kipande cha mkate na supu”] vililiwa. **Yoh 13:23-26** anarejea jambo hili: “*Na palikuwapo mmoja wa wanafunzi wake, ameegama kifuani pa Yesu, ambaye Yesu alimpenda.*”²⁴ *Basi Simoni Petro akampungia mkono, akamwambia, Uliza, ni nani amtajaye?* ²⁵ *Basi yeye, hali akimwelekea Yesu kifua chake, akamwambia, Bwana, ni nani?* ²⁶ *Basi Yesu akajibu, Ndiye mtu yule nitakayemtowelea tongue na kumpa. Akatowelea tongue, akalitwaa akampa Yuda, mwana wa Simoni Iskariote.*” Aidha, hata hivyo, kwa kuwa wengine wote walipokea kipande cha mkate kile kile kutoka kwa Yesu, bado hawakuelewa kuwa alikuwa anamzungumzia Yuda.

Pia kuna sherehe ambapo kunakuwepo kitambaa chenyewe mifuko mitatu. Kila mifuko kuna kipande cha matzah (mkate usiotiwa chachu). Kile cha katikati kinachukuliwa, kinamegwa, kinafungwa kwenye kitambaa cha Hariri, kisha kinafichwa (Ibid.: 13). Baada ya chakula kuliwa, mlo wenyewe ukishaliwa. Basi kinachofuata hilo, kile kipande cha katikati kinagunduliwa (na watoto kama wapo nyumbani) na kuletwa mezani. Kipande hiki ndicho mkate ule amba Yesu alisema, “*Chukueni, huu ni*

⁶¹ Ukristo wa Kiorthodox unashukilia kwamba Yesu alisulubiwa Ijumaa na kufufuka Jumapili asubuhi. Hata hivyo, kuna mabishano kuhusu ni *siku gani* ya *Kiebrania* ambayo pasaka ilifanyika (chakula cha kawaida cha Pasaka “kingaliweza kuanza mara tu baada ya jua kuzama siku ya Nisan lakini kingeliweza *kuendelea* hadi siku iliyofuata ya Nisan 15” [Parsons 2016b: ‘Passover at the Temple’]) na iwe kwamba Yesu alisulubiwa siku ya 14 au 15 ya Nisan (kumbuka kuwa siku za *Kiebrania* zinahusisha sehemu ya siku mbili za *Kirumi* kwasababu siku za *Kiebrania* zilianza wakati wa jua kuzama, na siyo katikati ya usiku, na kuendelea hadi jua kupunga siku iliyofuata). Michael Scheifler anaweka msingi wa chakula cha mwisho cha Bwana ndani ya Nisan 13-14 na Nissan 14 kama siku ya kusulubiwa (Scheifler n.d.: n.p.); Alfred Edersheim anaweka msingi kati ya Nisan 14-15 kama siku ya chakula cha mwisho na 15 kusulubiwa (Edersheim 1988: 244-59, 389-401).

mwili wangu" (**mst. 22**). Baada ya hapo, kikombe cha tatu cha mvinyo (kilichoitwa kikombe cha ukombozi) kinanyewa Hiki ndio kile kikombe Yesu alisema, "*Hii ni damu yangu ya agano, inayomwagwa kwa ajili ya wengi*" (**mst. 24**). Baada ya hapo, "Zaburi 113-1118 (zinazojulikana kwa ujumla wake kama Hallel) huimbwa na wale waliokusanyika kusherehekeea pasaka" (Ibid.: 33). **Mistari 26** unarejeo jambo hili: "*Nao walipokwisha kuimba walitoka kwenda mlima wa Mizeituni.*"

Kisa hiki hakiishii hapa. Wakati wa chakula kile cha jioni Yesu alianzisha *Pasaka mpya*—Chakula cha Bwana (**Mat 26:20-29; Marko 14:12-25; Luka 22:1-22; Yoh 13:1-2; 1 Kor 11:23-32**). Pasaka mpya, kama inavyowakilishwa na Chakula cha Bwana, ni ukombozi wetu, siyo kutoka utumwani misri, lakini kutoka katika utumwa wa dhambi, kwa msingi wa kile Kristo alichotutendea katika mwili na damu yake. Bretscher (1954: 199-209) anaorodhesha mambo ya kulinganishwa 11 katika ya Pasaka ya asili/ mkate usiotiwa chachu na Chakula cha Bwana:

- *Sherehe zote ziliagizwa na Mungu (Kut 12:1; 1 Kor 11:23).*
- *Sherehe zote zilihusu dhabihu ya mwanakondoo (Kut 12:3; 1 Kor 5:7).*
- *Kwa kila mojawapo mwanakondoo alipaswa kuwa asiwe na mawaa (Kut 12:5; 1 Pet 1:19).*
- *Kila sherehe hakuna mfupa wa mwanakondoo wa dhabihu ulivunjwa (Kut 12:46; Yoh 19:31-36).*
- *Katika kila sherehe ni kwa kula nyama ya mwanakondoo wa dhabihu ndiko kulikoleta faida kwa washiriki wa dhabihu na kibinasi kupokea Baraka yake (Kut 12:47; Yoh 6:52-57; 1 Kor 10:18; Mat 26:26; Marko 14:22; Luka 22:17-19; 1 Kor 11:24).*
- *Katika kila sherehe damu iliyomwagwa ilikushika nafasi muhimu ya sherehe.* Katika Pasaka damu ya mwanakondoo iliwekwa katika miimo ya milango ya nyumba (**Kut 12:7, 22**); Katika chakula cha Bwana damu ilikuwa sehemu ya sherehe yenye matokeo, kwasababu haina mipaka kwa kuwaokoa wanaoshiriki kimwili tu bali mwili na roho kwa uzima wa milele (angalia **Mat 10:28**).
- *Sherehe zote zimetolewa kama kumbukumbu kusherehekewa na vizazi na vizazi.* Pasaka ni kumbukizi ya ukombozi wa Israeli kutoka Misri (**Kut 12:14, 24-27**). Chakula cha Bwana ni kumbukizi ya Kristo ambaye katika kifo chake, "*alichukua dhambi ya ulimwengu*" (**1 Kor 11:25-26**).
- *Sherehe zote zinataka imani.* Utii wa Waisraeli kwa Mungu wakati wa Pasaka ulidhihirisha imani yao na kumtegemea katika yale aliyosema (**Kut 12:27-28**) na hivyo akawaokoa na mauti. Katika chakula cha Bwana, washiriki kadhalika lazima wajichunguze wenyewe na kushiriki chakula kwa namna inayostahili; kushindwa kufanya hivyo kunapelekeea katika hukumu, hata kufa (**1 Kor 11:27-32**).
- *Damu halisi ilitumika katika sherehe zote, lakini damu iliyotumika katika chakula cha Bwana ina uendelevu, thamani ya ndani na nguvu, wakati damu iliyotumika katika Pasaka haina vitu hivyo.* Damu ya mwanakondoo katika pasaka ilikuwa ni "ishara" tu kwamba Mungu angeangalia wakati malaika wake wa mauti atakapokuwa akipita Misri lakini haikuwa na nguvu ya ndani yake ya kuweza kumuokoa mwanadamu mwenyewe (**Kut 12:13**). Kwa upande mwingine, damu ya Yesu ambayo ilitumika katika chakula cha Bwana ni damu ya Mwana wa Mungu, ambayo peke yake ina nguvu na inatosha "*kuchukua dhambi za ulimwengu*" (**Mat 26:28**). Hivyo, Yesu angweza kusema, "*Hili . . . ni agano jipyka katika damu yangu*" (**Luka 22:20**), siyo tu kwamba damu yake ilikuwa "ishara" ya agano jipyka.
- *Sherehe zote ni za kipekee.* Pasaka ilikuwa ni kwa Waembrania tu; asiyekuwa mwisraeli alilazimika kutahiriwa ili aweze kushiriki (**Kut 12:43-45**). Chakula cha Bwana ni kwa ajili ya mwili wa Kristo (**1 Kor 10:16-17, 20-21**). Ni kwa njia ya dhabihu ya Yesu kwamba Waisraeli, na yelete yule ambaye "atakula mwili wake na kuinywa damu yake," anakuwa huru kutoka utumwani—jambo ambalo Yesu na sehemu yote ya Agano jipyka inafundisha (angalia **Yoh 8:31-36; Rum 6:1-23; Ebr 2:14-15**).

Mwishi, Kama Pasaka ilivyokuwa ishara wakilishi na ya kinabii, kadhalika chakula cha Bwana. "Kuanzishwa kwa chakula cha Bwana kunadai kwamba hali ambayo kanisa linapita katika historia hajafikia ukomo wake. Chakula cha mwishi chenyewe ni namna ya unabii unaojitegemea, namna ambayo inaashiria sherehe ya mbeleni ambayo Kristo atasherehekeea na wanafunzi wake katika ufalme wa Mungu (Luka 22:15-18; Marko 14:25; Mat 26:29; 1 Kor 11:26). Kwahiylo, kila chakula cha Bwana kinaposherehekewa na kanisa kinaashiria ukomo ujao (Rev 21:2ff.)." (Goppelt 1982: 116)

3. **mst. 17-21—Unabii wa Yesu wa Kusalitiwa na wanafunzi kuhojiana wao kwa wao**

Utabiri wa Yesu kuhusu kusalitiwa kwake na mmoja wa wale kumi na wawili katika **mst. 18** ni rejea ya **Zab 41:9**. Kama maelezo ya Litvin kuhusu utaratibu wa wa chakula cha Pasaka ndicho kilichofuatwa na Yesu na wanafunzi, **mst. 20** ("*Ni mmoja wa hao Thenashara, ambaye achovya pamoja*

nami katika kombe") yanaonekana kurejea chakula cha **Yoh 13:26** kilicholiwa baada ya kikombe cha pili cha mvinyo (angalia hapo juu). Maswali ya kujiuliza ya wanafunzi ("ni mimi?," mst. **19**) ni hali nzuri ya kutokujiamini na kutambua nguvu dhambi ndani mwetu sote (angalia **Rum 7:14-24**). Kujiuliza kama huko ni kuzuri kuliko kujisifia ambako wote walionesha baadaye (angalia **mst. 29, 31**). **Mst.ari wa 21** ("*Mwana wa adamu yu aenda kama alivyoandikiwa*") huenda unarejea **Isaya 53**. Pamoja na kwamba kusalitiwa na kufa kwa Yesu kulisha pangwa kabla (**Isa 53:10-12; Mdo 2:23; 4:27-28**), Yuda anawajibika na atatoa hesabu kwa usaliti wake.⁶²

4. mst. 22-25—Kutangazwa kwa agano jipya

Yer 31:31-34 alikuwa ameahidi Agano Jipy "na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda." Agano jipya litakuwa agano la milele ambako Mungu ataandika sheria yake katika miyo yao, watu wake hasa watamjua Bwana viliyyo, naye atawasamehe dhambi zao na hatazikumbuka tena (angalia pia **Yer 32:38-40; 50:4-5; Ezek 11:14-20; 36:24-32; 37:15-28**). Hapo nyuma Yesu alikuwa amesema kuwa alikuwa "mkate wa uzima" (**Yoh 6:35, 48**). Sasa katika chakula cha mwisho anaashiria kwamba kwa kuutwaa mkate, akisema "huu ni mwili wangu" (**mst. 22**). Anaweka wazi kwamba alikuwa anazindua Agano Jipy kwa damu yake (**Luka 22:20**; ona **1 Kor 11:25**). Yesu alisema, "Hii ni damu ya agano" (**mst. 24; Mat 26:28**). Ni mwangwi wa maneno ya Musa katika **Kut 24:8**. agano la Musa halikusamehe dhambi au kutoa uzima wa milele; Agano Jipy, ambalo Yesu anazindua katika damu yake, linasamehe dhambi na kutoa uzima wa milele. Agano lilithibitishwa na kuhitimishwa pale msalabani (**Ebr 9:12-17**). Likathibitika wakati Yesu alipofufuka kutoka kwa wafu, kisha akapaa mbinguni na kukaa katika enzi na Baba. (**Ebr 10:11-18**). "Upya" wa Agano Jipy unaonekana katika "kuhusiasha dhabihu ambayo itaondoa dhambi [**Ebr 9:12-14**], hekalu jipya ambalo halijafanywa na mikono ya watu [**Ebr 9:11**], ukuhani mpya unatoka katika kila kabilna taifa [**1 Pet 2:5; Ufu 1:6; 5:9; 7:9**], na watu wapya wa Mungu waliozaliwa kutoka juu kwa Roho [**Yoh 3:3; 2 Kor 5:17**]. Kwahiyu, Kristo, ndiye kinyume cha Adamu, kichwa cha kizazi chote kipywa na utaratibu mpya wa dunia, uliostawishia kwa misingi ya kazi yake ya kuokoa (cf. Rum. 5:12-25)." (Smith 1999b: ch. 13) "Yeye siyo mpatanishi tu wa Agano Jipy la Mungu; ndiye aliyefanyika agano jipya" (Goppelt 1982: 116).

Yesu kurejea kuhusu damu yake "kumwagwa kwa ajili ya wengi" (**mst. 24**) inarejea **Isa 53:12** na ni mwangwi wa kile alichosema katika **Mat 20:28** ("mwana wa Adamu ahakuja kutumikiwa bali kutumikia, na kuutoa uhai wake kama fidia ya wengi"). **Mistari 25** unaonesha kuwa chakula cha Bwana hakitaondolewa wakati wa kilele cha ufalme wa Mungu, kwasababu kitatimizwa tena katika chakula cha ndoa ya mwanakondoo (**Ufu 19:7-9**) Hatimaye, chakula cha Bwana lazima kisherehekewe leo "kama ukumbusho wa kweli mbili muhimu: *shangwe* ya wokovu wetu ambao tayari tumeshauapata na *tumaini* la kurudi kwa Yesu mara ya pili na ushirika wetu naye milele" (Cole 2006: 1196).

5. mst. 26-31—Unabii wa kupigwa kwa mchungaji na kutawanyika kwa kondoo, na kukana kwa Petro

Katika **mst. 27**, Yesu anatabiri kuwa wanafunzi wake wote watarudi nyuma. Katika hili, ananukuu **Zak 13:7** na kulihusisha na yeye mwenyewe. Nukuu ya Yesu kutoka kwa Zakaria ilikuwa ya makusudi, kuwa muktadha wa **Zakaria 13** unaonesha kwamba Mungu yuko nyuma ya temdo la kupigwa kwa mchungaji na kutawanyika kwa kondoo (angalia pia **Isa 53:10**).⁶³ Kutawanyika ni kupitia changamoto, kujaribiwa, na kuwatakasa kondoo (**Zak 13:8-9**)—na hilo ndilo lililotokea kwa wanafunzi. Unabii wa ulikuwa umetimizwa alipokamatwa (**mst. 50**, "Na wote wakamuacha na kukimbia"). Unabii wa kukana kwa Petro ultimizwa katika **mst. 66-72**.

MASWALI YA KUJADILI

1. Angalia mlinganisho kati ya mwitikio wa mashaka wa wanafunzi au kuulizwa kwa swali katika **mst. 19** na kujishuku katika **mst. 31**. ambao ulikuwa ni mwitikio mzuri au sahihi kuwa nao, na kwanini?
 - Tunaweza kujuunza nini kutokana na hili?
2. Katika chakula cha mwisho, Yesu alitwaa vile vitu vya chakula cha Pasaka na kuviwekea maana mpya

⁶² Swala la ukuu wa Mungu, uwajibikaji wa mwanadamu, na uwepo wa dhambi na uovu vimejadiliwa kwa kina katika Menn 2021: 108-32.

⁶³ "Mtumishi katika Isaya 53 na mchungaji katika Zak. 13 vina mengi ya kufanana. Wote wanateseka kwasababu ilikuwa ni mapenzi ya Bwana iwe hivyo. Wote wanapitia kwenye uzoefu wa kufa kimakosa na kuamsha huzuni na wasiwasi mionganoni mwa watu kwa makosa yaliyotendwa kwao. Muhimu zaidi, wote wanateseka ili kuleta utakaso wa dhambi." (Klein 2008: 389)

(au, labda kwa usahihi, alionesa vilikuwa vimekusudiwa kubeba maana gani tangu mwanzo). Katika **mst. 22-25** alizindua Agano Jipywa ambalo lilikuwa limetabiriwa na Yeremia (**Yer 31:31-34**; angalia pia **Ezek 36:25-27; Luka 22:20; 2 Kor 3:2-6; Ebr 8-9**), hivyo kulifanya Agano la Kale kuwa kitu kilicho pitwa na wakati (**Ebr 8:13**). Hili “Agano Jipywa” ni nini, na sifa zake muhimu ni zipi?

3. Kwanini Ushirika uwe (au unapaswa kuwa) sehemu muhimu ya maisha ya kanisa na maisha binafsi ya mkristo?

- Imekuwa hivyo kwako? Kama sivyo, ni kwa namna gani unaweza kushika nafasi yake sahihi katika moyo na maisha yako?

14:32-42:³² *Kisha wakaja mpaka bustani iitwayo Gethsemane; akawaambia wanafunzi wake, Ketini hapa muda niombapo.*³³ *Akamtwaa Petro na Yakobo na Yoh pamoja naye, akaanza kufadhaika sana na kuhangaika.*³⁴ *Akawaambia, Roho yangu ina huzuni nyangi kiasi cha kufa; kaeni hapa mkeshe.*
³⁵ *Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akiomba ya kuwa, ikiwezekana, saa hiyo imwepuke.*
³⁶ *Akasema, Aba, Baba, yote yavezekana kwako; uniondolee kikombe hiki; walakini, si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe.*³⁷ *Akaja akawakuta wamelala usingizi, akamwambia Petro, Je! Simoni, umelala? Hukuweza kukesha saa moja?*³⁸ *Kesheni mwombe, msije mkaingia majaribuni, roho i radhi ila mwili ni dhaifu.*³⁹ *Akaenda zake tena, akaomba, akisema neno lilo hilo.*⁴⁰ *Akaja tena akawakuta wamelala, maana macho yao yamekuwa mazito, wala hawakujua la kumjibu.*⁴¹ *Akaja mara ya tatu, akawaambia, Laleni sasa, mpumzike; yatosha, saa imekuja; tazama, Mwana wa Adamu anatiwa mikononi mwao wenyewe dhambi.*⁴² *Ondokeni, twendeni zetu; tazama, yule anayenisaliti amekaribia.*

mst. 32-42—Katika Bustani ya Gethsemane

Pale bustanini, Kristo “*alifadhaika na kuhangaika*” (**mst. 33**), na roho yake “*ikashikwa na huzuni kiasi cha kufa*” (**mst. 34**). **Luka 22:44** anaongeza, “*Naye kwa vile alivyokuwa katika dhiki, akazidi sana kuomba; hari yake ikawa kama matone ya damu yakidondoka nchini.*” Kuhangaika kwake na maumivu yalikuwa makali kiasi kwamba aliomba, “*Abba, Baba, yote yavezekana kwako; uniondolee kikombe hiki; walakini, si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe*” (**mst. 36**). Ni wazi kikombe ndicho alikuwa anakwenda kukinywea siku iliyofuata msalabani. Ingawa katika ngazi ya kimwili kusulubiwa kulikuwa kunatekelezwa taratibi, kwa maumivu makali, na kudhalilisha, haya hayahesabiwi katika ngazi ya kuhangaika kwake. Badala yake, “*kikombe*” alichokuwa anaenda kukinywa kilikuwa ni kikombe cha ghadhabu ya Mungu (angalia **Zab 75:8**). Yeye ambaye “*hakujuwa dhambi*” alifanywa “*kuwa dhambi*” kwa ajili yetu (**2 Kor 5:21**). Haiwezekani kwetu, ambao nguvu ya dhambi inakaa ndani mwetu kuelewa asili ya kile Kristo alichojibebesa mwenyewe. Kufanyika kwake dhambi kwa ajili yetu kulilazimisha kukinywea kikombe cha ghadhabu ya Mungu jambo amablo lina maana kuwa Baba—katika mahusiano makamilifu ya kuwa kitu kimoja katika upendo—anamuacha.⁶⁴ Tena, haiwezekani kwetu kuelewa kina cha maana ya hayo yote. Alichokuwa akifanya Yesu pale msalabani ilikuwa ni kupokea hukumu, kulipa gharama, na kujitwisha adhabu ilioletwa na wanadamu: “*Katika Mathayo 10:28 Yesu anasema kwamba hakuna uharibifu unaoweza kulinganishwa na uharibifu wa kiroho kuzimu, wa kupoteza uwepo wa Mungu. Lakini hili hasa ndilo lililotokea kwa Yesu msalabani – aliachwa na Baba (Mathayo 27:46).* . . . Alipopaza sauti kwamba Mungu wake amemuacha alikuwa anapitia matezo ya kuzimu. Lakini fikia—kama deni letu la dhambi ni kubwa kwamba kamwe halilipiki pale, bali kuzimu yetu inaendelea hadi milele, sas tutakuwa na nini cha kuhitimisha kutoka katika uhalisia kwamba Yesu alisema malipo ‘yalikamilika’ (Yoh 19:30) aada ya masaa matatu tu? Tunajifunza kwamba kile alichohisi msalabani kilikuwa kibaya na cha kina kuliko kuzumu zetu wote zikiwekwa pamoja. . . . Yesu alipotenganishwa na Mungu aliingia katika shimo refu mno na kwenye moto mkali mno, kuliko tunavyowenza kufikiri. Alikutana na ghadhabu kamili ya Baba. Na alifanya hivyo kwa kujitolea, kwa ajili yetu.” (Keller 2009: sec.4)

Pale bustanini, “Mungu Baba aliachia kikombe kama kilivyokuwa kimepangwa, ali akinywee.

⁶⁴ Kina cha urafiki wa karibu na Baba kinaakisiwa katika ukweli kwamba Yesu alizungumza na Baba moja kwa moja, akitumia neno la Kiaramaiki “*Abba*” neno la urafiki wa kibinagsi wa karibu (**mst. 36**). ijapo kuna nyakati za kipekee zinazotokea kwa nadra kwa Wayahudi wengine *zinazomwelezea* Mungu kama Abba, “hatuna ushahidi wa wengine kabla ya Yesu waliowahi kumuita Mungu Abba” (Bauckham 1978: 249, mkazo umeongezewa). “Kwa uchache wake katika kutumia Abba kulimuweka katika daraja la mtu mtakatifu anayefurahia kiwango cha juu cha urafiki wa karibu na wa kipekee na Mungu, na kwa shida tunaweza kuelezea matumizi haya isipokuwa kama yanavyoakisiwa kufahamu kwake kuhusu urafiki huu wa kipekee wa karibu” (Ibid.: 248).

... Alikuwa na mtazamo wa karibu wa tanuru la ghadhabu, ambako ilipaswa atupwe; aliletwa kwenye mdomo wa tanuru ili alichungulie, na asimame hapo akiangalia hasira ya miali yake, na aone mwako wa joto lake, ili ajue kwamba anakokwenda na mateso anayoyakaribia. Hii ilikuwa jambo ambalo lilijaza nafsi yake huzuni na giza, muonekano huu wa kutisha ulimmaliza kabisa." (Edwards 1739: n.p.) Jonathan Edwards anaelezea kwanini hii hali ya utangulizi wa kikombe ilikuwa ni ya lazima: "Kama asili ya kibinadamu ya Yesu isingekuwa imewekwa wazi kwa namna isiyo ya kawaida kuhusu mateso atakayokutana nayo, asingeweza, kama mtu, kujua kikamilifu kabla ya mateso aliyokuwa anakwenda kukabiliana nayo, na hivyo kama mtu asingejua kikamilifu kile atakachokuwa ametenda wakati wa kuchukua kikombe na kukinywea, kwasababu angekuwa hajui kikombe kilimaanisha nini–kikiwa ni kikombe ambacho hajawahi kukinywea kabla. Kama Kristo angekuwa amejiingiza mwenyewe katika mateso hayo, bila kufikiria mbele kikamilifu, lazima awe hakujuwa kitakachomtokea. Kama mtu, angeweza kujiringiza mwenyewe kwenye mateso ya kiasi hicho kama angekuwa hayajui, kwahiyio aliiingia kama kipofu; na kujichukulia mateso haya kusingekuwa tendo lake mwenyewe. Kristo, kama Mungu, kwa hakika alijua haya mateso yalikuwa yanabeba nini; lakini pia ajitambue kama kama mtu; kwakuwa alikuwa anakwenda kuteseka kama mtu, na tendo la Kristo katika kukinywea kikombe likuwa ni tendo la Mungu mtu. . . . Kristi alikuwa akienda kutupwa katika tanuru la moto mbaya kabisa wa ghadhabu ya Mungu, na ilikuwa si sawa kwamba ajitupe humo kama kipofu, kama hajui makali ya tanuru. Kwahiyio, ili asifanye hivyo, Mungu alimleta karibu kabisa na mdomo wa tanuru, ili achungulie humo, na aangalie ukali wake na ghadhabu ya mwako wa miali yake, na kuona ni wapi anakokwenda, na kwa hiari aingie humo na kustahimili kwa ajili ya wenye dhambi, akijua alikuwa nani. mtazamo huo Kristo alikuwa nao katika kuugua kwake." (Edwards 1739: n.p.; angalia pia Cole 2006: 1197).

Maana ya "Gethsemane" ni "shinikizo la kukamulia mafuta" (Vander Lann and Markham 1996: 160). Pale bustanini, "wakati Yesu akiwa anabeba uzito wa kile kilichomaanisha kuwa mwanakondoo wa Mungu na dhabihu ya dhambi ya dunia, matone ya damu yake ya upako yalianza kumtoka, kama mafuta ya thamani kubwa yanapokamuliwa kutoka kwa mzeituni. Yesu kwa hiari yake aliiingiza katika maumivu mabaya kama hayo kuonesha uzito wa upendo wake. Uhitaji wetu ulimuingiza huko na kumuweka katika bustani ya kifo cha kujitolea kama dhabihu." (Ibid.) Kwa nuru ya haya yote, maombi yake, "*walakini, si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe*" (**mst. 36**) yote hayo siyo ya kawaida. Hiyo inapaswa kuwa ndiyo nia ya kila mkristo, hasa kwa kuwa "kwasababu alikamuliwa kwa ajili yetu, hatutahitaji tena kubeba uzito wa adhabu kwa ajili ya dhambi zetu" (Ibid.).

Ukichukulia mahangaiko makubwa ya Yesu, na hata wosia wake aliourudia kwa Petro, Yakobo na Yoh wa "*kesheni na kuomba*" (**mst. 34, 38**), inashangaza kwamba wote watatu walilala wakati amba Bwana wao aliwhahitaji kuliko wakati mwingine. Ombi la "*Kesheni na kuomba*" linawahusu waamini wote, Hasa wanapokabiliana na majoribu na mateso. Hatuwezi kutegemea ukweli kwamba roho yetu I radhi, kwa kuwa mwili wetu ni dhaifu sana na unaweza kupotoshwa kwa urahisi. Mwili wetu unakuwa na nguvu tu unapokuwa umewekwa chini ya Roho Mtakatifu. Hilo linaweza kutokea bila kujali nguvu ya mwili au udhaifu. Mwili wetu ni mahali pa majoribio ya dhamira yetu na imani yetu. Ni maisha tu yaliyobeba tabia ya kukesha na maombi yatakayoweza kututunza ndani ya uaminifu na kutuepusha na tusiangukie dhambini.

Maneno ya mwisho ya Yesu kuhusu "*kusalitiwa na kukamatishwa kwa mikono ya wenye dhambi*" (**mst. 41**) una mguso mkubwa zaidi kuliko unavyoweza kuonekana. Ukweli ni kwamba, kiuhalisia kuna aina mbili tu za watu: wenye dhambi na watakatifu. Watu wengi, kama Yuda, wanaweza kutumia miaka yao wakiwa na Yesu na bado kumbe ni wenye dhambi. Ni lazima "tukeshe na kuomba" hao siyo sisi.

MASWALI YA KUJADILI

1. Maombi ya Yesu katika Bustani ya Getsemane yana maana kubwa sana. Kwa nini ni muhimu kwa madai ya Ukristo kuwa njia *pekee* ya kumfikia Mungu na wokovu?

- Mungu alithhibitishajekuwa Yesu ndiye njia *pekee* ya kumfikia Mungu na wokovu?

2. Ni kwa namna gani maneno yale yale, "*, si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe,*" yanaweza kuwa dalili ya ama *uaminifu* au *kutokuamini*?

3. Katika **mst. 38**, wakati Yesu aliposema kwamba "*roho I radhi, lakini mwili ni dhaifu,*" alimaanisha "*udhaifu katika mambo ya Mungu na Roho.*" Angaliweza pia kusema kwamba "*roho I radhi, lakini mwili una nguvu [yaani, una nguvu katika dunia na mambo ya mwili].*" Ni kwa namna gani yeoyote anaweza kuwa na nguvu katika mambo ya Mungu na Roho, na kuwa dhaifu katika mambo ya dunia na mwili?

14:43–15:20a:⁴³ *Basi alipokuwa katika kusema, mara Yuda alifika, mmoja wa wale Thenashara, na pamoja naye mkutano, wana panga na marungu, wametoka kwa wakuu wa makuhani, na waandishi, na wazee.*⁴⁴ *Na yule anayemsaliti alikuwa amewapa ishara, akisema, Nitakayembusu, huyo ndiye; mkamateni, mkamchukue salama.*⁴⁵ *Basi alipokuja, mara akamwendea, akasema, Rabi, akambusu.*
46 *Wakanyosha mikono yao wakamkamata.*⁴⁷ *Na mmoja wao waliokuwapo akafuta upanga, akampiga mtumwa wa Kuhani Mkuu, akamkata sikio.*⁴⁸ *Yesu akajibu, akawaambia, Je! Ni kama juu ya mnyang'anyi mmetoka wenye panga na marungu, kunitwaa mimi?*⁴⁹ *Kila siku nalikuwa mbele yenu hekaluni nikifundisha, msinikamate; lakini haya yamekuwa ili maandiko yapate kutimia.*⁵⁰ *Ndipo wakamwacha, wakakimbia wote.*⁵¹ *Na kijana mmoja alimfuata, amejitanda mwili wake nguo ya kitani; wakamkamata;*⁵² *naye akaiacha ile nguo ya kitani, akakimbia yu uchi.*

⁵³ *Nao wakamchukua Yesu kwa Kuhani Mkuu; wakamkusanyikia wote, wakuu wa makuhani na wazee na waandishi.*⁵⁴ *Naye Petro akamfuata kwa mbali, hata ndani katika behewa ya Kuhani Mkuu; akawa ameketi pamoja na watumishi, anakota moto mwangani.*⁵⁵ *Basi wakuu wa makuhani na baraza yote wakatafuta ushuhuda juu ya Yesu wapate kumwua; wasione.*⁵⁶ *Kwa maana wengi walimshuhudia uongo, walakini ushuhuda wao haukupatana.*⁵⁷ *Hata wengine wakasimama, wakamshuhudia uongo, wakisema,*⁵⁸ *Sisi tulimsikia akisema, Mimi nitalivunja hekalu hili lililofanyika kwa mikono, na katika siku tatu nitajenga jingine lisilofanyika kwa mikono.*⁵⁹ *Wala hata hivi ushuhuda wao haukupatana.*
60 *Kisha Kuhani Mkuu akasimama katikati, akamwuliza Yesu, akisema, Hujibu neno? Hawa wanakushuhudia nini?*⁶¹ *Lakini akanyamaza, wala hakujibu neno. Kuhani Mkuu akamwuliza tena, akamwambia, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wake Mtukufu?*⁶² *Yesu akasema, Mimi ndiye, nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija na mawingu ya mbinguni.*

⁶³ *Kuhani Mkuu akararaa nguo zake, akisema, Tuna haja gani tena ya mashahidi?*⁶⁴ *Mmesikia kufuru yake; mwaonaje ninyi? Wote wakamhukumu kuwa imempasa kuuawa.*⁶⁵ *Wengine wakaanza kumtemeama mate, wakamfunika uso, na kumpiga makonde, na kumwambia, tabiri. Hata watumishi nao wakampiga makofi.*

⁶⁶ *Na Petro alikuwa chini behewani; akaja mmoja wa vijakazi wa Kuhani Mkuu,*⁶⁷ *akamwona Petro akikota moto; akamkazia macho, akasema, Wewe nawe ulikuwapo pamoja na yule Mnazareti, Yesu.*⁶⁸ *Akakana, akasema, Sijui wala sisikii unayoyasema wewe. Akatoka nje hata ukumbini; jogoo akawika.*⁶⁹ *Na yule kijakazi akamwona tena, akaanza tena kuwaambia waliosimama pale, Huyu ni mmoja wao.*
70 *Akakana tena. Kitambo kidogo tena wale waliosimama pale wakamwambia Petro, Hakika u mmoja wao, kwa sababu u Mgalilaya wewe.*⁷¹ *Akaanza kulaani na kuapiza, Simjui mtu huyu mnayemnena.*⁷² *Na mara jogoo akawika mara ya pili. Petro akalikumbuka lile neno aliloambiwa na Yesu, Kabla ya kuwika jogoo mara mbili, utanikana mara tatu. Na alipolifikiri, akalia.*

¹⁵ *1 Mara kulipokuwa asubuhi wakuu wa makuhani walifanya shauri pamoja na wazee na waandishi na baraza nzima, wakamfunga Yesu, wakamchukua, wakamleta mbele ya Pilato.*² *Pilato akamwuliza, Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi? Akajibu, akamwambia, Wewe wasema.*³ *Nao wakuu wa makuhani walikuwa wakimshitaki mambo mengi.*⁴ *Pilato akamwuliza tena akisema, Hujibu neno? Tazama ni mambo mangapi wanayokushitaki!*⁵ *Wala Yesu hakujibu neno tena, hata Pilato akastaajabu.*

⁶ *Basi wakati wa sikukuu huwafungulia mfungwa mmoja, wamwombaye.*⁷ *Palikuwa na mtu aitwaye Baraba, amefungwa pamoja na watu waliosanya fitina, na kufanya uuaji katika fitina ile.*⁸ *Makutano wakaja, wakaanza kuomba awafanyie kama vile alivyozoea.*⁹ *Pilato akawajibu, akisema, Je!*
*Mnataka niwafungulie mfalme wa Wayahudi?*¹⁰ *Kwa maana alitambua ya kuwa wakuu wa makuhani wamemtoa kwa husuda.*¹¹ *Lakini wakuu wa makuhani wakawataharakisha makutano, kwamba afadhali awafungulie Baraba.*¹² *Pilato akajibu tena akawaambia, Basi nimtendeje huyu mnayemnena kuwa ni mfalme wa Wayahudi?*¹³ *Wakapiga kelele tena, Msilibishe.*¹⁴ *Pilato akawaambia, Kwani, ni ubaya gani alioutenda? Wakazidi sana kupiga kelele, Msilibishe.*¹⁵ *Pilato akipenda kuwaridhisha makutano, akawafungulia Baraba; akamtoa Yesu, baada ya kumpiga mijeledi, ili asulibiwe.*

¹⁶ *Nao askari wakamchukua ndani ya behewa, ndiyo Praitorio (yaani, nyumba ya uliwali), wakakusanya pamoja kikosi kizima.*¹⁷ *Wakamvika vazi la rangi ya zambarau, wakasokota taji ya miiba, wakamtia kichwani;*¹⁸ *wakaanza kumsalimu, Salamu, Mfalme wa Wayahudi!*¹⁹ *Wakampiga mwanzi wa kichwa, wakamtemeama mate, wakapiga magoti, wakamsujudia.*²⁰ *Hata wakiisha kumdhihaki, wakamyua lile vazi la rangi ya zambarau, wakamvika mavazi yake mwenyewe; wakamchukua nje ili wamsilibishe.*

mst. 43–15:20a—Kusalitiwa kwa Yesu, kukamatwa, kuhojiwa mbele ya baraza, Petro kumkana, na kuhojiwa mbele ya Pilato

Sehemu hii ya injili ya Marko inaelezea kusalitiwa kwa Yesu na kukamatwa, kuhojiwa na kukataliwa mbele ya baraza la Kiyahudi, Petro kumkana Yesu, na kuhojiwa na kukataliwa mbele ya Pontio

Pilato. Jambo gumu ni kwamba, jamaa ya Kiyahudi ya Yesu walivunja taratibu zao wenyewe za kisheria kumhukumu Yesu kwa hila kama walivyokuwa wameazimia kabla kufanya, lakini alipokabidhiwa kwa Wamataifa, mtawala wa Kirumi, Pontio Pilato, hakuweza kuona kosa kwake lakini pamoja na hayo alitii shinikizo la kutoka kwa viongozi wa Wayahudi na kumtoa Yesu auwawe.

Mlinganisho wa injili nne unatupatia mtiririko kamili wa matukio tangu wakati wa kukamatwa kwa Yesu kule bustanini Getsemane hadi kifo chake na kuzikwa kwake (jedwali lifuatalo limechukuliwa kutoka kwa Powell 1954: 42-43):

Kukaribia usiku	Kukamatwa
Usiku wa manane hadi mchana	Yesu apelekwa kwa Anasi (Yoh 18:13, 19-24) Kuhojiwa mbele ya Kayafa na baraza la Sanhedrin (Marko 14:53-65 ; angalia Mat 26:57-68; Luka 22:54, 63-71)
Asubuhi: saa 6:00 (“ <i>mara baada ya machweo</i> ”)	“ <i>Kuwasiliana na wazee na waandishi na baraza lote</i> ” (Marko 15:1a ; angalia Mat 27:1)
Jua kutokeza: saa 6:00 - 9:00 (saa la 12 hadi la 3)	Kuhojiwa mbele ya Pilato (Marko 15:1b-5 ; angalia Mat 27:2, 11-14; Luka 23:1-5; Yoh 18:28-38a) Kuhojiwa mbele ya Herode (Luka 23:6-12) Yesu tena mbele ya Pilato, apigwa na kutolewa asulubiwe (Marko 15:6-20a ; angalia Mat 27:15-30; Luka 23:13-25; Yoh 18:38b-19:16)
9:00 - mchana (saa la 3-6)	Kuelekea Kalvari na kusulubiwa (Marko 15:20b-32 ; angalia Mat 27:31-44; Luka 23:26-33; Yoh 19:17-25)
Mchana saa - 3:00 (saa la 6-9)	Yesu masalabani (Marko 15:33-36 ; angalia Mat 27:45-49; Luka 23:34-44; Yoh 19:26-29)
3:00 (saa ya 9)	Kufa kwa Yesu na Kuzikwa (Marko 15:37-46 ; angali Mat 27:50-60; Luka 23:45-54; Yoh 19:30-42)

1. mst. 43-52—Kusalitiwa na kukamatwa kwa Yesu

Marko kumtaja Yuda kama “*mmoja wa wale kumi na wawili*” (**mst. 43**) kunatonesha msingi wa hila yake. Ni wazi Yuda alikuwa amepanga usaliti kwa kina: ilikuwa ni usiku na katika sehemu isiyo na watu ambako makutano wasingegekuwepo (makuhani wakuu walipaogopa); alikuja na wawakilishi wa viongozi wa dini waliokuwa na silaha katika tukio hilo wanafunzi au wengine walipinga (Petro kukata mtumishi wa kuhani mkuu kwa upanga) [**mst. 48**; angalia **Yoh 18:10**] alionesha busara za mipango ya Yuda; na kwa kuwa ilikuwa usiku, aliwapa viongozi wa dini ishara—kwamba angembusu atakayekuwa anamsaliti—ili kusiwepo na mashaka nani ndiye Yesu. Kiuhalisia, neno “busu” hapa ni *kattaphileō*, lenye maana ya “kukisi kwa shauku, kwa mguso, au kwa kurudia” (Zodhiates 1992: *kattaphileō*, 847). Maneno ya Yesu kuhusu maandiko kutimizwa (**mst. 49**) huenda yalirejea **Isa 53:12**, kama inavyooneshwa katika **Luka 22:37**, na pia yanaweza yakarejea **Zak 13:7**, ambayo Yesu alikuwa amenukuu awali wakati wa chakula cha mwisho cha jioni.

Mistari 50 unakazia kwamba “*wote walimwacha wakakimbia*.” Sasa Yesu alikuwa peke yake kabisa na mikononi mwa adui zake waliokuwa wakimtafuta siku nyingi kumuua. Wengi wanafikiri kuwa “*kijana*” ambaye “*alikimbia akiwa uchi*” (**mst. 51-52**) ni Marko mwenyewe. Marko alikuwa na nyumba kule Yerusalem (**Mdo 12:12**). Baadaye mapokea yalishikilia kuwa hiyo ilikuwa ndiyo nyumba ambako chakula cha mwisho cha Pasaka kilifanyikia (Cole 1989: 301). Swift anaeleza kuwa, “Hakuna sababu nzuri inayoweza kuoneshwa kwa kuwekea tukio hilo kumbukumbu isipokuwa kama lina msingi kwa kumbukumbu za mtu binafsi” (Swift 1970: 883).

2. mst. 53-65—Yesu kuhojiwa mbele ya baraza

Mistari 55 unarejea kusikilizwa au kuhojiwa Yesu mbele ya “*baraza lote*.” Ni wazi hii ilikuwa Sanhedrin kubwa zaidi. “Kulingana na *Mishnah*, kulikuwa na koti tatu za sheria kule Yerusalem: Baraka kuu la Sanhedrin, Baraza dogo la Sanhedrin na koti ya chini” (Powell 1954: 36). Baraza kuwa zaidi la Sanahedrin lilikuwa na wajumbe 71 na lilikuwa ndilo baraza pekee lililokuwa na mamlaka ya kuhukumu “*nabii wa uongo*” (Neusner 1988: 584, Sanhedrin §§1:5.A; 1:6.A). *Mishnah* ilikuwa imeandikwa mwanzoni mwa miaka ya 200 BK na kuweka kumbukumbu ya mapokeo yaliyotolewa kwa mdomo. Kama mapokeo na utaratibu kuhusiana na Sanhedrin ulikuwa unasimama mahali pake kama wakati wa Yesu, basi viongozi wa kidini walivunja utaratibu wao wenyewe ili wapate fursa ya kukamilisha matokeo walivoyakusudia: kumtoa Yesu asulubiwe na kuuwawa. Kwa mfano, *Mishnah* inasema kwamba, katika shauri la mauaji, majaji lazima “*wahoji shauri mchana na kulikamilisha mchana*” (Neusner 1988: 590, Sanhedrin §4.1.J) Katika mashauri ya

mauaji, majaji “wanafikia uamuzi wao wa mwisho siku hiyo hiyo, *lakini siku inayofuata kumtia mtuhumiwa hatiani*” (Ibid.: Sanhedrin §4.1.K); kwahiyu, “Hawahukumu [mashauri ya mauaji] jioni ya sabato au jioni ya sikukuu” (Ibid.: Sanhedrin §4.1.L) Aidha, “katika mashauri ya mauaji wananza na shauri la kumweka mtuhumiwa huru” (Ibid.: 589, Sanhedrin §4.1.E). Hakuna taratibu ye yote katika himo iliyo fumatwa. Hakika, **Mat 26:59** hata anasema, “*Basi wakuu wa makuhani na baraza yote wakatafuta ushuhuda wa uongo juu ya Yesu, wapate kumwua.*”

Jambo la kuvutia ni kwamba, ingawa baraza la Sanhedrin lenyewe lilikuwa likitafuta ushahidi wa uongo ili kumtia Yesu hatiani, bado lilifuata matakwa ya *Mishnah* kwamba “wakati [mashahidi] wanapopingana, ushuhuda wao haukulaliki” (Ibid.: 592, Sanhedrin §5.2.F). Hivyo, Marko anataja mara mbili kwamba ushahidi wa mashahidi “*haukupatana*” (**mst. 56, 59**). Ushuhuda wa mashahidi kwamba Yesu alisema ataharibu hekalu na kulijenga upya kwa siku tatu (**mst. 58**) ingeweza kutafsiriwa kama kukufuru na uchawi, ambapo adhabu ya yote mawili ni kifo. Hata hivyo, kama Frank Powell anavyosema, “Ndiyo ushahidi huu siyo walioutaka Sanhedrin. Walitaka kusikia ushahidi mzito zaidi kuliko huo ambao ungekuwa tishio kubwa la kuharibu hekalu au madai ya kulijenga katika siku tatu. Kwahiyu ni katika hali ya kiufundi sana kwamba ‘ushaidi ulitofautiana’ wangekataa kuukataa.” (Powell 1954: 68)

Katika hatua hii, hapakuwepo na shauri la Yesu kujibu. “Katika mazingira haya yote ilikuwa ni jukumu la Kuhani Mkuu kutangaza kwamba hakuna mashtaka yaliyofanywa na kwamba mtuhumiwa angewekwa huru” (Ibid.: 69). Kuhani mkuu hakufanya hilo. Badala yake, kuhani mkuu mwenyewe alimwambia Yesu “*wewe ndiye Kristo, Mwana mbarikiwa?*” (**mst. 61**) Yesu alijibu, “*ndiye, na utamwona Mwana wa Adamu akiwa amekaa katika mkono wa kuume wa mbinguni*” (**mst. 62**). Kama matokeo ya jibu la Yesu “*kuhani mkuu anapasua vazi lake na kusema, ‘tunahitaji ushahidi gani zaidi? mmemsikia akikufuru. Uamuzi wako ni nini? Na wote walimhukumu kuwa anastahili kuuwawa.*” (**mst. 63-64**)

Swali la kuhani mkuu lilikuwa haliko kisheria kabisa. Kwanza, mtu alikamatwa na hatia ya kukufuru “pale tu atakapokuwa ametaja jina la Mungu kikamilifu” (Neusner 1988: 597, Sanhedrin §7.5); pia, kwasababu kukufuru ilikuwa ni kosa la mauaji (**Law 24:10-16**), mashtaka ya kukufuru yalitakiwa yawe na mashahidi aghalau wawili au watatu kutoa ushahidi kwamba walimsikia maneno hayo kutoka kwa mtuhumiwa (angalia **Hes 35:30; Kumb 17:6; 19:15**; Neusner 1988: 597-98, Sanhedrin §§7.4.A, D; 7.5). Kwasababu hakuna shahidi aliyeshudia kwamba Yesu alikuwa ametenda kosa la kukufuru, kuhani mkuu hakuwa na haki ya hata kuibua swala la kukufuru au kuuliz`a swalii. Kuhani mkuu “hakuwa na mamlaka ya kutengeneza hitimisho la mahojiano kwa kumuliza mtuhumiwa” (Powell 1954: 70). Pili, swalii la kuhani mkuu lilikuwa pia siyo halali kisheria kwasababu “mahakama ilikuwa inajaribu kutuhumu kwa misingi kwamba alikuwa ametenda kosa hata *kabla hajaingia* kotini (jambo ambalo halikuwa na ushahidi) na siyo kwa *jambo lililosemwa na mtuhumiwa kotini*” (Powell 1954: 71).

Tatu, swalii la kuhani mkuu kiuhalisia lilikuwa ni tamko. James Edwards anasema, “katika lugha ya asili ya maneo ya Kigiriki yamewekwa katika muundo wa tamko lililokusudiwa liwe swalii (‘Wewe ni Kristo, Mwana wa aliyebarikiwa’). ‘Wewe’ lina nguvu, na Mwana wa mbarikiwa,’ namna ya Kiyahudi ya kutaja jina la Mungu, maana yake siyo nyingine zaidi ya ‘Mwana wa Mungu.’ Athari ni kuleta ukiri wa Kikristolojia katika mdomo wa kuhani mkuu!” (Edwards 2002: 446)

Jibu la Yesu kwa kuhani mkuu ni uthibitisho wake kwa kuunganisha na Mwana wa Adamu katika Dan 7:13 na Zab 110:1. Mwana wa Mungu hapa ni nafasi kamilifu ya kiungu na ya juu sana, ‘kukaa katika mkono wa kuume wa aliye juu’ . . . Kwa namna hivyo Yesu anathibitisha Uana wake mbele ya kuhani mkuu na kujidhihirisha kama anayekamilisha misheni ya kieskatolojia ya Mwana wa Mungu, uthibitisho unaomuweka katika bila kivuli cha mashaka katika nafasi ya Mungu.” (Ibid.: 447) Craig Blomberg anajadili kwanini madai ya Yesu ya kuwa “Mwana wa Mungu” katika muktadha huu ni muhimu: “Huyu ‘Mwana wa Mungu’ badala ya madai ya namna fulani kwamba alikuwa na namna ya umasihi, ndilo ambalo lingeliweza kumpelekeea kuhani mkuu kupasua vazi lake na kudai kwamba Yesu amekufuru [**mst. 63-64**]. Madai ya umasihi yalikuwa siyo kosa la mauaji; vinginevyo, Wayahudi kamwe wasingeweza kumpokea masihi! Lakini kudai kuinuliwa, Mwana wa Mungu wa kimbingu, ambaye ni Bwana na wa karibu na Baba mwenyewe mbinguni, yalivunja mipaka kwa yale ambayo Wayahudi waliowengi wangeliweza kuvumili yakihusishwa na binadamu wa kawaida.” (Blomberg 2007: 93) N. T. Wright anajadili sehemu nyingine na maana ya jibu la Yesu kwa Kayafa: “Hakuna kitu cha kawaida au kilichotamkwa kuhusu uhalali wa ‘Mwana wa mungu’ katika Daniel 7.14, 18 na 27. . . Anada kwa wawakilishi wa watu halisi wa Mungu. . . . Hivyo anatangaza kwamba Mungu wa Israeli atamtetea; na utetezi utahusisha kuharibiwa kwa Hekalu ambo limekuwa alama na kiwakilishi cha uasi dhidi ya Mungu.⁶⁵ . . . Mionganoni mwa maana zingine zinazotoa mwangwi kuto kana na

⁶⁵ Kwa namna ya mifano iliyo tumika kuonesha mwisho wa hekalu wakati alipolitakasa hekalu (**Marko 11:15-17**) na

matamko haya makali, kuna moja ambayo hakika Kayafa hakuiacha. Kama Yesu angehesabiwa kuwa mwakilishi wa kweli wa watu wa YHWH; na kama Kayafa, kwa wakati uliokuwepo anakaa kumhukumu; basi Kayafa mwenyewe, na utawala anaouwakilisha, umemulikwa na mwanga unaoonesha makosa yao. Mahakama yake imekuwa sehemu ya nguvu ya uovu inayomkandamiza Israeli wa kweli, na ambayo itaangushwa wakati YHWH atakapowahesabia haki watu wake. Kayafa, Kuhani mkuu, amekuwa Antiochus Epiphanes mpya, dikteta katili anayewakandamiza watu wa YHWH.⁶⁶ Sanhedrin ilichukua nafasi ya mnyama wa nne [angalia **Dan 7:7**] kwa Yesu Mwana wa Mungu. . . . Chumba cha mahakama kimependiliwa ndani nje: mfungwa anakuwa mtoa hukumu, mtoa hukumu mhalifu (Wright 1996: 524, 525-26)

Hapa, tena, kuhani mkuu na baraza la Sanhedrin hawakufuata taratibu za kisheria kama zilivyoandikwa katika *Mishnah*. “Katika matukio haya ilikuwa ni wajibu wao usioepukika kuchunguza ukweli au udanganyifu wa madai. Ni wazi hili walishindwa kulitimiza. Hapakuwa na uchunguzi wa madai ya Yesu kuwa Masihi na ‘Mwana wa Mungu.’. . . Mwenendo wa majaji walipopokea taarifa za kufufuka kwa Yesu, mbali na waliyotenda kabla na wakati wa shauri lenyewe, kunahalalisha kuamini kwamba *hapakuwepo na hali ye yeyote ile* ingweza kuandaliwa kukubali madai ya Yesu kuwa Masihi wa Israeli. Wakati habari za kufufuka zilipowafikia, badala ya kuweka juhudu kuwasiliana na Yesu ili kupata taarifa za ukweli, au kufanya maongezi ya kuthibitisha taarifa hizo—huenda kwa mtazamo wa kushikilia mahojiano mapya—walitoa pesa nyangi kwa maaskari walitotoa ushahidi, kama rushwa ya kuwashawishi waanzishe kisa cha uongo kwamba walipokuwa wamelala wanafunzi waliiba mwili wa Yesu.” (Powell 1954: 74, 89)

Zaidi ya hayo, kwa kuwa walimtia Yesu hatiani, walitakiwa waahirishe hukumu hadi siku iliyofuata. Wangeweza kuondoka wawili wawili na wasingeweza kula sana au kunywa mvinyo siku hiyo yote, na wangezungumzia swala hilo usiku kucha. Na siku iliyofuata wangeweza kuinuka na kuja mahakamani.” (Neusner 1988: 593, Sanhedrin §§5.5.A, B, C) Hawakufanya hivyo lakini, badala yake, walimtemea mate Yesu na kumpiga (**mst. 65**); hizo zilikuwa ni njia za kidesturi za kuonesha kumkataa mtu (angalia **Hes 12:14; Kumb 25:9; Ayb 30:10; Isa 50:6**). Kuhani mkuu kuchana mavazi yake ilihitajika mbele ya Sanhedrin wakati mtu alipoonekana kuwa na hatia ya kukufuru (Ibid.: 598, Sanhedrin §7.5.E). Mwenendo wote umejaa makosa: Sanhedrin wanakalia sheria na Yesu amekaa kuhukumiwa, lakini katika uhalisia Sanhedrin huvunja sheria na Yesu anaziheshimu. Ushahidi kwamba Sanhedrin wako kinyume na Yesu unakaribia kufikia mwisho kwa Yesu mwenyewe kuleta madai kwamba ni Mwana wa Mungu. Yesu anasimama mbele ya Sanhedrin, lakini baraza la Sanhedrin litasimama mbele ya Mwana wa Mungu atakaporudi katika utukufu wake. Sanhedrin wanadhihaki uwezo wa Yesu kutabiri, lakini utabiri wake wote hutimia. Zaidi ya yote, ni kuhani mkuu, na siyo Yesu, anayekufuru, kwasababu Yesu *ni* mwana wa Mungu. (Edwards 2002: 449) Kejeli moja ya mwisho ni kwamba kuhani mkuu anapasua mavazi yake ambayo, kama Samwel kuchana mavazi ya Sauli, kulimaanisha kuwa ukuhani wake ungechanwa na kuondolewa kwake, ambapo hata wakati wa kusulubiwa mavazi ya Yesu yalitunza yasichanwe vipande (**Yoh 19:23-24**), ikimaanisha ukuhani wake na ufalme wake usio na mwisho (**Ebr 2:17; 4:14-15; 10:19-22**).

3. **mst. 66-72—Kukana kwa Petro**

Uwepo wa Petro behewani unaonesha kuendelea kwake kumjali Yesu na kutaka kujuu yatakayomfika. Hata hivyo, kujali kwake kuhusu hali ya Yesu kulihatarisha kujijali yeye mwenyewe. Wakati kijakazi alipomwambia Petro kwamba ni mmoja wa wale waliokuwa na Yesu, Petro alikana, “*Sijui wala sisikii unayoyasema wewe*,” ni muhimu kwakuwa kulichukua “sura rasmi iliyojulikana ya kirabi katika kukana jambo kisheria (Lane 1974: 542; angali Neusner 1988: 637, Shabuot §8:3.B). Angeweza kusema ukweli au jibu lisiloeleweka (mf., “nadhani umekosea”), lakini badala yake alitoa tamko la kukana lenye nguvu kama lile ambalo mtu angetoa mahakamani. Mara mbili za kwanza za kukana kwake iliusu kwamba alikuwa pamoja na Yesu, lakini kukana kwake mara ya tatu alimkana Yesu mwenyewe (“*Simjui mtu huyu mnayemnena*,” **mst. 71**). Kwa nyongeza, kukana kwa Petro mara ya tatu kulikuwa ni zaidi ya kukana

uharibifu wa hekalu uliotabiriwa katika **Marko 13:2, 14-18**. Wakati wa kuhojiwa kwake, mashahidi wa uongo walishuhudia, “*Sisi tulimsikia akisema, Mimi nitalivunja hekalu hili lililofanyika kwa mikono, na katika siku tatu nitajenga jingine lisilofanyika kwa mikono*” (**Marko 14:58**). Hilo likikuwa ni nukuu iliyokosewa ya kile Yesu alicho sema. Katika **Marko 13:2** alitabiri kwamba hekalu litaharibiwa, lakini Warumi, na siyo yeye, wataliharibu. Katika **Yoh 2:19** alisema, “*Liharibuni hekalu hili, na kwa siku tatu nitalijenga*.” Alikuwa hasemi kwamba ataliharibu hekalu lakini aliwapa changamoto Wayahudi na “*alikuwa akizungumzia kuhusu hekalu la mwili wake*” (**Yoh 2:21**).⁶⁶ Mtawala wa Kigiriki Antiochus Epiphanes alitaala juu ya Yuda kuanzia mwaka wa 175–164 KK. Katika mwaka wa 167 KK alitoa dhabihu ya nguruwe katika madhabahu ya hekalu na alikuwa amepiga marufuku kisheria dini ya kiyahudi. Jambo hilo liliamsha mapinduzi ya Wamakabayo mwaka 167–164 KK. (Bartlett 1993: 476; Metzger 1957: 132)

kulikojulikana kuwa na nguvu kama vile mahakamani; **mst. 71** unasema kwamba “*Akaanza kulaani na kuapiza.*” uhara wa kujilaani na kuapa “*haumaanishi . . . kwamba alitumia maneno ya kukufuru;* lakini badala yake alithibitisha kiapo chake. Aliita ‘*anathema*’ ya Mungu juu yake mwenyewe kama kile alichosema hakikuwa kweli.” (Swift 1970: 883) *Anathema* inamaanisha kwamba mtu anajitolea kuharibiwa kwa ajili ya Mungu (Sept.: Hes. 21:1-3; Kumb. 13:16-18); kwahiyu, kuijingga katika laana na uharibifu, kulilaaniwa (1 Kor. 12:3; 16:22; Gal. 1:8, 9). Katika Rum. 9:3, kujitenga na Kristo na wokovu wake. Neno halioneshi adhabu iliyokusudiwa kama adibisho lakini inatolewa kama kitu cha kukataliwa kiungu. Ina maana ya kiapo kisichotenguliwa.” (Zodhiates 1992: *anathema*, 148-49). Petro asingemkana na kumkataa Yesu Kristo kwa nguvu zaidi ya vile alivyofanya katika **mst. 71**.

Tazama udanganyifu wa kutisha wa moyo wa mwanadamu (**Yer 17:9**) Na hali ya kujiangalia kibinagsi inayooneshwa na Petro: ameanza na “*wewe ndiwe Kristo*” (**Marko 8:29**) na kuishia na “*Simjui mtu huyu mnayemnena*” (**mst. 70**). Wakati wa kumkana mara ya tatu jogoo akawika mara ya pili (**mst. 72**); **Luka 22:61** inatuambia kwamba wakati huo Yesu aligeuka na kumtazama Petro, na Petro akakumbuka kwamba Yesu alikuwa amemtabiria angefanya hivyo, “*Na alipolifiki, akalia sana*” (**mst. 72**). Tunahitaji kujua kwamba kila mtu anabeba mbegu ile ile ya udanganyifu na kujijali kama Petro alivyoonesha. Haya yanaweza kudhihirishwa kwa njia mbalimbali, hasa katika nyakati za kujaribiwa na mateso. Hii ndiyo maana tunahitaji kuijandaa kukabiliana na majaribu na mateso kabla hayajatokea. Hata hivyo, kuanguka vibaya namna hiyo kwa Petro kunapaswa kutukumbusha kwamba mara zote kuna njia wazi ya kutubu, msamaha, na urejesho (angalia **Marko 16:7; Yoh 21:15-17**).

4. **mst. 15:1a—Mawasiliano mionganoni mwa wazee, waandishi na Sanhedrin**

Inawezekana kwamba kulia kwa jogoo mara ya pili “ni jambo la wakati maalumu [ambao] una maana halisi ya kupambazuka, tofauti na kulia kwa jogoo usiku wa manane; 15:1, ‘mara baada ya kupambazuka’, inakubaliana na hilo” (Cole 1989: 309). Ni wazi kwamba baraza kuu la Sanhedrin lilijaribu usiku. Kisha “*mara ya kupambazuka*” (**mst. 1**) kulikuwa na mukutano mwengine wa baraza kuu la la Sanhedrin, wakiwemo makuhani wakuu, wazee, na waandishi. Inawezekana viongozi hawa waliohudhuria waliweza kufikia 100. Powell anasema, “ingeweza kuonekana kwamba mukutano huu wa pili ulikuwa wenye makusudio ya kiushauri tu, uliofanyika kwa sababu moja ya kuamua njia ya kufaa ya kufanya maamuzi ya mahojiano ya awali ya baraza la Sanhedrin ya kumuua Yesu. . . . Hakika ilikuwa muhimu kwamba Kuhani Mkuu, kama kiongozi mkuu wa Wayahudi, alipaswa kuwa na hakika kwamba baraza lote la maafisa wa sheria linakubaliana na kile kilichokuwa kimetendeka.” (Powell 1954: 81-82) Mathayo anaelezea vizuri zaidi, “*Na ilipokuwa asubuhi, wakuu wa makuhani wote na wazee wa watu wakafanya shauri juu ya Yesu, wapate kumwua.*” (**Mat 27:1**).

Waliama kumpeleka Yesu kwa Liwali, Pontio Pilato kwa kuwa ni Pilato tu ndiye aliyekuwa na mamlaka ya kisheria ya kutoa hukumu ya kifo (angalia **Yoh 18:31**). Kulikuwa na sababu zingine za kumtoa Yesu kwa Pilato: “Mamlaka ya gavana yengekuwa muhimu katika kudhibiti sauti ambazo zingeweza kuibuka kwa niaba ya Yesu. Zaidi ya hayo, hukumu ya Rumi dhidi ya Yesu—na hasa ile aibu ya kufa kwa kusulubiwa—ingeliweza kuathiri sana jaribio la upande wa wafuasi wa Yesu kumsaidia.” (Edwards 2002: 457-58) Hata hivyo, ni wazi kuwa viongozi wa Kiyahudi waliama kutokekumwambia Pilato kuhusiana na kuhojiwa kwa Yesu na Sanhedrin. Huenda sababu ilikuwa kwamba “kama wangetoa habari za mahojiano yaliyofanya katika mahakama yao wenyewe, hali ya kuvunjwa kwa taratibu za kisheria ingeweza kuwa wazi kwa Pilato, kwa kuwa angeweza kujua kwamba kulingana na sheria za Kifarisyao mahojiano yasingeweza kufanyika usiku kisheria. Pilato angetaka kujua ni kosa gani Yesu ametiwa hatiani. Asingeshawishiwa na hatia ya kukufuru. Swali la ajabu lingeweza kuulizwa na hapo wasingeweza kuwa na jibu. Utata ungeweza kuibuka. Mara moja Pilato angeweza kutupilia mbali madai yao dhidi ya Yesu na kumweka Yesu huru. Ilikuwa bora wasiseme chochote kuhusu mahojiano waliyofanya na wakataja tu kwamba Yesu alikuwa amekamatwa usiku na sasa ilikuwa asubuhi mapema, analetwa mbele ya Pilato kuhojiwa?” (Ibid.: 83-84)

Hatimaye, kwa kuwa Pilato na maafisa wengine wa Kirumi hawakujali na wasingeliweza kusikiliza shauri lenye misingi ya sheria za kukufuru (angalia **Yoh 18:31; Mdo 18:12-16**), viongozi wa Kiyahudi walilazimika kutengeneza mashitaka mengine “ambayo yangemvutia Pilato, na ambayo *yangemlazimu* ayashughulikie. Na, zaidi ya kutoa shitaka dhidi ya sheria ya Kirumi, ilikuwa iwe ni ile inayohusiana na adhabu ya mauaji. Matukio yaliyofuata yanaweka wazi mipango ya utekelezaji wao. Watamshitaki Yesu kwa kosa la uhaini—Uhaini dhidi ya mtawala. Pilato angelazimika kuangalia madai hayo na asingeweza kuwarudisha kwa baraza la Sanhedrin. . . . Kama Pilato angeonesha dalili za kumfungua Yesu walikuwa na nafasi moja. Wangefanya watu waibue madai kuwa kama angemfungua Yesu basis i rafiki wa Kaisari, na wangemuingiza katika shauri gumu la jaribio la kumpindua Kaizari kule Yudea.” (Ibid.: 85)⁶⁷

⁶⁷ Craig Evans kwa kujiamini anatuambia kwamba kiuhalisia, Yesu hakuwa ametiwa hatiani na Pilato kwa “tuhuma ya uhaini.” Tukichukua kutoka katika kitabu cha mtawala Justinian, *Digesta* (530-533 BK), mkusanyiko wa sheria za

5. mst. 1b-20a—Yesu mbele ya Pilato na askari wa Kirumi

Pontio Pilato alikuwa liwali wa Yudea kati ya mwaka wa 26-36 BK. Kwa hali hiyo, alikuwa “amepewa na mtawala mamlaka kamili ya maisha na kifo. Wakati wa kusikiliza shauri la mtu ambaye siyo raia wa kirumi hakulazimika kufuata utaratibu wa mahakama ya Rumi. Alikuwa na mamlaka kamili mikononi mwake. Yeye alikuwa ndiye jaji na sheria kwa pamoja.” (Powell 1954: 101)

Katika **mst. 2**, swalii la Pilato kwa Yesu, “*wewe ni mfalme wa Wayahudi?*” ni kama swalii la Kuhani mkuu kwa Yesu katika **14:61**, kwamba, tamko lenye swalii lilimaanishwa (yaani, Wewe ni mfalme wa Wayahudi?”). “kama katika swala la kuhani mkuu, maneno ya Marko yanamfanya Pilato kuwa anayekiri bila kujulikana. Tena, hata midomo ya maadui wa Yesu bila kujielewa wanamkiri.” (Edwards 2002: 458) Msingi wa maswali ya Pilato ni unapatikana katika maelezo ya Luka kuhusu shauri, “*Wakasimama mkutano wote, wakampeleka kwa Pilato. Wakaanza kumshitaki, wakisema, Tumemwona huyu akipotosha taifa letu, na kuwazuia watu wasimpe Kaisari kodi, akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo, mfalme.*” (**Luka 23:1-2**) Itikio la Yesu, “*wewe wasema*” (**mst. 2**) unakazia Wewe. “siyo uthibitisho wa moja kwa moja, au vinginevyo Pilato mara moja angemtia hatiani kuuwawa. Na wala siyo kukana. Majibu ni ya mapendekezo, sawa na kusema, ‘ingekuwa vema kufikiria swalii.’” (Ibid.: 459) Makuhani wakuu walitambua kwamba madai yao kwamba Yesu alikuwa “*anawakataza kulipa kodi*” (**Luka 23:2**) yalikuwa ya uongo, kwakuwa walimjaribu Yesu katika hilo siku mbili tu kabla ya kukamatwa kwake, lakini Yesu alikuwa amekataa kuingia katika mtego wao (**12:13-17**; angalia pia **Mat 17:24-27**). Walijua pia kwamba madai yao kwamba Yesu alikuwa “*anasema kuwa yeye ndiye Kristo, mfalme*” (**Luka 23:2**) yalikuwa uongo. Alihukumiwa na Sanhedrin kwasababu *hakudai* kuwa alikuwa Masihi wa kisiasa lakini alidai kuwa yeye hakuwa Masihi (Kristo) wa kisiasa na Mwana wa Mungu. Hivyo, mashitaka yao yalikutana na ukimya wa Yesu (**mst. 3-5**), katika kutimiza **Isa 53:7**.

Yoh 18:33-38 anatoa maelezo kamili ya mabadilishano ya maneno kati ya Pilato na Yesu kwa kuheshimu swalii la Pilato: “³³*Basi Pilato akaingia tena ndani ya Praitorio, akamwita Yesu, akamwambia, Je! Wewe ni Mfalme wa Wayahudi?*” ³⁴*Yesu akamjibu, Wewe wasema hivi kwa nafsi yako, au watu wengine walikuambia habari zangu?* ³⁵*Pilato akajibu, Ama! Ni Myahudi mimi! Taifa lako na wakuu wa makuhani ndio waliokuleta kwangu. Umefanya nini?* ³⁶*Yesu akajibu, Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa.* ³⁷*Basi Pilato akamwambia, Wewe u mfalme basi? Yesu akajibu, Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu.* ³⁸*Pilato akamwambia, Kweli ni nini? Naye akiisha kusema neno hilo akawatokea Wayahudi tena, akawaambia, “Mimi sioni hatia yo yote kwake.”* Yesu alikuwa anasema, kuhusiana na hilo, “katika kujibu changamoto, Nakiri na kuepuka”; hivyo ni kusema, Nakubali nilidai na ninakubali mashtaka dhidi yangu; Nakubaliana kwamba madai hayo. *kwa maana niliyomaanisha*, ni kweli na hakika. Hata hivyo, sidai hivyo kwa *kwa maana wanayodai washitaki wangu*. Nakubali kwamba ninadai kuwa mimi ni mfalme, lakini siyo mfalme kwa maana inayowasilishwa na Makuhani Wakuu. Siletii madai ye yote ya kuwa mfalme, mpinzani wa Kaisari. Sina hatia ya uhaini dhidi ya mtawala. Nakubali na ninasimamia kwamba nimekuja kwa ajili ya ufalme lakini siyo wa kidunia.” (Powell 1954: 115-16)

Kwakuwa Pilato alijua Yesu alikuwa hana hatia (**mst. 14**) na ndio alikuwa tu ameletwa kwake kwasababu ya wivu wa Makuhani Wakuu (**mst. 10**), katika **mst. 6-15** Pilato anajaribu kumuachia Yesu kwa msingi wa desturi iliyokuwepo ya kumtoa mfungwa mmoja wakati wa sikukuu. Mpango wake uligonga mwamba, na hivyo, “*akitaka kuwapendeza makutano*” (**mst. 15**), Pilato anawafungulia muuaji, Barabba, na kumhukumu Yesu kuuwawa. Kama katika matukio mengi mengi katika maisha ya Yesu, kulikuwa na shida kubwa katika hili. Yesu alishitakiwa na viongozi wa Kiyahudi kuwa alikuwa mfalme wa kisiasa, mashtaka waliyojua yalikuwa uongo, na Pilato amemuhukumu kifo pamoja na kujua kuwa Yesu hana hatia, wakati huo huo, akimfungulia mtu aliyejua kuwa ana hatia. Zaidi ya hayo, “Pilato, anayeanza na kujaribu kumtoa Yesu katika hatari ya kifo, yeye mwenyewe anaishia kutaka auwawe. Kwa upande mwingine,

Kirumi unatokana zaidi na makabrasha kutoka katika karne ya kwanza na ya pili, Evans anaeleza hivi, “Hainekani kuwa Yesu alikuwa amehulkumiwa kwa “kosa la uhaini” ukizingatia uhaini ulivyojadiliwa katika (*maiestas*) katika *Digesta* 48.4.1–11. Mamlaka zilizonukuliwa ni pamoja na Ulpian, Marcian, Scaevola, na wengine. Karibu mifano yote iliyojadiliwa katika sura ya 4 ya kitabu cha 48 inahusiana na ukatili halisi kinyume cha serikali, “kinyume cha raia wa kirumi au dhidi ya usalama wao,” ikiwemo njama za mauaji dhidi za mtawala, njama au jaribio la mauaji dhidi ya maafisa wa Kirumi, kutengeneza jeshi, kushindwa kutoa amri ya kijeshi, kujiunga na adui wa mtawala, kuchocheara uundwaji wa uasi wenye silaha, kugeuza washirika kinyume cha Rumi, n.k. Yesu hakufanya lolote lililokaribia matendo kama haya.” (Evans 2016: “Roman Law”) Pilato mwenyewe alijua kwamba Yesu alikuwa anatolewa kwasababu za wivu na alitaka kumfungua (**Marko 15:10; Luka 23:20; Yoh 19:12; Mdo 3:13**). Aliegeme madai ya viongozi wa Kiyahudi kwasababu tu za kukubalika kisiasa.

Wayahudi ambao wajibu wao ni kutii, wanashinikiza mmatakwa yao na kushinda siku hiyo. Gavana kwa namna isiyo ya kawaida antawaliwa. Mtawala mwenye mamlaka (siyo kijina cha mtu wa kwanzakatika mst. 9 na 12) anapoteza uhuru kwa nguvu ambayo anaitawala, ambapo Yesu, mfungwa mkimya ambaye hana uthibiti wowote, anabakia kuwa halisi kwa kusudi la kiungu lililoamriwa, na hivyo yeye pekee anabakia kuwa huru hasa.” (Edwards 2002: 464) Maelezo ya Yoh ya muendelezo wa shauri huonesha kwamba viongozi wa kidini wa Kiyahudi na watu waliweka pembedi kumnyenyeka Mungu lakini walijitoa kumnyenyeka Kaisari. **Yoh 19:12** inasema, “*Na tangu hapo Pilato akatafuta kumfungua; lakini Wayahudi wakapiga makelele wakisema, Ukimfungua huyu, wewe si rafiki yake Kaisari; kila mtu ajifanyaye kuwa mfalme humfitini Kaisari.*” **Yoh 19:15** inaongeza, “*Pilato akawaambia, Je! Nimsulibishe mfalme wenu! Wakuu wa makuhani wakamjibu, Sisi hatuna mfalme ila Kaisari.*” **Mat 27:24-25** anahitimisha kwa kusema kwamba hata watu walikubaliana (sawa Petro kumkana Yesu mara ya tatu) kwamba damu ya Yesu’ iwe juu yao na juu ya watoto wao: “*Basi Pilato alipoona ya kuwa hafai lo lote, bali ghasia inazidi tu, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya mukutano, akasema, Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki; yaangalieni haya ninyi wenyewe. Watu wote wakajibu wakasema, Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu!*”

Jambo hili la kutisha haliishii hapo. Barabbas lina maana ya “mwana wa Baba”; Yesu ndiye Mwana wa kweli wa Baba. Hivyo, muuaji “mwenye aliyetiwa hatiani anaachiliwa, na katika nafasi yake asiye na hatia anahukumiwa kifo. Siyo jambo gumu kuona kinachoakisiwa katika mbadilishano huu wa wafungwa mbadilishano wa ondoleo la dhambi: ‘Tulipokuwa tungali wenyе dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu’ (Rum 5:8); ‘Kristo alikufa kwa ajili yetu, mwenye haki kwa wasio na haki’ (1 Pet 3:118).” (Ibid.: 461) Vivyo hivyo, ni kweli kuhusiana nasi: kama Barabba alivyokuwa mfungwa kama mtu wa vurugu na muuaji, vivyo tumefungwa na dhambi kama waasi dhidi ya Mungu na sheria yake na tumejiua kwa njia ya dhambi na, kupitia dhambi zetu, tulijiletea dhambi na kifo katika dunia yetu; zaidi sana, kama Barabba alivyokuwa amehukumiwa kifo kwa kosa lake, kadhalika tumehekumiwa kifo kwa dhambi yetu, na kama vile Barabba alivyokuwa hana alichowenza kufanya ili kuijokoa na kifo, lakini aliwekwa huru kwa neema ya Pilato na kifo cha Yesu, kadhalika hatuna tunachowenza kufanya kwa ajili ya wokovu wetu wenyewe lakini tumeokolewa kwa neema ya Mungu kabisa kwa kuwa Yesu alichukua adhabu ya dhambi zetu msalabani tuliyostahili ambayo Pilato alimhukumu.

Dihhaka na kupigwa kwa Yesu na askari (**mst. 16-20a**) inaturudisha nyuma alivyotendewa Yesu mapema akipokelewa na Sanhedrin (**14:65**). Zambarau ilikuwa rangi iliyokuwa ya gharama zaidi na ya kifahari katika siku za zama hizo na iliwakilisha utawala wa kifamlme (Ibid.: 466). Yesu alichukua mijeledi ya askari, mapigo, na kumdhihaki katika **Isa 50:6** na **53:5**.

MASWALI YA KUJADILI

1. Katika **14:62** Yesu alinukuu kutoka katika **Zab 110:1** na **Dan 7:13**, na akatumia mistari hiyo kwake mwenyewe. **Zab 110:1** ilinukuliwa au kuhusishwa na matukio mengi katika Agano Jipy, ikiwemmo **Mat 22:44; Marko 12:36, 16:19; Luk 20:42-43; Mdo 2:34-35; 1 Kor 15:25; Ef 1:20-22; Kol 3:1; Ebr 1:3** na **13; 8:1; 10:12-13; na 12:2**. Ni hoja au mambo gani ambayo yalitakiwa kuthibitshwa na moja ya mistari hii?
2. Ni kwa namna gani kuchana mavazi kwa Kayafa (**mst. 63**) kulikuwa ishara dalili ya kinabii”
3. Angalia vitendo vya Petro usiku ule: kujiuliza maswali kwake akiwa na wanafunzi wenzake (**mst. 19**); matamko yake ya uaminifu kamili (**mst. 29-31**); kulala kwake na kushindwa kumjibu Yesu (**mst. 33-40**); kukata sikio la mtumwa wa kuhani mkuu (**mst. 47**); kukimbia kwake (**mst. 50**); kumfuata Yesu kwa mbali hadi uani mwa kuhani mkuu (**mst. 54**); kukaa kwake na maafisa kuota motoa (**mst. 54**); kukana kwamba hata hakumjua Yesu (**mst. 66-71**); kulia kwake kwa uchungu (**mst. 72**). Haya yanakuambia nini kuhusu Petro?
- Ni kwa namna gani anafanana nawe?
4. Ni kwa namna gani Roho Mtakatifu anamtumia mjakazi? Jogoo? Roho amewahi kumtumia mtu asiye Mkristo, wanyama au hata vitu visivyo na uhai kuleta funzo lolote katika maisha yako?
5. Kama umewahi kutenda dhambi kwa namna ambayo ulijisikia kama vile Mungu hatakutumia tena, ulishindaje hisia hizo?

- Amekutumia tena?

6. Ni kwa njia gani maelezo kuhusu Barabba yanakuwa mfano au kitu kidogo kuhusu wokovu wetu katika Kristo?

7. Unafikiri ni kwa nini kwamba watu, baada ya kuona miujiza ya Yesu, kusikia mafundisho yake na kuingia kwake kishujaa Yerusalem na nyimbo za hosanna, kwamba sasa wanadai Yesi asulubiwe (**15:13-14**)? Kujibu hilo “*makuhani wakuu waliwachochea makutano*” (**mst. 11**), ingawa ni kweli, haitosh; swali ni *kwa nini walikubali kuchochewa*?

8. Pilato “[*ali]tamani kuwapendeza makutano*” (**mst. 15**), na hivyo kumtoa Yesu asulubiwe, hata kama alijua Yesu alikuwa hana hatia na kwamba ameshitakiwa kwa wivu tu (**mst. 10, 14**). Hakika, Pilato, hakuwa Mkristo. Tangu umekuwa Mkristo “umewahi kuambatana na makutano” na kutenda jambo ambalo ulijua lilikuwa ni kosa, kwasababu ya shinikizo kutoka kwa wengine?

- Kwanini ulifanya hivyo? (Tena, unasema kirahisi tu, “ulikuwa mwili” au “ibilisi alinifanya nitende hivyo,” kusema kweli haya siyo jibu; swali ni *kwanini uliruhusu kushawiwishiwa au kushinikizwa na wengine kufanya jambo ulilojua ni kosa?*)
- Matokeo yalikuwaje (kwako, ushuhuda wako kwa wengine, mahusiano yako na Mungu, kwa ujumla)?

9. Kwa upande mwingine, uliwhi *kupinga* kukubaliana na walio wengi?

- Umewahi *kupinga kwasababu wazi za Kikristo*?
- Ni kwa namna gani au kwanini uliweza *kupinga* shinikizo la wengine?
- Matokeo yalikuwaje?

10. Umewahi kudhihakiwa kwa kuwa Mkristo?

- Ulikabilianaje na hali hiyo?
- Kama hukukabiliana na hali hiyo ipasavyo, unafikiri ulipaswaje kukabiliana na hali hiyo?
- Kulikuwa na athari gani (kwako/kwa wengine)?
- Kwa upande mwingine, tunamdhihakije Yesu, pamoja na kudai kuwa ni mfalme wetu na kupiga magoti na kuinama mbele zake?

15:20b-47: ^{20b}Wakamchukua nje ili wamsulibishe. ²¹Wakamshurutisha mtu aliyekuwa akipita, akitoka mashamba, Simoni Mkirene, baba yao Iskanda na Rufo, ili auchukue msalaba wake. ²²Wakamleta mpaka mahali paitwapo Golgotha, yaani, Fuvu la kichwa. ²³Wakampa mvinyo iliyotiwa manemane, asiupokee. ²⁴Wakamsulibisha, wakagawa mavazi yake, wakayapigia kura kila mtu atwae nini. ²⁵Basi ilikuwa saa tatu, nao wakamsulibisha. ²⁶Palikuwa na anwani ya mashitaka yake iliyoandikwa juu, MFALME WA WAYAHUDI. ²⁷Na pamoja naye walisulibisha wanyang'anyi wawili, mmoja mkono wake wa kuume na mmoja mkono wake wa kushoto. ²⁸Basi andiko likatimizwa linenalo, Alihesabiwa pamoja na waasi.] ²⁹Nao waliokuwa wakipita njiani wakamtukana, wakitikisa-tikisa vichwa, wakisema, Ahaa! Wewe mwenye kulivunja hekalu na kulijenga katika siku tatu, ³⁰jiponye nafsi yako, ushuke msalabani. ³¹Kadhalika na wakuu wa makuhani wakamdhihaki wao kwa wao, pamoja na waandishi, wakisema, Aliponya wengine; hawezi kujiponya mwenyewe. ³²Kristo, mfalme wa Israeli, na ashuke sasa msalabani tupate kuona na kuamini. Hata wale waliosulibiwa pamoja naye wakamfyolea.

³³Na ilipokuwa saa sita, palikuwa na giza juu ya nchi yote, hata saa tisa. ³⁴Na saa tisa Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu, Elo, Elo, lama sabakthani? Maana yake, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? ³⁵Na baadhi yao waliosimama pale, walisema, Tazama, anamwita Eliya. ³⁶Na mmoja akaenda mbio, akajaza sifongo siki, akaitia juu ya mwanzi, akamnywesha, akisema, Acheni, na tuone kwamba Eliya anakuja kumtelemsha. ³⁷Naye Yesu akatoa sauti kuu, akakata roho. ³⁸Pazia la

hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini.³⁹ Basi yule akida, aliyesimama hapo akimwelekea, alipoona ya kuwa alikata roho jinsi hii, akasema, Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu.

⁴⁰ Palikuwako na wanawake wakitazama kwa mbali; mionganoni mwao alikuwamo Mariamu Magdalene, na Mariamu mama yao Yakobo mdogo na Yose, na Salome;⁴¹ hao ndio walifuatana naye huko Galilaya, na kumtumikia; na wengine wengi waliopanda pamoja naye mpaka Yerusalem.

⁴² Hata ikiisha kuwa jioni, kwa sababu ni Maandalio, ndiyo siku iliyo kabla ya sabato,⁴³ akaenda Yusufu, mtu wa Arimathaya, mst.ahiki, mtu wa baraza ya mashauri, naye mwenyewe anautazamia ufalme wa Mungu; akafanya ujasiri, akaingia mbele ya Pilato akauomba mwili wake Yesu.⁴⁴ Lakini Pilato akastaajabu, kwamba amekwisha kufa. Akamwita yule akida, akamwuliza kwamba amekufa kitambo.⁴⁵ Hata alipokwisha kupata hakika kwa yule akida, alimpaa Yusufu yule maiti.⁴⁶ Naye akanunua sanda ya kitani, akamtelemsha, akamfungia ile sanda, akamweka katika kaburi lililochongwa mwambani; akavingirisha jiwe mbele ya mlango wa kaburi.⁴⁷ Nao Mariamu Magdalene na Mariamu mamaye Yose wakapatazama mahali alipowekwa.

mst. 20b-47—Kusulubiwa, kufa, na kuzikwa kwa Yesu

Kusulubiwa, kufa, na kuzikwa kwa Yesu Kristo yote yalitimiza maandiko na unabii (angalia, hasa, **Mwa 3:15; Isa 53:3-12**). Maelezo mengi mionganoni mwa hayo yalitimizwa:

- Walimsukumizia Yesu mvinyo uliochacha (**mst. 23, 36**) yalitimiza **Zab 69:21b**, “*Nami nilipokuwa na kiu wakaninywesha siki.*”
- Kuinuliwa juu ya msalaba (**mst. 24**; angalia pia **Yoh 3:14; 12:32**) yalitimiza **Hes. 21:9**, “*Musa akafanya nyoka ya shaba, akaiweka juu ya mti, hata ikiwa nyoka amemwuma mtu, alipoitazama ile nyoka ya shaba, akaishi.*”
- Kufa kwa kusulubiwa (**mst. 24**) kulitimizwa **Kumb 21:23**, “*kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu*” (angalia **Gal 3:13**).
- Kuchomwa kama sehemu ya kusulubiwa na askari kumchoma Yesu ubavuni ili kuthibitisha kuwa amekufa (**Yoh 19:34**) kulitimizwa **Zab 22:16**, “*Kwa maana mbwa wamenizinguka; Kusanyiko la waovu wamenisonga; Wameniumiza mikono na miguu..*” **Isa 53:5**, “*Bali alijeruhwiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu,*” na **Zak 12:10**, “*nao watamtazama yeye ambaye walimchoma.*”
- Maombi ya Yesu, “*Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo.*” (**Luka 23:34**) yalitimizwa **Isa 53:12**, “*Walakini alichukua dhambi za watu wengi, Na kuwaombea wakosaji.*”
- Kugawana mavazi ya Yesu kwa kuyapigia kura (**mst. 24**) kunatimizwa **Zab 22:18**, “*Wanagawanya nguo zangu, Na vazi langu wanalipigia kura.*”
- Kusulubiwa katikati ya wanyang’anyi wawili (**mst. 27**) kunatimizwa **Isa 53:12**, “[Aka] hesabiwa pamoja na hao wakosao.”
- Watu kusimama pembeni, wakimtzama (**Luk 23:35**) kulitimizwa **Zab 22:17**, “*Naweza kuihesabu mifupa yangu yote; Wao wanantazama na kunikodolea macho.*”
- Kutikisa-tikisa vichwa na kumdhihaki *wakisema; wakitikisa vichwa vyao*” na *walinitikisia vichwa vyao.*”(**mst. 29-32**) kutimizwa **Zab 22:7**, “*Wote wanionao hunicheka sana, Hunifyonya, Zab 109:25, “Nami nalikuwa laumu kwao, Wanionapo hutikisa vichwa vyao.*”
- Matamko ya viongozi wa dini, “*Amemtegemea Mungu; na awokoe sasa, kama anamtaka; kwa maana alisema, Mimi ni Mwana wa Mungu.*” (**Mat 27:43**) kulitimiza **Zab 22:8**, “*Husema, Umtegemee Bwana; na amponye; Na awokoe sasa, maana apendezwa naye!*”
- Giza juu ya nchi yote (**mst. 33**) kulitimiza **Mwa 15:12, 17**, “*hofu ya giza kuu ikamwangukia.*” na “*ilikuwa giza nene.*”⁶⁸
- Yesu kulia, “*Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?*” (**mst. 34**) kunatimiza **Zab 22:1**, “*Mungu wangu, Mungu wangu, Mbona umeniacha?*”
- Yesu kusema, “*Naona kiu*” (**Yoh 19:28**) kunatimiza **Zab 22:15**, “*Nguvu zangu zimekauka kama gae, Ulimi wangu waambatana na taya zangu; Unaniweka katika mavumbi ya mauti.*”
- Yesu kulia, “*Baba mikononi mwako, naiweka roho yangu!*” (**Luka 23:46**) kunatimiza **Zab 31:5**, “*Mikononi mwako naiweka roho yangu; Umenikomboa, Ee Bwana, Mungu wa kweli.*”
- Mifupa ya Yesu kutokevunjwa (**Yohan 19:31-36**) kulitimiza **Kut 12:46**, “*wala msivunje mfupa wake uwao wote*” (angalia pia **Hes 9:12; Zab 34:20**).
- Mwili wa Yesu kuchomwa na askari ili kwamba “*maji na damu*” yatoke ubavuni mwake (**Yoh 19:34**) Kulitimiza **Zab 22:14**, “*Nimemwagika kama maji, Mifupa yangu yote imeteguka, Moyo wangu*

⁶⁸ Kwa majadiliano juu ya namna Mwanzo 15 ilivyotabiri kwa kina kusulubiwa, angalia hotuba, Menn, n.d.: “Mwa 15:1-18—Unabii mkubwa kabisa katika Biblia.”

umekuwa kama nta, Na kuyeyuka ndani ya mtima wangu.”⁶⁹

- Marafiki zake na wanafunzi wake kusimama mbali (**mst. 40**; angalia pia **Luka 23:49**) kulitimiza **Zab 38:11**, “*Wanipenda na rafiki zangu wanasmama mbali na pigo langu; Naam, walio karibu nami wamesimama mbali.*”
- Kuzikwa katika kaburi la Yusufu wa Arimathaya (**mst. 43-46**) kulitimiza **Isa 53:9**, “*Wakamfanya kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake.*”

1. **mst. 20b-32—Kusulubiwa kwa Yesu**

Kusulubiwa kwa Yesu hakukuwa tukio binafsi au la faragha. Badala yake, lilikuwa tukio la hadharani liliowahusisha maafisa wa serikali ya Kirumi, Viongozi wa Kiyahudi (Baraza la Sanhedrin), na watu wa kawaida, marafiki na maadui wa Yesu. Ryan Turner anaeleza kwa kifupi hivi, “Ingawa wanafunzi walimwacha Yesu, baadhi yao walikuwa bado wakishuhudia kwa mbali (Marko 14:54). Pia, walikuwepo wanafunzi wasiojulikana [huenda Yoh] ambaye Yesu, angali akiwa msalabani, amuamuru kumuangalia Mariamu (Yoh 19:26-27). Injili ya Luka inaeleza kwamba wakati Yesu akiwa anabeba msalaba, ‘. . . watu wengi walikuwa wakimfuata, wanawake, ambao pia walimuombolezea’ [**Luka 23:27**]. Kwa kuongezea kwa watu hawa walijotajwa tayari injili zina rejea sehemu mbalimbali kuwalusu viongozi wa Kiyahudi (Mt. 27:41; Marko. 15:31), Akida wa Kirumi (Mt. 27:54; Marko. 15:39; Luka. 23:47) na askari (Mt. 27:35; Marko. 15:24; Luka. 23:35; na Yoh 19:18, 23) ambao wote walishuhudia kusulubiwa kwa Yesu.” (Turner 2014: Eyewitness Sources) Mama yake Yesu mwenyewe, dada wa mama yake, na wanawake wenginealiowajua walikuwa mionganii mwa walioshuhudia kwa macho kusulubiwa kwa Yesu (**Yoh 19:25-27**). Zaidi ya haya, Yesu alipokuwa akiongozwa kwenda kusulubiwa, “*Wakamshurutisha mtu aliyejkuwa akipita, akitoka mashamba, Simoni Mkirene, baba yao Iskanda na Rufo, ili auchukue msalaba wake.*” (**Marko 15:21**). Timothy Keller anaeleza kuwa, “hakuna sababu ya mwandishi kuhusisha majina kama hayo isipokuwa kama wasomaji wanawajua au wanaweza kuwapata. Marko anasema, ‘Alexander na Rufus ni mashahidi wa kweli wa kile ninachowaambia, kama mnataka mwaweza kuwaauliza.’” (Keller 2008: 101) Kusulubiwa kwa Yesu ni moja ya matukio yaliyoshuhudiwa vema katika historia.⁷⁰

“Kusulubiwa kulikuwa ni adhabu iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya raia wasio wa Kirumi ambako ukatili uzidio ulitekelezwa kwa waia wa chini wasiweza kujitetea katika jamii—watumwa, wahalifu katili, na wafungwa wa vita. . . . Kuingiza aibu (Ebr 12:2) na maumivu makali ya kusulubiwa, wahanga waliuwawa hadharani kama maonesho, na wanaume kwa kawaida walisulubiwa wakiwa uchi, na kupigiwa kura kwa mavazi ya Yeus kunathibitisha hili.” (Edwards 2002: 468)⁷¹ Tunahitaji kukumbuka kwamba Yesu alitoa kila alichokuwa nacho kwa ajili yetu: kitu pekee alichomiliki (mavazi yake); uhai wake; na aibu yake (kumbuka kuwa mama yake mwenyewe alikuwepo na alimwona Yesu akiwa uchi, **Yoh 19:26-27**). Mara nyingi hatutambui kwamba kina cha dhambi zetu ni kikubwa mno kiasi cha kumnyang’anya Yesu *kila kitu* alichokuwa nacho, hata aibu yake ili tuondolewe dhambi. “Sababu halisi ya kifo cha Yesu kama wahanga wengine waliosulubiwa, kinaweza kuwa kiligubikwa na sababu nyingi na zinazohusiana kimsingi na mshituko unaotokana na kupoteza majimaji yanayozunguka seli za mwili au kupungua kwa damu, kushindwa kupata hewa ya kutosha kutokana na kuchoka, na labda hali mbaya ya moyo kushindwa kufanya kazi.” (Edwards, et al. 1986: 1463)

Kusulubiwa kwa Yesu Golgotha (**mst. 22**) kulikuwa nje ya lango la mji wa Yerusalem (**Yoh 19:20**).⁷² Hili, pia, lina maana muhimu ya kitheolojia na kutimiza maandiko. **Ebr 13:10-12** inasema, “¹⁰ *Tuna madhabahu ambayo wale waihudumiao ile hema hawana ruhusa kula vitu vyake.*”¹¹ *Maana wanyama wale ambao damu yao huletwu ndani ya patakatifu na kuhani mkuu kwa ajili ya dhambi, viviliwili vyao huteketezwa nje ya kambi.*”¹² *Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango.*” Mwandishi wa Waembrania anarejea **Kut 29:14** na **Law 4:12** ambayo wanabainisha kuwa miili ya mafahali iliyotolewa kwa ajili ya dhambi ilichomwa moto “*nje ya kambi.*”

⁶⁹ Uzito wa ushahidi wa kihistoria na kitabibu unaonesha kuwa Yesu alikuwa amekufa kabla ya kutobolewa ubavuni na kubaliana na mtazami uliozoleka kwamba mkuki, uliokuwa umechomwa katikati ya mbavu zake za kulia, inawezekana ultoboa siyo tu pafu la kulia lakini pia nyama ya moyo na hapo kufa kwake kuhakikiwa.” (Edwards, et al. 1986: 1463)

⁷⁰ Kwa ushahidi wa kibiblia na kihistoria unaoelezea hali ya kihistoria ya kusulubiwa, angalia Menn 2020: 23-29.

⁷¹ **Yoh 19:23-24** anabainisha kuwa askari walimvua Yesu vazi la nje na kanzu yake (vazi la ndan), jambo linalomaanisha kuwa alisulubiwa akiwa uchi.

⁷² “‘Golgotha’ ni neno lililotengenezwa kutoka katika neno la Kiaramaiki la fuvu, ambapo neno ‘kalvari’ limetoka katika tafsiri ya Vulgate ‘Calvariae locus,’ calva likiwa neno la Kilatini lenye maana ya fuvu” (Wessel 1984: 778).

Hes 19:1-3, 5, 9 inaendelea kueleza, “*Bwana akanena na Musa na Haruni, na kuwaambia,*

² *Hii ndiyo amri ya sheria Bwana aliyoagiza, akisema, Waambie wana wa Israeli wakuletee ng'ombe mke mwekundu asiye na kipaku, mkamilifu, ambaye hajatiwa nira bado; ³ nanyi mtamleta kwa Eleazari kuhani, naye atakwenda naye nje ya kambi, na mtu mmoja atamchinja mbele yake. . . . ⁵ Kisha mtu mmoja atamchoma moto huyo ng'ombe mbele yake; ngozi yake, na nyama yake, na damu yake, pamoja na mavi yake pia atachoma moto. . . . ⁹ Kisha mtu mmoja aliye safi atayazo majivu ya huyo ng'ombe, na kuyaweka yawe akiba katika mahali safi nje ya kambi, nayo yatatunzwa kwa ajili ya mukutano wa wana wa israeli, kuwa ndiyo maji ya farakano; ni sadaka ya dhambi.” **Ebr 9:12-14** anarejea dhabihu ya mtamba mwekundu, “¹² kwa damu yake mwenyewe [Kristo] aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele. ¹³ Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na masahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyononyiziwa wenye uchafu hutakasa hatu kuusafisha mwili; ¹⁴ basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai.” Wakristo wa kwanza walitambua umuhimu wa hili. Injili ya Barnaba (c. 70-131) inaeleza, “Lakinini ninyi mnafikiraje mfano, ambapo amri ilitolewa kwa Israeli kwamba watu wale, ambao dhambi zao ni dhahiri, watoe mtamba na wamchinje na kumchoma moto, na kisha wana wa Israeli wachukue majivu, na kuyaweka katika vyombo, na kuzonga pamba nyekundu ya kondoo kwenye mti (ona hapa kwa mara nyingine tena kuna mfanano wa msalaba na pamba nyekundu ya kondoo), na hisopo, na kwamba haya yakisha tendeka wana wa Israeli wanapaswa kuwanyunyizia watu mmoja baada ya mwingine, ili kwamba waweze kutakaswa na dhambi zao? Elewa jinsi inavyoletwa kwa uwazi kwako; mtamba ni Yesu, watu wanaomtoa, wakiwa wenye dhambi, ndio wanaomtoa kwa ajili kuuwawa. Baada ya hili siyo watu tena (wanaotoa); utukufu siyo wa wenye dhambi tena.” (*Epistle of Barnabas* 1989: 8:1-2)*

Kulia kwa Yesu, “*Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?*” (**mst. 34**) kumesheheni maana. Hukumu ya dhambi ni kutengwa na Mungu milele, kunakojulikana kama kuzimu. Kuzimu inaelezwa sehemu mbalimbali katika Biblia kama “*giza la nje*” (**Mat 25:30**). Giza la angani wakati Yesu alipokuwa msalabani (**mst. 33**) ulikuwa ni ishara ya hukumu juu ya dhambi ambazo Yesu alikuwa akizibeba. Giza hilo liliwakilisha giza lenyewe la nje la kuzimu.⁷³ Kwa kuwa uhalisia wenyewe wa kuzimu ni kutengwa na Mungu, Yesu alipolia akiwa msalabani, “*Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?*” alikuwa kipitia uzoefu wa kuzimu. Kwa maelezo, kuzimu itadumu milele. Yesu hakubeba tu umilele wa kuzimu, lakini mamiliioni ya umilele kuzimu, yote yakiwa yameletwa pamoja juu yake wakati alipokuwa msalabani. Hilo liko nje ya uwezo wetu kulielewa, lakini linafunua kwamba kile ambacho Yesu alipitia msalabani hakifikiriki. Hiyo ilikuwa ndiyo gharama ya kutukomboa kutoka katika adhabu ya dhambi zetu.

Upande mwingine wa kulia kwake, “*Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?*” kunatuhakikishia kusikilizwa. Kulia kwa Yesu kutokea msalabani kunabainisha utii wake kamili (**Flp 2:8**). Katika maisha yake yote hapa duniani Kristo mwenyewe kwa kurudia alisema kuwa hakufanya lolote kwa kulianzisha yeche kila alifanya tu yale ambayo Baba alimtaka kufanya (**Yoh 5:19, 30; 6:38; 8:28; 12:49; 14:10**). Kulia kwake “*Mungu wangu*” kunabainisha ukaribu wa kimahusiano aliokuwa nao na Baba. Pale msalabani, Yesu alistahimili mateso yasiyo na mwisho na laana ya Baba (**Gal 3:13**); na bado aliendelea kumtii Baba katika njia yake yote hadi mwisho. Kulia kwake ni nukuu ya **Zab 22:1**, zaburi ya Daudi, ambaye alikuwa nabii (angalia **Mdo 2:30**). Katika kunukuu zaburi hiyo katika matukio hayo, Yesu alikuwa anasema kwamba **Zab 22:1** ilikuwa ikinena na kutimizwa katika kile alichokuwa akitenda msalabani. Yesu alijua kabisa nini kilikuwa kinaendelea. Kiuhalisia, alikuwa anasema, “Nakuamini Baba, Naamini mpang’ wako kwa ajili ya wokovu wa nafsi, na ninakupenda sana kiasi kwamba nitakutii kikamilifu, hata kama itamaanisha kutengwa kabisa nawe na kulazimika kuvumilia kuzimu yote ya dhambi za wanadamu.”

Yesu alifanya yote kwa kujitolea (**Yoh 10:18**) kwasababu tulikuwa wa thamani kwake. Kama **Isa 53:11** anavyosema, “*Ataona mazao ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika.*” Kile Kristo alichofanya msalabani kinaonesha, kwa namna fulani hakuna dini nyingine hata inayokaribia, ni jinsi gani watu wana thamani machoni pa Mungu. Timothy Keller anahitimisha, “Yesu aliteseka zaidi kuliko nafsi ye yote ya mwanadamu kule kuzimu, na bado alitutazama na kusema, ‘ilistahili.’ Nini zaidi kinaweza kutufanya tujisikie tunapendwa na kuthaminiwa? poteze, na hakuna mwokozi mwingine aliywahi kutupenda kwa gharama ya namna hiyo.” (Keller 2009: sec.4)

Kama ilivyo katika maeneo mengine ya maisha, mlinganisho wa injili nne unatoa maelezo kamili ya maandishi aliyo kuwa ameandika Pilato ambayo yalipigiliwa juu ya msalaba wa Yesu. Marko anaeleza kilichokuwepo, “*Mfalme wa Wayahudi*” (**mst. 26**); Mathayo ana, “*Huyu ni Yesu, Mfalme wa Wayahudi*”

⁷³ Gruenler anatzamisha mfanano ufuatao wa giza: “Katika Injili ya Marko kifo cha Yesu (**15:33-41**) kinaonekana kubeba na kutimiza dhamira ya Pasaka na kutoka. Janga la giza lililowaangukia Wamisri kabla ya Pasaka (Kutoka 10:21-22) linaanguka juu ya nchi ya Wayahudi na Yesu anakuwa Pasaka wa mwisho na mbadala wa laana (mst. 33; cf. Gal. 3:13).” (Gruenler 1989: 797)

(**Mat 27:37**); Luka anasema, “*Huyu ndiye Mfalme wa Wayahudi*” (**Luka 23:38**); Yoh anaeleza, “*Yesu wa Nazarth, Mfalme wa wayahudi*” (**Yoh 19:21**). Haya hayapingani. Wakati yote yanapokuwa yametazamwa vema, matamko kamili yanasmeka. “*Huyu ni Yesu wa Nazareth, Mfalme wa Wayahudi*” Jambo la kuvutia, ingawa anaweza akawa hakutambua hivyo, Pontio Pilato alikuwa anakiri, kwa maandishi ya (Kiaramaiki, Kilatini, na Kigiriki, **Yoh 19:20**) ili watu wote waone, ukweli kwamba Yesu alikuwa nani hasa. Hii ndiyo maana makuhani wakuu walikataa isiandikwe hivyo, Pilato hakubadilisha, akisema, “*Nilichoandika nimeandika*” (**Yoh 19:22**).

2. mst. 33-41—Kifo cha Yesu

Kifo cha Yesu (**mst. 37**) “siyo kwamba alifikia mwisho ila kwa sababu za matukio mawili ya kipekee: Kupasuka kwa pazia la Hekalu (**mst. 38**) na ukiri wa akida (**mst. 39**). Matukio haya mawili yana maanisha kwamba kifo cha mateso ya Mwana wa Mungu hakikuwa tukio la kufikia mwisho bali tukio la utimilifu wa kiungu na ufunuo.” (Edwards 2002: 477)

Kulikuwa na mapazia mawili (au vitambaa) katika hekalu: moja lilikuwa mbele ya patakatifu (sehemu kubwa ya hekalu) patakatifu pa Patakatifu (**Ebr 9:1-5**). Mwanahistoria wa karne ya kwanza Josephus aliona maana ya kipekee katika pazia la kwanza la hekalu. Ilikuwa ni sura ya dunia yote. . . . Pazia hili lilikuwa pia limepambwa lote mambo ya mbinguni, isipokuwa kwamba kati ya ishara [kumi na mbili], zilizowakilisha viumbe” (Josephus 1987b: 707 [*Wars*: 5.212-14]; angalia **Kut 26:31; 2 Nyak 3:14**). Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu palitenganishwa na vitambaa vya pazia la blue, zambarau, na nyekundu (**Kut 26:31-37; 2 Nyak 3:14**). Hieleweki vema ni pazia lipi au kitambaa Marko anakzungumzia. Neno la Kigiriki la pazia katika **mst. 38**, *katapetasma*, ni neno sawa na lililotumika kwa pazia lililosimama mbele ya Patakatifu pa Patakatifu katika **Ebr 6:19; 9:3**; na **10:20**, nan i neno hilo hilo lililotumika katika biblia ya Septuagint (LXX) kwa Pazia la Patakatifu pa Patakatifu **Kut 26:31-37**, Ambapo LXX imetumia neno lingine kwa pazia lililokuwa mbele ya Patakatifu. Hilo linatuambia kwamba pazia linalohusika lilikuwa ni lili lililokuwa limewekwa mbele ya Patakatifu pa Patakatifu. Kwa upande mwingine, pazia la nje lilikuwa ni lile lililoonekana kwa watu wote, na **mst. 39** na **Mat 27:51-54** unatuambia kwamba inawezekana akida aliona pazia likipasuka. Sehemu nyingine ya pekee mbali na **mst. 38** ambapo Marko anatumia neno *schizein* (“kupasuka”) ni wakati wa ubatizo wa Yesu (**1:10**) ambapo “kupasuka kwa mbingu kulimfunua Yesu kuwa ndiye Mwana wa Mungu” (Edwards 2002: 478). Kwamba pazia la nje liliwakilisha ulimwengu na mbingu inaonesha kuwa Marko anaunganisha na **1:10** kupasukakatika kwa pazia la nje katika **mst. 38**, ikimaanisha “katika ubatizo na kifo cha Yesu maskani ya mbingu na ya dunia ya Mungu vimefunguliwa kwa wanadamu” (Ibid.: 479)

Bila kujali ni pazia gani lilihusika, maana ni ile ile. Kupasuka kwa pazia kuliwakilisha kuharibiwa kwa hekalu na uhuru wa kuingia kwa Mungu ambao sasa watu wanao kwa njia ya Yesu. Matokeo ya dhabihu ya Yesu, sasa tunao “*tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu . . . kwa njia ile aliyo tuanzia iliyo mya, iliyo hai, ipitayo katika paziau*” (**Ebr 10:19-20**). Kusema kweli, **Ebr 10:20** hasa inasema kwamba “*Pazia*” ni “*mwili wake*.” Kwa maneno mengine, hekalu lilikuwa likimzungumzia Kristo wakati wote. “Siyo kwa kiwango ambacho Kristo anatimiza kile kilichomaanishwa na hekalu lililokuwepo. . . . Kristo ndiye hekalu la kweli, nuru ya kweli ya utukufu, maana ya kweli, mzabibu wa kweli. Kuwepo kwa ilikyo kweli kunafunika iliyo kwa mfano. Pazia la hekalu lililofanywa kwa mikono limeharibiwa, kwa kuwa lilichokuwa linawakilisha kimefika.” (Clowney 1972-73: 177, 183) Kwa maneno mengine, ijapokuwa jengo la hekalu liliendelea kusimama hadi lilipoharibiwa mwakawa 70 BK, wakati wa kifo chake msalabani, Yesu alizindua Agano Jipyambalo lilifanya Agano la Kale na kila kilicholihusu kwa habari ya ibada, ikwa ni pamoja na hekalu, vilikuwa vimepitwa na wakati (**Ebr 8:13**). Mfumo mzima wa hekalu hauna kazi tena; Yesu ndiye kilele cha ukweli wa kiroho. **Ebr 8:1-10:22** inatuambia kwamba hekalu halisi ni la mbinguni na hekalu la mfano ni la duniani. “Hata Waembrania 9:8-9 hurejea ‘hema ya kukutania’ ya zamani (hasa, patakatifu) kama ‘alamu’ ya hema ya kukutania ya siku za mwisho (mfano, katika 9:11) ili kuelewa kwamba hema ya kukutania ya awali haikuwa ndiyo halisi” (Beale 2004: 295). **Ebr 4:14-5:10; 7:1-10:22** inamueleza Kristo kama kuhani mkuu na hema ya kukutani/hekalu. **Ebr 10:12, 14** inasema, “*alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu, . . .*¹⁴ *Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.*” Na “*yeye, kwa kuwa akaa milele, anao ukuhani wake usioondoka*” (**Ebr 7:24**). Yesu Kristo ndiye njia pekee ya kumfikia Mungu. Hii ndiyo maana msalaba na kupasuka kwa pazia kunaleta maana.

Katika **mst. 39** akida anakiri, “*Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu.*” Wakati Pilato anakiriri kwamba Yesu “*alikuwa mfalme wa Wayahudi*” (**mst. 26**) na matamko ya Kayafa katika **14:61**, “*Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mbarikiwa*” yote yalikuwa kweli, yote yalitajwa kwa kudhifak. Tamko la Akida lilikuwa ukiri wa kweli. Kusema kweli, “Akida alikuwa mtu wa kwanza katika injili kumkiri Yesu kama

Mwana wa Mungu, ukiri wake unathibitishwa na shauku yake—mateso yake na kifo chake msalabani. . . . Mawazo ya kuteseka kwa Yesu msalabani, ambayo kwa hakika yanapingana na matarajio ya umasihi wa Kiyahudi na ‘mtu wa kiungu’ wa Kiyunani, yanageuka kwa njia ya Mungu, dirisha la moyoni na maana ya Yesu, maana ambayo inaeleweka kutokana na ukiri ‘Mwana wa Mungu.’” (Edwards 2002: 479-80).⁷⁴

Mistari 40-41 inayomzungumzia mwanamke ambaye amemfuata na kumhudumia Yesu inafaa kuangaliwa, hasa kumfuata mara baada ya ukiri wa akida. Akida alikuwa Mmataifa mpagani; kwa hali hiyo alikuwa ni mtu “wa nje” na alihesabiwa kuwa “najisi” na Wayahudi walio wengi. Wanawake kwa kawaida walitengwa na kuhesabiwa, wasio na uwezo, “raia wa daraja la pili” na Wayahudi wengi. Tunachoambwi na hili ni kwamba mara nyingi ni wale walitengwa na walio nje ambaeo hupata imani kubwa zaidi na ambaeo miongoni mwao Mungu hutenda kazi kubwa.

3. mst. 42-47—Kuzikwa kwa Yesu

Kuzikwa kwa Yesu, na matukio yanayozunguka tukio hili, ni muhimu, kwasababu yanathibitisha kwamba hakika Yesu alikuwa, siyo “alikaribia kufa” au alipoteza fahamu au alizimia. Kwasababu Yesu alikuwa kama saa 9:00 mchana, Yusufu wa Arimathaya alikuwa na kama saa tatu hivi kuhakikisha kuwa Yesu anazikwa kwa wakati, kwa kuwa **Kumb 21:22-23** iliweka wazi kwamba mtu “aliyeangikwa mtini” anapaswa kuzikwa siku hiyo hiyo (na siku za Kiyahudi zilianza kwa kuzama jua au saa 12:00 jioni). Mshangao wa Pilato kwamba tayari Yesu alikuwa amekwisha kufa unaeleweka, kwakuwa wakati mwingine mhanga wa kusulubiwa aliweza kukaa kwa siku kadhaa msalabani kabla ya kukata roho. Kuutoa mwili kwa mtu mwingine zaidi ya mwanafamilia au kuutoa mwili mara zote hakukuwa jambo la kawaida. Hivyo, Pilato alimtaka akida athibitishe kuwa Yesu alikuwa amekufa kweli (**mst. 44**). Kama Yesu hakuwa amekufa kweli, lakini akida alitoa taarifa kwa Pilato kwamba amekufa, angekuwa amevunja utaratibu na angekuwa anamdaganya kamanda wake na huenda angelazimika kulipa kwa maisha yake mwenyewe. Matokeo yake, ni jambo lisilo na mashiko kupinga kuwa Yesu hakuwa msalabani.

Miili ya wafu waliokuwa wahalifu ilikuwa ni mali ya serikali ya Rumi. Miili mingi ya waliosulubiwa iliruhusiwa kubaki kwenye misalaba yao kama onyo kwa wengine. “Aibu ya kusulubiwa iliingia kwa kina zaidi ya kuwa uchi, kuteswa, na kudhilihakiwa. Mara nyingi, miili iliyosulubiwa hata haikuzikwa. Badala yake, siku iliyofuatia baada ya aliYesulubiwa kufa midomo ya tai na meno ya mbwa mwitu ilichana chana ule mzoga vipande vipande na vikasambaa kila mahali.” (Jones 2012: n.p.) Hata hivyo, haikufanyika hivyo kila wakati. Mwanahistoria wa karne ya kwanza Josephus anaeleza kuwa “wayahudi walichukulia jambo la kuzika watu kwa umakini, kwamba waliwateremsha wale waliokuwa wamehukumiwa na kusulubiwa, na kuwazika kabla ya jua kuzama” (Josephus 1987b: 679 [*Wars*: 4.314]). Kwa kuongezea **Kumb 21:22-23**, *Mishnah* inasema kwamba hata wauaji waliokuwa wamesulubiwa walizikwa (Neusner 1988: 595, Sanhedrin §§6:5-6). Baba yake Josephus anaeleza kuwa Warumi “hawawalazimishi wanaowatawala kuvunja sheria za nchi zao” ikiwemo sheria “ya kutokumuacha yeyote bila kumzika” (Josephus 1987c: 798 [*Against Apion*: 2.73, 2.211]). Graig Evans anasema, “Mchakato uliopelekea kusulubiwa kwa Yesu . . . ukianzishwa na baraza la Kiyahudi. Kwa mujibu wa sheria na taratibu wakati baraza la Kiyahudi (Sanhedrin) lilipomhukumu yeyote kifo, kwa namna yeyote ile iliwaangukia baraza kwamba wahakikishe mtu huyo anazikwa. Hiyo ni nafasi aliyokuwa ameshika Yusufu wa Arimathaya, mmoja wa wajumbe wa baraza (Marko 15:43).” (Evans 2016: “Concluding Remarks”) Evans anahoji sheria ya Kirumi na mwenendo. Kitabu cha *Officio Proconsulis (Duties of Proconsul)* kilichoandikwa na mwanasheria wa Kirumi Ulpian (c. AD 170–223) kina maelezo, “miili ya wale waliohukumiwa kufa jamaa zao wasizuiliwe”; Evans anaangalia, “Ulpian anasimamia wazo lake kwa kulisemea kwamtawala mkuu Augustus (aliyetawala miaka ya 31 KK – 14BK), ambayo ilielezwa katika wasifu wake ulioandikwa karibu na maisha yake. Ulpian anaemdelea kusema kwamba ‘miili ya wale walioadhibiwa itazikwa tu ikiwa ombi hilo litawasilishwa na kibali kutolewa.’” (Ibid.: “Roman Law”) Hivyo, “kuzikwa kwa miili ya waliouwawa kwa njia hii kuliruhusiwa katika himaya ya Rumi wakati wa Yesu. Ilikuwa ni jambo lililozoleka la utawala wa Ki-augustino na ilikuwa ni mawazo ya Ulpian ambaye alishi karne mbili baadaye.” (Ibid.) Kwahiyio haishangazi kwamba Pilato alitoa mwili wa Yesu kwa Yusufu wa Arimathaya.

Kaburi ni mihimu. “Limechongwa kwenye mwamba, na akaviringisha jiwe mbele ya mlango wa kaburi” (**mst. 46**; angalia pia **16:4**, “lilikuwa kubwa sana”). Kiasi kwamba hakuna yeyeto angeliweza kuchimba atoke au aingie. N. T. Wright anaeleza kwamba, “Kutajwa kwa maziko ya Yesu [**1 Kor 15:4a**] kunaweza tu kupata heshima kama kwa kifupi katika simulizi za kidesturi kama maziko yenewewe

⁷⁴ Ingawa katika Kigiriki “Mwana wa Mungu” hakubebi kiambishi kinachotoa hakikisho ya jina, jambo ambalo linapelekea baadhi kufikiri akida ilimaanisha *mwana* kuliko *Mwana* wa Mungu, Edwards anaeleza yote matumizi yote katika sarufi za Kigiriki na sababu zingine “Mwana wa Mungu” ndiyo usomaji sahihi (Edwards 2002: 480-81).

